2000/=

# CHUO KIKUU CHA KENYATTA
# IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

## DHULUMA DHIDI YA WATOTO KATIKA RIWAYA ZA KISWAHILI

NA
PETER N. KAVURIA

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

MEI 2008

Kavuria,Peter N.
*Dhuluma dhili ya watoto katika riwaya*
2008/330258

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

-----------------------------------------------

PETER N. KAVURIA

(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo hiki.

-----------------------------------------------

DKT. C. M. NDUNGO.

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

NA

-----------------------------------------------

DKT. E. MASINDE

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## TABARUKU

Kwa bibi yangu mpendwa Dalphine Wachuka .

Kwa watoto wangu Evalyn Wanjiru, Bernard Mugendi,na Junias Wachira.

Kwa wazazi wangu Bernard Kavuria na Rael Mairu, na wazazi wote wa karne hii.

## YALIYOMO UKURASA

Mada ---------------------------------------------------------------- i

Ikirari ---------------------------------------------------------------- ii

Tabaruku ---------------------------------------------------------------- iii

Yaliyomo ---------------------------------------------------------------- iv

Shukrani ---------------------------------------------------------------- viii

Ikisiri ---------------------------------------------------------------- ix

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI WA TASNIFU**

1.0 Ufafanuzi wa dhana muhimu -------------------------------- x

1.1 Utangulizi ---------------------------------------------------------- 1

1.2 Swali la utafiti ------------------------------------------------------ 4

1.3 Maswali ya utafiti ---------------------------------------------- 5

1.4 Malengo ya utafiti ---------------------------------------------- 5

1.5 Sababu za kuchagua mada -------------------------------- 6

1.6 Upeo na mipaka ya Tasnifu ------------------------------------ 7

1.7 Misingi ya nadharia ---------------------------------------- 10

1.8 Udurusu wa tafiti za awali ---------------------------------------- 14

1.9 Ukusanyaji wa data ---------------------------------------------- 19

1.10 Uchanganuzi wa data ------------------------------------------ 20

## SURA YA PILI

## AINA ZA DHULUMA, ZINAVYOBAINIKA NA SABABU ZAKE


2.0 Utangulizi ---------- 21

2.1.1 Kujeruhiwa kimwili ---------- 22

2.2.2 Dhuluma za kihisia ---------- 26

2.2.3 Unyanyasaji wa kimapenzi ---------- 34

2.1.4 Kutowatunza watoto ---------- 37

2.2 Sababu za utekelezaji wa dhuluma dhidi ya watoto---------- 41

2.2.1 Ufuasi wa tamaduni za kijadi ---------- 41

2.2.2 Mfumo wa kuumeni ---------- 44

2.2.3 Kufurahisha nafsi zao ---------- 49

2.2.4 Kukata tamaa ---------- 50

2.2.5 Ubinafsi ---------- 53

2.2.6 Tabia mahsusi ya mdhulumu ---------- 54

2.2.7 Utegemezi ---------- 57

2.3 Hitimisho ---------- 59


## SURA YA TATU

## UTEKELEZAJI WA DHULUMA NA ATHARI ZAKE


3.0 Utangulizi ---------- 61

3.1.1 Wazazi ---------- 61

3.1.2 Walezi ---------- 63

3.1.3 Watoto ---------- 65

3.1.4 Waajiri ---------- 67

3.1.5 Waalimu ---------- 68

3.1.6 Walinda haki ---------- 69

3.2 Athari za dhuluma katika maisha ya watoto

3.2.1 Majeraha ya mwili ---------- 71

3.2.2 Huzuni ---------- 73

3.2.3 Kukata tamaa ---------- 76

3.2.4 Kutoroka nyumbani ---------- 78

3.2.5 Maisha mabaya ---------- 81

3.2.6 Magonjwa ---------- 83

3.2.7 Hitimisho ---------- 84

**SURA YA NNE**

**USAWIRI WA WAANDISHI WA JINSIA TOFAUTI KUHUSU DHULUMA KWA WATOTO NA JINSI YA KUKABILIANA NALO**

4.0 Utangulizi ---------- 86

4.1 Waandishi wa kiume ---------- 86

4.2 waandishi wa kike ---------- 95

4.3 Ulinganifu ---------- 103

4.3.1 Aina za dhuluma ---------- 103

4.3.2 Utegemezi ---------- 104

4.3.3 Mabadiliko ya kiuchumi ---------- 105

4.3.4 Wadhulumu ---------------------------------------- 106

4.3.5 Masuala ya haki za watoto ---------------------------------------- 108

4.3.6 Unyonyaji wa watoto ---------------------------------------- 110

4.4 Tofauti

4.4.1 Wanaowadhulumu watoto zaidi ---------------------------------------- 111

4.4.2 Aina za watoto wanaodhulumiwa zaidi ---------------------------------------- 113

4.4.3 Ukubalifu wa tatizo hili ---------------------------------------- 113

4.5 Suluhu za dhuluma dhidi ya watoto ---------------------------------------- 115

4.6 Hitimisho ---------------------------------------- 118

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

5.0 Utangulizi ---------------------------------------- 120

5.1 Muhtasari ---------------------------------------- 120

5.2 Matokeo ya utafiti ---------------------------------------- 122

5.3 Mapendekezo ---------------------------------------- 130

**MAREJELEO** ---------------------------------------- 131

## SHUKRANI

Natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wa kazi hii Dkt. Ndungo na Dkt. Masinde kwa uongozi na ushauri wao katika kila hatua ya utafiti huu.

Pia natoa shukrani nyingi kwa wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunishauri na kunielekeza kila nilipohitaji msaada wao.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu kwa kunitia moyo na kushiriki vyema katika mijadala iliyonisaidia pakubwa.

Napenda kutoa shukrani za kipekee kwa bibi yangu Dalphine Wachuka na watoto wetu Evalyne, Bernard,na Junias kwa kuvumilia mengi nilipokuwa masomoni.

Mwisho ningependa kutoa shukrani kwa Tume Ya Kuajiri Waalimu kwa kunipa likizo ya masomo ingawa huduma zangu zilihitajika sana kazini .

## IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto kama yanavyobainika katika riwaya teule za Kiswahili. Mtafiti amehakiki kazi teule za waandishi za riwaya zilizoandikwa na waandishi wa kike na wa kiume. Riwaya zilizohakikiwa ni: *Siku Njema*, ya K. Walibora, *Tumaini* ya C. Momanyi, *Yatima* ya K.Wamitila. na *Kipimo cha Mizani* ya Z.Burhani .

Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni ya Ukata tamaa na ushari. Nadharia hii hujumuisha mambo ya kibinafsi na yale ya kijamii ambayo yanaweza kueleza chanzo cha aina nyingi za dhuluma.

Tasnifu hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Vilevile imegusia udurusu wa tafiti za awali, misingi ya nadharia, ukusanyaji wa data pamoja na uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili imetalii aina mbalimbali za dhuluma zinazowakabili watoto, zinavyodhihirika pamoja na athari zake.

Katika sura ya tatu, wanajamii wanaotekeleza dhuluma dhidi ya watoto wameonyeshwa. Sura ya tano nayo imeshughulikia tofauti na ukubaliano wa waandishi wa kiume na wa kike kuhusu dhuluma kwa watoto.

Sura ya tano ni hitimisho linalotoa muhtasari na matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo ya mtafiti. Mwisho Kuna marejeleo ya utafiti huu.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

Dhuluma : Ni dhana inayojumuisha vitendo visivyo vya haki, maonevu ya kimwili kijinsia, kihisia, na matumizi ya lugha anayofanyiwa mtu au mtoto kwa namna ambayo inamvunjia heshima na kumnyima haki zake za kibinadamu. Pia matumizi ya nguvu au matamshi ili kumuumiza au kumjeruhi mtu.

Mtoto : Mtu mwenye umri mdogo, aliye chini ya miaka kumi na minane. Anayetegemea wazazi, walezi kwa mahitaji ya kila siku.

Ukata tamaa: Ni hali inayoletwa na hali ya kutotimia kwa malengo

fulani aliyokusudia mtu.

Ushari : Ni vitendo vyovyote viovu vinavyolenga kumuudhi mtu anayetendewa.

Jibu badili : Kitendo chochote kinachopunguza kwa kiasi fulani kitendo kilichokusudiwa kutendwa hapo awali.

Kizuizi cha lengo: Ni kitendo au hali ambayo huzuia tendo linalozuia jambo fulani kutendeka.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Kulingana na ushahidi wa kihistoria, suala la dhuluma dhidi ya watoto limekuwepo tangu mwanzo wa ustaarabu (Aries 1962 na Radbill 1968). Kwa muda mrefu watoto wamekuwa wakidhulumiwa na asasi mbalimbali za kijamii kama vile dini na utamaduni. Hoja hii inaungwa mkono na Burgess (1979) anayesema kuwa, kwa muda mrefu wazazi wamekuwa wakiwadhulumu watoto wao.

Zamani katika nchi ya Roma, pamoja na jamii nyingi za Kiafrika, watoto walichukuliwa kama mali ya wazazi wao, na wangeweza kuwaua au kuwatendea maovu mbalimbali bila kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria (Cicchetti 1980). Katika Biblia, kuna visa kadhaa vya mauaji ya watoto vinavyoelezwa katika vitabu vya Kutoka 1:15, 1:22,Matayo 2:16. Kwa hivyo, kiongozi angeweza kutoa amri ya kuuawa kwa watoto hata bila kupingwa na jamii. Pia kwa karne nyingi jamii nyingi zilikuwa zikipendekeza adhabu kali itolewe kwa watoto wasiokuwa watiifu. Kwa mfano katika jimbo la Massachusetts, katika mwanzo wa karne ya kumi na saba kulipitishwa sheria ya kuuawa kwa mtoto asiyekuwa mtiifu (Fraser 1976). Baadhi ya wazazi hupata kisingizio cha kuwadhulumu watoto wakidai kuwa hata Biblia hupendekeza adhabu kali itolewe kwa mtoto kama njia ya kumwokoa kutokana na moto (Methali 23:13-14). Kulingana na Korbind (1977) anaonelea kuwa suala la maonevu kwa watoto limeenea katika baadhi ya jamii mbalimbali.

Ingawa tatizo hili limekuwepo tangu wakati huo, jamii nyingi hazikulizingatia kama suala muhimu.

Kabla ya miaka ya sitini, sekta nyingi, ikiwemo ya utabibu, hazikukubali kuwepo kwa tatizo hili (Cicchetti na wengine 1989). Ni kuanzia mwaka wa 1961, ambapo madaktari walianza kushtushwa na ongezeko la watoto walioumizwa waliokuwa wakipelekwa katika vituo vya afya huko Marekani. Ni kutokana na visa hivi ambapo mkereketwa C. Henry Kempe na wenzake(1995) walipoandaa kongamano kuhusu dhuluma kwa watoto. Kutokana na juhudi hizo, mashirika mengi yalianza kuundwa yakilenga kushughulikia watoto pamoja na masuala yanayohusu haki zao (Kempe 1995). Kulingana na Goldstein na wengineo (1973), ni wazi kwamba suala la dhuluma dhidi ya watoto lilianza kutiliwa maanani na kuanza kushughulikiwa. Juhudi za serikali nyingi, ikiwemo ya Kenya, zilianza harakati za kutunga sheria ili kulinda watoto. Ithibati hii ni thibitisho tosha ya juhudi hizi.

Katika mwaka wa 1974, Bunge la Marekani lilipitisha sheria dhidi ya dhuluma kwa watoto. Ilipendekeza pia majimbo mengine yapitishe sheria kama hiyo. Nchini Kenya, sheria juu ya watoto ilipitishwa mwaka wa 2001(Kenya Gazette Supplement). Kutokana na usuli huu, waandishi mbalimbali wa kazi za fasihi walianza kujishughulisha na maandishi ya kisanaa yaliyolenga kueleza na kuupiga vita uovu huu mpya wa kijamii. Mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi

hawezi kujiepusha na hali halisi inayomzunguka kwa vile ndiyo iliyomzaa na kumkuza (Senkoro 1982).

Utafiti huu unachunguza maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto katika baadhi ya riwaya teule za fasihi andishi zilizoandikwa hivi karibuni. Kuanzia miaka ya tisini , tatizo hili lilianza kuangaziwa kwa undani zaidi. Riwaya hizi ni: *Siku Njema* ya K.Walibora, *Kipimo cha Mizani* ya Z.Burhani, *Tumaini* ya C.Momanyi, na *Yatima* ya K.Wamitila, Waandishi hawa wamesawiri tatizo hili kwa mapana na marefu. Vitabu hivi vyote vimeandikwa miaka ya hivi karibuni, kuanzia mwaka wa 1996 na 2006 ambapo harakati za kupiga vita tatizo hili zimekuwa zikipamba moto. Utanzu wa riwaya ulichaguliwa kwa vile ndio unaomwezesha mtunzi kubuni kwa njia inayojitosheleza zaidi kuliko tanzu zingine. Ubunifu wa mtunzi kuhusu dhana hizi za kisaikolojia hudhihirika zaidi katika riwaya kuliko tanzu zingine. Utafiti huu unachunguza sura mbalimbali za dhuluma, asasi mbalimbali zinazoendeleza dhuluma, njia mbalimbali za utekelezaji wa dhuluma, utambuzi wa dhuluma pamoja na athari mbalimbali kwa watoto. Mtazamo wa kiuhalisia unachukulia kuwa mwandishi hana budi kuusawiri uhalisi katika ukamilifu wake (Lukacs 1963). Kwa hivyo yale yatokeayo katika jamii hayana budi kusawiriwa na mwandishi. Msisitizo ni kuwa yale yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi.

## 1.2 Swali la utafiti

Utafiti huu unachunguza maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto kama yalivyosawiriwa na waandishi teule wa riwaya za Kiswahili. Unabainisha aina za dhuluma, sababu za utendaji wa dhuluma, kuonyesha asasi zinazotekeleza dhuluma, vile dhuluma zinavyobainika pamoja na athari kwa maisha ya watoto. Vilevile unachunguza jinsi waandishi wa jinsia tofauti walivyolisawiri tatizo hili na kuangalia baadhi ya mikakati inayoweza kuwekwa ili kupunguza tatizo hili. Ingawa jamii nyingi hazikuchukulia baadhi ya vitendo kuwa viovu, au hatari kwa maisha ya watoto, mabadiliko ya mwelekeo wa kijamii yanachukulia kuwa watoto ni viumbe muhimu katika jamii. Maonevu yaliyozidi kiasi dhidi yao ni uovu unaofaa kupigwa vita na kuangamizwa kwa njia zote. Vitendo vilivyovuka mipaka dhidi yao vimeanza kumulikwa na wadau mbalimbali wakiwemo waandishi ili kuuweka wazi uovu huu. Fauka ya hayo asasi mbalimbali kama vile dini, na uzingatifu mpofu wa utamaduni vinachangia katika kuutekeleza uovu huu. Baadhi ya asasi huratibisha kanuni ambazo zinafaa kufuatwa na jamii bila kukiukwa. Ingawa vitendo hivi havikuwa vikichukuliwa kuwa ni dhuluma, siku hizi huchukuliwa kuwa ni uovu ambao husababisha madhara makubwa kwa watoto wahasiriwa .

Kwa maoni ya mtafiti, maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto hayajachunguzwa kama mada ya utafiti. Tafiti nyingi zimefanywa zikishughulikia maswala kama vile: unyonyaji, ukatili na matatizo ya kifamilia baadhi ya mengine. Haya ni

masuala yanayoikumba jamii kwa jumla bila kuzingatia mtoto kama mhusika muhimu. Masuala yanayowahusu yamesitiriwa katika mawazo ya kijumla kwa hivyo matatizo yao yamewekwa kama sehemu duni. Tafiti za hapo awali kama vile Kimani (2003),na Gitau (2005), zilishughulikia dhuluma dhidi ya wanawake na wanaume. Utafiti huu unanuia kuchangia katika juhudi za kuelimisha umma ili iache kutekeleza vitendo vilivyopitwa na wakati dhidi ya watoto, kwa vile ni kuwadhulumu na ni hatia katika sheria za Kenya.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

1. Ni aina zipi za dhuluma dhidi ya watoto zinazobainika katika kazi za fasihi zilizoteuliwa na zinabainika vipi?
2. Chanzo cha dhuluma hizi ni nini?
3. Asasi zinazowadhulumu watoto ni zipi na dhuluma zina taathira gani kwa watoto?
4. Je watunzi wa jinsia tofauti wamelisawiri vipi tatizo hili?
5. Wasanii wa kike na wa kiume wanatoa suluhu zipi kwa tatizo hili?

## 1.4 Malengo ya utafiti

1. Kueleza aina za dhuluma dhidi ya watoto na zinavyobainika.
2. Kuchunguza chanzo cha dhuluma hizi.

3. Kuonyesha asasi zinazotekeleza dhuluma na athari kwa maisha ya watoto.
4. Kubainisha vile watunzi wa jinsia tofauti walivyolisawiri tatizo hili.
5. Kutalii suluhu zinazotolewa na wasanii wa kike na wa kiume juu ya tatizo la dhuluma ya watoto.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Msukumo wa utafiti huu umetokana na ongezeko la haraka la visa mbali mbali vya dhuluma vinavyoripotiwa katika vyombo vya habari. Hili ni suala nyeti ambalo linahitaji kushughulikiwa. Kwa mfano, uchunguzi uliofanywa na Namwamba (2005) mmoja wa watetezi wa haki za kibinadamu, ulionyesha kuwa katika mji wa Nairobi visa zaidi ya mia saba viliripotiwa katika mwaka wa 2004 . Pia kutokana na ongezeko la kusambaa kwa ugonjwa wa ukimwi, kuna vifo vingi vinavyotokea kila siku. Kuna watoto wengi mayatima wanaoachwa bila walezi na wengine huachwa mikononi mwa jamaa zao. Wengine huweza kuanguka mikononi mwa walezi wanaoishia kuwafanyia maovu ya kila aina . Kwa hivyo tatizo hili ni muhimu kutafitiwa ili suluhisho liweze kupatikana. Vilevile mada hii imechaguliwa kuzingatia ukweli kwamba watoto ni miongoni mwa viumbe muhimu katika jamii yoyote na wanahitaji ulinzi. Kwa kawaida viumbe hawa huwategemea wazazi wao au wanajamii wengine kuwatimizia mahitaji yao ya kila siku. Ingawa nyumbani wanakoishi watoto hawa kunatarajiwa kuwa makazi yenye usalama mwingi, panaweza kuwa mahali hatari sana na pasipo na

usalama kwa watoto (Namwamba 2005). Suala kuhusu dhuluma dhidi ya watoto ni miongoni mwa masuala ibukizi yanayoangaziwa na baadhi ya mashirika mengi yasiyo ya kiserikali kama vile: United Nations Children Development Fund (U.N.IC.E.F.), World Health Organisation(W.H.O) na mengineyo.

Watoto huwa mikononi mwa watu wanaowaamini kama wazazi, jamaa na majirani na wanapotendewa maovu hawawezi kujitetea ama kupinga maonevu hayo. Kwa hivyo utafiti unaoangazia matatizo yao unahitajika ili kuwalinda kutokana na wazazi wasioajibika au walezi waovu. Baadhi ya watu hao waliopewa jukumu la kuwatunza watoto hutekeleza dhuluma hizi labda bila kujua, wakishikilia kufuata kanuni fulani za kitamaduni au za kidini.

Siku hizi kuna ongezeko la haraka la visa mbalimbali vya dhuluma zinazoelekezwa kwa watoto na huacha athari kubwa kwa viumbe hawa hafifu. Miongoni mwa dhuluma zinazoripotiwa ni: kunajisiwa, kuuawa miongoni mwa zingine (Benedictis na wengine, 2006). Pia fasihi ya watoto imeanza kutiliwa maanani sana katika vyuo vikuu na shule za msingi. Udurusu wa tafiti za awali unaonyesha kuwa tafiti nyingi zimelenga dhuluma dhidi ya wanawake na wanaume Gitau (2005) na Kimani (2003). Kwa hivyo kuna umuhimu wa kuchunguza dhuluma zinazowakumba watoto na athari zake kama zinavyosawiriwa katika fasihi. Tangu jadi, jamii nyingi huchukulia kuwa watoto ni baadhi ya mali ya wazazi wao (Mbiti1975). Pia watu wazima huwachukulia kuwa viumbe duni ambao lazima walindwe kwa vile hawana uwezo wa kujiamulia

masuala yanayowahusu . Utafiti huu unachangia katika kuangazia dhuluma dhidi ya watoto kama inavyobainika katika fasihi. Pia unadhamiria kuwazindua wana jamii wanaotekeleza dhuluma hizi ili waache tabia hizo. Mashirika yanayoshughulikia watoto waliodhulumiwa yatapata baadhi ya maoni yanayoweza kuchangia katika kusuluhisha tatizo hili. Baadhi ya watoto wanaodhulumiwa watazinduliwa ili wapinge dhuluma wanazotendewa.

## 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu unajikita katika kuchunguza swala la dhuluma dhidi ya watoto katika kazi teule za fasihi, kama mojawapo ya masuala ibukizi yanayoshughulikiwa na waandishi na wahakiki wengi wa kazi za fasihi. Baada ya usomaji wa vitabu mbalimbali mtafiti aliteua vitabu vifuatavyo vya riwaya:

1 *Siku Njema* , ya K.Walibora, ( 1996).

2 *Kipimo Cha Mizani,* ya Z.Burhani, ( 2004 ).

3 *Tumaini* , ya C.Momanyi, (2006).

4 *Yatima* , ya K.Wamitila, (2006)

Sababu za kuchagua vitabu hivi ni kwamba utafiti wa awali ulionyesha kuwa waandishi hawa wameshughulikia mada hii kwa undani zaidi, kwa hivyo vinachangia data inayohitajika kutafitia swala hili. Asasi mbalimbali zinazotekeleza dhuluma pamoja na athari zake kwa watoto zimeonyeshwa. Pia

wahusika wakuu wa vitabu hivi ni watoto, na kulingana naTucker (1981), lengo lao kuu linaweza kufasiriwa kuwa, walidhamiria kuangazia masuala muhimu yanayowakumba watoto .

Pia uchaguzi uliongozwa na wazo kuwa mwandishi haandiki katika ombwe tupu. Lazima msanii aangazie masuala muhimu yanayoikumba jamii yake. Vilevile riwaya hizi zote ziliandikwa kati ya mwaka wa 1996 na 2006, katika kipindi hiki, kilele cha harakati za kupigania haki za watoto nchini Kenya kilifikiwa mwaka wa 2001 ambapo sheria ya watoto ilipitishwa. Jambo hili la kupinga dhuluma dhidi ya watoto limeanza kutiliwa nguvu sana na mashirika mbalimbali katika nchi ya Kenya. Nchi ya Kenya ina mahakama za watoto ambazo hushughulikia watoto walioingia kwenye visa vya uvunjaji wa sheria labda kuepuka dhuluma katika aila zao (Thonden1997).

Utafiti unawahusisha watoto wote wa kiume na wa kike walio chini ya miaka kumi na nane. Hii ni kulingana na sheria ya watoto 2001. Ingawa riwaya hizi zina wahusika wa aina nyingi na maudhui mengi, utafiti huu unajifunga kwa wahusika watoto kwa miktadha itakayohusu dhuluma ili kutoa utoshelevu wa mada.

Uteuzi uliongozwa na ukweli kwamba mada ya dhuluma dhidi ya watoto ni suala nyeti ambalo limekuwepo tangu zamani katika jamii nyingi zinazofuata maadili ya kitamaduni na ya kidini. Watu wengi hujaribu kulipatia sura mbalimbali ili



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kuuficha na kusingizia kuwa wanawatia watoto adabu kumbe huishia kuwatendea vitendo vya dhuluma.

Pia ni muhimu kuonyesha jinsi waandishi wa kiume na wa kike walivyoshughulikia maudhui haya, kwa vile huenda ikawa kuna baadhi ya vipengele ambavyo watunzi wa jinsia tofauti walilishughulikia tofauti na wengine. Vitabu viwili vya riwaya vilivyoandikwa na wanawake vimeteuliwa na viwili vilivyoandikwa na wanaume.

### 1.7 Misingi ya nadharia

Utafiti unaongozwa na nadharia ya Ukata tamaa na Ushari. Waasisi wa nadharia hii ni Dollard J. na wenzake (1939). Walieleza kuwa wamepata chanzo cha ushari wote. Wanasisitiza kuwa tabia yoyote ya ushari hujitokeza baada ya mtu kukumbwa na ukata tamaa wa aina fulani, ambapo mhusika huzua tabia fulani ya ushari. Hata ingawa mhusika hatatenda jambo wakati huo, au atajaribu awezavyo kuficha athari zozote za kukata tamaa ili isionakane wazi, haimaanishi kuwa athari hizo zimeisha kabisa akilini mwake, zitaweza kuibuka baadaye. Buss (1961), alifafanua nadharia hii na kusema kuwa kuna uwezekano wa kuwa na mambo mengine ya kijamii yanayoweza kutanguliza ushari kama vile wivu na uhasama. Naye Fromn (1973),anaeleza kuwa tabia ya mtu binafsi huweza kuchangia katika kuongezeka au kupungua kwa ukatishi tamaa. Alitoa mfano wa mtu mlafi kukasirika zaidi akosapo chakula. Sababu za kuchagua nadharia hii ni

kuwa inajihusisha na masuala ya kijamii ya kueleza hasa chanzo cha ushari katika jamii.

Nadharia hii huunganisha dhana za kisaikolojia ambazo haziwezi kuonekana wazi pamoja na za kijamii ambazo zinaweza kuathiri tabia za watu . Athari hii inaweza kumfanya asababishe ushari kwa watu anaohusiana nao kwa vile atawaona kama vizuizi vya malengo yake. Pia inachangia katika welewa wa chanzo cha dhuluma kinyume na nadharia za kijadi zilizowachukulia watekelezaji wa dhuluma kama watu wasio na akili timamu na waliojawa na maovu ya aina zote (Sidebotham 2003). Inawaonyesha wadhulumu kama watu wenye akili timamu. Uhusiano kati ya wadhulumu na wadhulumiwa unaangaziwa kwa hivyo kuwaona katika maisha yao ya kawaida. Ingawa nadharia ya kisaikoanalitiki imeeleza chanzo cha ushari, ina upungufu wa kusisitiza zaidi hisia za mapenzi ya kimwili na kupuuza mambo mengine . Nadharia ya ukata tamaa na ushari ni jumuishi zaidikwa vile inajumusha mambo yanayotokana na mtu binafsi na mazingira yanayomzunguka. Kuna hali inayotanguliza tendo linalotokea baadaye.

Hali hii inayotokea mwanzo huweza kuonekana wazi au kufahamika na huchochea matukio yanayofuata hali hiyo. Kitendo ambacho huzuia tendo linalodhamiriwa huitwa kizuizi cha lengo. Kitendo hiki kikitokea hupunguza athari iliyotazamiwa. Kwa hivyo hali ya ukatishi tamaa hutokea baada ya kutotimizwa

kwa lengo fulani lililokusudiwa. Pia lazima mtu aonyeshe kuwa kulikuwa na kitu kilichotarajiwa kufanya mambo fulani lakini kikazuiliwa kutendeka.

Jibu badili

Ni kitendo chochote kinachozuia kutendeka kwa kitendo kilichodhamiriwa. Kitendo chochote kinacholenga kumdhuru mtu anayetendewa kinaitwa ushari. Kulingana na Dollard, haya ndiyo matokeo ya kimsingi ya ukata tamaa. Matokeo haya yanaweza kudhihirika kwa vitendo vya matumizi ya nguvu, matumizi ya matusi na matumizi mengine ya maneno yanayolenga kumchafulia mtu jina. Mara nyingine si lazima matokeo ya ushari yatokee kwa uwazi, mhusika huweza kuzua mbinu za siri za kudhuru au kulipiza kisasi au hata kuangamiza kisirisiri. Kisasi hiki kinaweza kuelekezwa kwa kitu kinachofikiriwa ndicho chanzo au kilicho na uhusiano na kinachokatisha tamaa au hata kitu kingine ambacho hakina hatia yoyote. Kitu kinacholengwa kutendewa ushari kinaweza kuwa binadamu au kitu kisicho na uhai. Wakati mwingine ushari haulekezwi kwa kitu chochote. Kwa mfano, mtu anaweza kutoa matusi au kupiga siyahi baada ya kujiumiza kwa kifaa fulani kama vile nyundo. Maneno hayo ni ishara ya ushari. Nadharia hii huongozwa na kanuni mbili za kisaikolojia.

(i) Kanuni za kisaikolojia za kwanza

.Hii hushikilia kuwa ukatishi tamaa huzua matendo ya ushari. Dhana hii hutusaida kubashiri vitendo ambavyo vinaweza kuchukuliwa kama chanzo cha

ushari. Pia yale matendo mengine ya kisaikolojia yapaswa kutiliwa maanani kama vile: Nguvu ya kitu kinachosababisha ushari. Nguvu hii hutegemea kiasi cha ukata tamaa unaohusika. Pia hutegemea nguvu za vizuizi vinavyozuia kukamilika kwa lengo fulani. Ingawa hivyo, ushari unaolengwa kutekelezwa hulingana na kiasi cha adhabu dhidi ya kitu kinachokusudiwa. Kwa hivyo kila tendo linalosababisha ukata tamaa huweza kuwa chanzo cha vitendo mbalimbali vya ushari.

(ii) Kanuni za kisaikolojia za pili

Kuna ushari wa wazi na usiokuwa wazi. Inachukulia kuwa ukata tamaa unapotokea basi ushari hutokea pia ukielekezwa kwenye vitu au viumbe vinavyofikiriwa kusababisha ukata tamaa huo. Vilevile ushari unaweza kuelekezwa kwa vitu vingine vinavyofikiriwa kuhusiana na vitu vinavyosababisha ukatishi tamaa huo. Kwa mfano, mfanyakazi aliyenyimwa ruhusa ya kwenda likizoni huweza kumkasirikia mwajiri wake pamoja na wafanyakazi wengine. Tendo lolote linalosababisha ukata tamaa huzua tendo la ushari. Ushari wa wazi unapozuiwa kutendeka kwa kuogopa adhabu kali ambayo inaweza kutolewa baada ya kugunduliwa, jambo hili huzidisha kukata tamaa kwa mhusika. Ongezeko hili la ukata tamaa linatarajiwa:

(a) Kuzua kwa uwazi vitendo vya shari dhidi ya kitu kinachokisiwa kuhusika na uvurugaji wa ushari wa awali uliokusudiwa kutekelezwa.

(b) Kwa njia ya siri zaidi, ushari unatekelezwa kwa nguvu zaidi kwa vitu vingine vilivyohusika katika ukata tamaa huo. Ikiwa ushari uliolengwa kwa kitu

fulani utazuiliwa, vilevile vitendo vingine vya ushari havitatekelezwa kwa kitu hiki. Kwa hivyo aliyekusudia kutekeleza ushari huu atauelekeza kwa kitu kingine, wanachokiita ushari uliohamishwa kutoka kitu kimoja hadi kingine. Nadharia hii ina mihimili ifuatayo:

1 Kuna hali fulani inayotanguliza tendo lolote linalotokea baadaye.

2 Kuna ushari wa wazi na wa siri unaoelekezwa kwa vitu vinavyofikiriwa kusababisha ukata tamaa au hata kwa vitu vingine.

3 Vitendo vya ushari hulenga kuumiza mlengwa kimwili au kihisia

4 Mbali na hali zinazotanguliza tendo, tabia ya mtu binafsi inaweza kuzidisha au kupunguza ushari

Mihimili hii inatumiwa kuhakiki aina za dhuluma katika jamii, zinavyobainika pamoja na kutambulisha asasi zinazotekeleza dhuluma hizo. Hali zinazotanguliza tendo lolote zinaweza kubainisha sababu mbali mbali za utekelezaji wa dhuluma kwa watoto. Vitengo viwili vya ushari, wazi na wa siri vinatusaidia kuchambua aina za dhuluma zinazojadiliwa pamoja na utambuzi wa asasi husika kwa vile uovu wowote unaotekelezwa, kuna wanaoutekeleza pamoja na sababu za kuutekeleza.

## 1.8 Udurusu wa tafiti za awali

Kuna baadhi ya watafiti ambao wamejishughulisha na maswala yanayohusu dhuluma dhidi ya wanadamu mbalimbali. Watafiti hao wamejikita katika sehemu mbalimbali. Kuna wale walioshughulikia swala la dhuluma kwa watoto kwa jumla,

na wengine walijishughulisha na maovu yanayotendewa wanawake na wengine waliochunguza maovu yatendewayo wanaume.

Kati ya walioangalia swala hili kwa jumla ni Burgess (1979), anayesema kuwa watoto wamekuwa wakidhulumiwa na asasi mbalimbali za kijamii. Kati asasi hizo ni wazazi na jamaa miongoni mwa zingine. Anaonyesha kuwa mtoto anatakiwa kustarehe, ahisi upendo, na usalama akiwa miongoni mwa watu anaowaamini. Nao Lynch na Roberts (1993), wanaonyesha kuwa dhuluma zina athari nyingi katika maisha ya watoto. Wanaeleza kuwa ingawa mtoto anaonekana msahaulivu wa matukio fulani, hukumbuka zaidi vitendo vya dhuluma. Uchungu huo unaweza kusababisha huzuni isiyoisha moyoni mwake na pengine kusababisha ulipishaji wa kisasi. Naye Namwamba(2005), analionyesha swala hili kama mojawapo ya maswala ibukizi yanayofaa kutiliwa mkazo sana. Anaeleza kuwa watoto wamezingirwa na hatari za aina nyingi kama vile kupigwa, magonjwa na kutojaliwa na jamii. Juhudi za mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile (U.N.IC.F.,W.H.O, na mengine yameonyeshwa. Maandishi haya yanaunda usuli mwafaka wa utafiti huu. Juhudi zao za kuangazia swala hili kunatusaidia kuchambua jinsi wasanii walivyolisawiri kisanii.

Ndungo (1998), alishughulikia taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi. Anathibitisha kuwa katika matumizi ya methali za Gikuyu na Kiswahili, mwanamke amepewa nafasi ya chini akilinganishwa na mwanamume. Mwanamke amechorwa kama kiumbe ambacho hakiwezi kutegemewa. Ingawa ni

mlezi, anatumiwa kama mfanyakazi katika sekta ya kilimo. Umashuhuri wa mwanamume ulipimwa kwa idadi ya ng'ombe aliomiliki, na wanawake alioweza kuoa. Vilevile walichukuliwa kama ngazi ya kupandia kijamii, kisiasa na kiuchumi. Walitakiwa kuwa wavumilivu hata wakiteswa na wanaume wao. Mambo hayo yote ni dhuluma kwa mwanamke. Kwa kulinganisha methali za Gikuyu na za Kiswahili utafiti huu ulionyesha kuwa kuna maoni sawa yanayomdhalilisha na kumwonea mwanamke. Pia tunazingatia kuwa masuala ya tohara, ndoa za lazima ni dhuluma dhidi ya watoto.

Utafiti huu una maana kwa vile unatupa picha ya mwanamke. Picha hii ni aina ya dhuluma dhidi ya mwanamke. Kuna uwiano kati ya nafasi aliyotengewa mwanamke na ile iliyotengewa watoto katika jamii nyingi. Nafasi hiyo duni inasaidia kuonyesha kuwa dhuluma watendewazo wanawake zinaweza kutendewa watoto pia. Mwanamke ndiye mlezi wa mtoto, misingi ya kijamii inayotumiwa kumdhulumu mwanamke inaweza kutumiwa dhidi ya mtoto hasa mtoto wa kike.

Momanyi (1998) alitafiti juu ya usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza iwapo mwanamke katika jamii ya Waswahili Waislamu amedunishwa na kubaguliwa katika misingi ya uana. Mtafiti alibainisha kuwa mwanamke amesawiriwa kama kifaa cha utumishi kama vile kidau, konde au tunda.

Mwanamke ni kifaa cha kumtumikia mwanamume. Amedunishwa kwa njia mbalimbali kama vile kutoshirikishwa katika njia halali za kujipatia riziki, kutoelimishwa sawa na mwanamume, ukosefu wa uhuru wa kibinafsi na kudharauliwa. Utafiti huu unatusaidia katika kumulika baadhi ya asasi zinazotumiwa na jamii kuwadhulumu wanadamu mbalimbali. Mtafiti ana-chunguza zaidi asasi hizo na vile zinavyojitokeza katika kazi teule zinazotumiwa kutafitia swala hili. Mabadiliko mbalimbali yanayozikumba asasi hizi husaidia kuonyesha vile zinavyoweza kutumiwa kuleta mabadiliko katika maisha ya jamii. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa vile wetu unadhamiria kuwalenga watoto na jinsi wanavyokabiliwa na maonevu katika riwaya za Kiswahili. Utafiti huu utawahusisha watoto wa kike na wa kiume kinyume na Ndungo na Momanyi waliolenga wanawake wakiwemo wasichana.

Tomison (1996) akitafiti juu ya uhusiano kati ya dhuluma kwa watoto na madawa ya kulevya. Anaonyesha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya mambo hayo mawili. Anatambua vyanzo mbalimbali vya dhuluma kama vile tabia za kibinafsi, matatizo ya kinyumbani na mambo mengine ya kijamii. Utafiti huu ulitambua aina mbalimbali za dhuluma kama vile: kutowatunza watoto kabisa, mauaji na matumizi ya nguvu iliyopita kiasi. Ulishughulikia suala ibukizi la matumizi ya madawa ya kulevya kama mojawapo ya maovu ya kijamii ambayo yanafaa kuangamizwa. Unapendekeza mafunzo ya kijamii pamoja na kushirikishwa kwa mafunzo hayo katika mitaala ya shuleni. Ingawa utafiti huu si

wa kifasihi, unachangia pakubwa katika kuielewa mada hii. Maswala muhimu ya kijamii yanayoangaziwa katika utafiti huu kama vile dhuluma zinazowakumba watoto katika nchi ya Australia ndiyo yanayoshughulikiwa kisanii na waandishi wa riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu. Tofauti ni kuwa utafiti wa sasa unafanywa katika mazingira, wakati, na utamaduni tofauti.

Kimani (2003) alitafiti juu ya swala la wanawake wakiwemo wasichana katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulibainisha kwamba mwanamke anakabiliwa na dhuluma za aina nyingi zinazotokana na wanaume. Dini na ndoa zinatajwa kama mifano ya asasi za kijamii zinazotumiwa kuwadhulumu wanawake na wasichana. Pia alionyesha kuwa kuna tofauti fulani kati ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu swala la dhuluma dhidi ya mwanamke. Utafiti huu utakuwa tofauti kwa vile utawaangalia watoto na jinsi wanavyodhulumiwa kwa misingi ya kidini, kitamaduni na kijamii.

Gitau (2005) alitafiti juu ya unyanyasaji dhidi ya wanaume katika fasihi andishi ya Kiswahili. Alionyesha kuwa ingawa wanasawiriwa kama viumbe walio na nguvu na ukakamavu, pia hukabiliwa na unyanyasaji wa aina nyingi katika maingiliano yao na wanawake au wanaume wengine. Alionyesha baadhi ya unyanyasaji kama vile matusi, kupigwa, na utengano wa kijamaa kati ya mengine. Alithibitisha kuwa waandishi wa kiume na wa kike aliowateua hulingana katika mtazamo wao wa kuwa, wanaume hukabiliwa na aina tofauti za

unyanyasaji. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa vile wetu unawaangalia watoto wa kike na wa kiume na huo uliwaangalia wanaume. Ulitumia nadharia ya Umuundo tekelezi na wetu unatumia ukata tamaa na ushari. Hata hivyo unadhamiria kuziba pengo lililoachwa na utafiti huo la kuchunguza maswala mengine ya uana .

## 1.9 Ukusanyaji wa data

Data inayotumiwa katika utafiti huu imekusanywa maktabani.

### Utafiti maktabani

Data imekusanywa kutokana na usomaji wa riwaya zilizoteuliwa. Kutokana na data hii aina mbalimbali za dhuluma dhidi ya watoto zimechunguzwa. Asasi mbalimbali zinazowadhulumu zimechunguzwa. Pia athari za dhuluma kwa wahusika hawa kama zinavyojitokeza katika riwaya hizi zimeonyeshwa.

Mtafiti anazingatia matukio mbalimbali katika kazi hizi ambayo yanaweza kufasiriwa kama dhuluma. Muktadha wa matendo hayo umechunguzwa ili kubainisha sababu za dhuluma hizo kama vile utamaduni. Mielekeo mbalimbali ya watunzi wa kike na wa kiume imechunguzwa.

Vilevile maandishi mbalimbali yanayohusu uhakiki wa fasihi yamesomwa yakiwemo, magazeti na majarida yanayoshughulikia suala la dhuluma katika jamii na hasa katika familia. Maandishi hayo yanachangia zaidi katika kupanua

mawanda ya utafiti huu. Vitabu vinavyotoa maelezo zaidi ya nadharia ya ukata tamaa vimesomwa. Upekuzi wa huduma ya mtandao umesaidia kuchunguza matokeo ya tafiti za hivi karibuni yanayohusiana na swala hili.

## 1.10 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Data kutoka katika kazi za fasihi zilizoteuliwa imechambuliwa kulingana na maswala ya utafiti. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yanahusu kubainisha na kuainisha aina za dhuluma zinazowakumba watoto. Pia inaonyesha chanzo cha dhuluma hizo, taathira zake kwa maisha ya watoto na jamii kwa jumla na hatua za kusuluhisha tatizo hili.

Kwa kutumia mihimili ya nadharia iliyoteuliwa utafiti umebainisha misingi ya unyanyasaji huo.

# SURA YA PILI

## AINA ZA DHULUMA DHIDI YA WATOTO, ZINAVYOBAINIKA NA SABABU ZAKE

### 2.0 Utangulizi

Mojawapo ya maswala ibukizi yanayoshughulikiwa na waandishi ni dhuluma dhidi ya watoto. Mwandishi yeyote anatarajiwa kueleza matatizo na malalamiko ya jamii yake, kwa kueleza matarajio yao (White na Couzens 1984:148). Kwa hivyo, ndiye jicho la jamii yake. Anatarajiwa aangazie maswala yote yatokeayo katika jamii anamoishi. Kwa hivyo, yale tunayoyasoma katika fasihi tunayahusisha na matukio ya kawaida katika jamii halisi. Mojawapo ya maswala ibukizi yanayoshughulikiwa na waandishi walioteuliwa katika utafiti huu ni dhuluma dhidi ya watoto. Kwa mujibu wa Gatobu (2003), watoto ni miongoni mwa waathiriwa wengi wa dhuluma dhidi ya wanajamii nchini Kenya.

Kwa kurejelea nadharia ya ukatai tamaa na ushari, aina za dhuluma dhidi ya watoto zinaelezwa kuwa za wazi na za siri (Dollard na wengineo1939). Hali hii inatokana na mila za jamii za Kiafrika na hali ya kiuchumi, baadhi ya mengine. Katika sura hii, aina mbalimbali za dhuluma dhidi ya watoto, na vile zinavyobainika, pamoja na chanzo zake zimejadiliwa kama zinavyojitokeza katika vitabu viteule vya riwaya za Kiswahili.

### 2.1.1 Kujeruhiwa Kimwili

Kwa mujibu wa Meier (1985:1), haya ni majeraha ya viungo vya mwili yanayotokana na vitendo vya ushari vinavyosababishwa na wazazi au walezi. Majeruhi haya yanaweza kutokana na mapigo ya aina mbalimbali, au hata adhabu kali iliyopita kiasi. Vitendo hivi vya matumizi ya nguvu dhidi ya watoto hujeruhi viungo vyao vya mwili. Wanaohusika na vitendo hivi hufanya hivyo kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na chuki, wivu, na kuwatia adabu miongoni mwa mengine.

Katika riwaya ya *Yatima,* (uk.20), kuna kisa cha kaka wawili Mwilu na Mwila, ambao wamezaliwa na mama tofauti. Baada ya kifo cha mamake Mwilu, Mamake Mwila anaanza kumchukia Mwilu, kwa sababu Mwilu "alikuwa mtoto mwenye sura nzuri. Pia alionekana kuwa na akili kuliko mwanawe" (Uk. 21). Kisa hiki kinaonyesha motifu ya mama wa kambo katika fasihi simulizi. Anajitokeza kama mwenye wivu na mwovu. Kwa hayo, anaanza kupanga mipango ya kumwangamiza Mwilu anayoitekeleza baadaye kwa kuchimba shimo kubwa na kutandika ngozi juu yake. Anamtaka Mwilu aketi juu ya ngozi ya ng'ombe iliyotandikwa pale ili asikilize maelezo vizuri. Anapoketi anatumbukia ndani ya shimo na mama huyo analifukia shimo hilo kwa mchanga mara moja,

na kumzika Mwilu akiwa hai. Kitendo hiki ni kiovu kwa vile Mwilu alimpenda na kumwamini mamake wa kambo (Uk. 25). Viungo vyake vya mwili vilijeruhiwa pakubwa. Ingawa aliokolewa baadaye, "mwili wake ulionekana mwembamba ajabu" (Uk. 27) Huu ni mfano wa majeraha yanayosababishwa na walezi ambao huwaonea wivu watoto wanaowalea.

Vilevile katika riwaya hii imebainika kuwa kuna waajiri kama Mam' Peter ambao wanawapiga watoto waliowaajiri (uk.63). Katiwa, anaizipoteza pesa alizokuwa ametumwa kwenda kununua mkate na maziwa. Sababu ya kuzipoteza fedha ni kumwogopa mtu aliyemwangalia kwa macho mekundu. Anapoanguka kwenye shimo la maji, pesa zinamdondokea humo majini. Anapofika nyumbani na kumweleza Mam' Peter yote yaliyotokea, mama huyo anaianza kumfokea "Hapana wewe ni mwizi! Umeficha zile pesa ... Leo utakiona (Uk. 52). Mama huyo haamini kuwa pesa zimepotea. Anampiga sana, hata watu wanaomwona akipigwa hawaji kumsaidia. Hali hii inaashiria hali ya jamii ya kutojali pale maafa yanapotekelezwa. Kwa mujibu wa mila za Kiafrika,mtoto si wa mtu ni wa jamii nzima.

Siku nyingine mama huyo anampiga sana Katiwa kwa kutumia mshipi wa nguo (Uk. 63). Hata baada ya kumsihi asimpige, mama huyo anaendelea kumpiga kwa nguvu "Kama aliyekuwa anapiga gunia" (Uk. 63). Sababu ya kumpiga hivyo ni kisingizio cha Peter, mwanawe kuwa ndiye aliyeiba pesa, ilhali yeye Peter

ndiye ameziiba. Haamini kuwa mwanawe ndiye ameiba pesa hizo. Katiwa anapojaribu kumwambia kuwa ni Peter anakataa katakata na kusema:

> "Mwanangu hawezi kuiba ... ni wewe tu. Hata shangazi yako aliniambia kuwa ulikuwa ukiiba ulipokuwa ukiishi naye. Wewe ni msichana mwizi" (Uk. 63).

Maneno haya ya Mama Peter yanaonyesha kuwa anamwadhibu Katiwa kwa kusingiziwa tu. Hawezi kuamini kuwa mtoto wake ni mwizi.

Aina hii ya dhuluma hubainika kwa kuonekana wazi kwa majeraha katika viungo vya mwili. Kwa mfano, baada ya kupigwa sana, Katiwa alikuwa akihisi maumivu mwili mzima. Jicho lake lilikuwa limevimba na alishindwa kuinua mikono yake vizuri (Uk. 52). Tunaweza kuchukulia kuwa pigo hili lilikuwa la kufidia pesa zilizopotea, pamoja na kuficha ukweli kuwa mwanawe Peter alikuwa mwizi. Kwa hivyo baadhi ya dhuluma watendewazo watoto hutumiwa kuficha ukweli fulani.

Katika riwaya ya *Tumaini,* kuna kisa mzee Masumbuko. Anajulikana katika kijiji cha Mabuyuni kutokana na jinsi anavyowalea wanawe kwa ukatili mwingi. Hamaki zake hasa anapolewa pombe zinavuka mpaka na kuwafanya watu wote wamwambae (Uk. 15). Vilevile, ana mazoea ya kuwaadhibu watoto wake kikatili kwa kuwafungia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Mtoto anachapwa kwa fimbo hadi inapovunjika au mpita njia atokee na kumkemea (Uk. 27). Adhabu hii inayotekelezwa na Masumbuko dhidi ya wanawe ilimfanya aogopwe na wanajamii. Sababu ya masumbuko kutekeleza adhabu hizi inatokana na tabia

yake mwenyewe pamoja na athari ya ulevi unaozidisha tabia hii mbaya. Ni wazi kuwa mapigo hayo, pamoja na mwasho unaotokana na majani ya upupu yanasababisha majeraha katika miili ya wahasiriwa. Kwa hivyo, adhabu hii ni mbaya kwa vile inaweza kujeruhi viungo vya mwili.

Kelly (1983) anaeleza kuwa, kutengwa na watu, humfanya mtu ahisi upweke unaoweza kumletea madhara ya kihisia. Kulingana na nadharia inayoongoza utafiti, jambo hili ni mojawapo ya mambo yanayosababisha ukata tamaa. Baadaye matendo ya ushari kama kuwapiga watoto kikatili hutokea yakielekezwa kwao .

Vilevile katika riwaya ya *Burhani*), tunakumbana na Mariyamu ambaye humpiga Ali kikatili. Anampiga kwa kutoka nyumbani na kwenda nje bila ruhusa. Anaanza kumpiga kwa makofi na kuendelea kwa mateke. Ali anapokosa kulia, anaingia ndani ya nyumba na kutoka na henzirani "akampiga popote alipoweza kumfikia" (Uk. 115). Adhabu hii ni mbaya kwa mtoto wa miaka tisa kama Ali. Madhara ya pigo hili yanabainika wazi anapojiburura kwa maumivu anapoitwa na Umari. Mwendo huo wa kujiburura unadhihirisha maumivu anayoyahisi mwilini baada ya kupigwa na Mariyamu. Baadaye mabishano kati ya Ali na Mariyamu juu ya usemi kuwa mama yake Ali ni mwendawazimu yanasababisha pigo kali kwa Ali. Anapinga vikali na kusema:

> "Uwongo! Si mwendawazimu" (Uk. 151).

Mariyamu anampiga kofi kali akimwambia:

> "Nani unamwambia mwongo. Na mkifanya ghasia nitawaitia polisi" .

Mtindo huu ndio unaoelezwa na Meier (1985:36) kuwa mojawapo ya hali zinazosababisha wazazi kuwapiga watoto wao. Anaeleza kuwa:

> "Baadhi ya wazazi huishia kuwapiga watoto wao kama mojawapo ya njia za kusuluhisha mabishano bila kujali kama wakisemacho ni cha ukweli au cha uwongo ili kuthibitisha uwezo wao juu ya watoto.
> (Tafsiri ya mtafiti)

Katika riwaya ya *Siku Njema,* Kongowea anafanyishwa kazi nyingi na Mwanasaumu, kama vile: kufagia nyumba, kuipiga deki, kupika, kupakua, kufua nguo, kukuna nazi kwa mbuzi, na kazi nyinginezo. Kazi hizi zilikuwa za kuchosha sana (Uk. 23). Kwa ajili ya uchofu na masumbufu mengine aliyokumbana nayo, anakaa akitarajia siku ambayo angetoka kwa mjomba wake Kitwana.

### 2.1.2 Dhuluma za Kihisia

Iwaniec (1996), anaeleza dhuluma za kihisia kama tabia ya uhasama inayoathiri sharifu ya kibinafsi ya mtoto na hushusha hali ya kutimiza malengo fulani. Pia huzuia hisi ya kujihusisha na jamii. Jambo hili hutekelezwa na wazazi na walezi ambao huaibisha, hutisha, hubeza, na huwatusi watoto na wanafanya hivyo kimaksudi wakiwa na lengo la kuwasononesha watoto (Tafsiri ya mtafiti).

Katika malezi, ni muhimu mtoto aonyeshwe mapenzi na wazazi na walezi ili akue akiwa na afya ya kimwili na kiakili (Ainsworth,1980) . Akosapo mapenzi, mtoto

huathirika kiafya na kihisia, hata maisha yake ya baadaye huweza kuathirika pia. Ukiukaji wa jambo hili huchukuliwa kuwa ni maonevu ya kihisia. Maonevu haya hujitokeza katika sura mbali mbali kama vile, matusi, kubezwa, kutengwa na jamii, masimango na vitisho, miongoni mwa mengine.

Katika riwaya ya *Yatima*, Katiwa anashangazwa na uamuzi wa shangaziye Juliana wa kumpeleka nyumbani akaishi na babu yake. Anashangaa ni kwa nini shangaziye anakataa kumchukua pamoja na wanawe huko atakakohamia. Pia anashangaa kama shangaziye anampenda, makubwa yanamfika wanapofika katika kijiji cha Masira. Babu yake anamkataa kabisa akisema:

> "Usiniletee mtoto hapa, ati mjukuu, mimi sio mlezi wa watoto ... Babu nini? Ondoka urudi naye mlikotoka" Uk. 6

Jambo hili la kukataliwa linamsumbua Katiwa sana asijue la kufanya, hasa shangaziye anapoondoka na kumuacha na kurejea mjini. Anapoingia kibandani alimo babu yake na kumwamkua, hageuki wala kumjibu. Baadaye anamwangalia na kutoka nje bila kusema lolote. Makubwa yanamfika baadaye anapomwuliza babu yake sababu ya kutotaka kuongea naye. Babu anamjibu:

> "Mimi sitaki kukaa nawe ... sikutaki ondokaa ... a .. a" (Uk. 9).

Kwa kuogopa, Katiwa anakimbilia nje na usiku huo analala pamoja na mbuzi na kondoo kibandani mwao. Analia kwa uchungu mwingi na kushangaa ni kwa nini

babu yake hampendi. Mawazo hayo yote yanasababisha huzuni nyingi kwa Katiwa.

Anapopelekwa na shangaziye kwa Mam' Peter, mama huyo analibadilisha jina na kumwita Mary. Hajui sababu ya kubadilishiwa jina hilo. Anashangaa ni kwa nini shangaziye akamwacha pale. Pia anahisi kuwa mama yule hampendi, anashangaa:

> "Je atawezaje kunipenda ikiwa hata jina langu halipendi?" (Uk. 45)

Mawazo haya yanamsumbua Katiwa akilini, kwa vile haelezwi kwa nini kaachwa pale na kwa nini ni muhimu kubadilishiwa jina.

Zaidi ya hayo, Katiwa haruhusiwi kula pamoja na wengine kwenye meza kuu. Anakula chakula chake jikoni kilichokuwa tofauti na wengine. Kutengwa huku na jamii ya Mam' Peter kunasababisha kubezwa na kudharauliwa na watoto wake. Watoto hao wanamcheka na kumwimbia wimbo unaomuudhi sana:

> "Mtazame ... mtazame ... Katiwa mjinga
> Moja na moja hawezi kuwanga
> Anajua tu ugali kusonga anachekesha mjinga ... " Uk. 54

Kila anapoimbiwa wimbo huu anasikitika na kulia sana. Anapomwambia Mam' Peter, anampigia kelele badala ya kuwakanya watoto wake dhidi ya kumuudhi. Anaathirika pakubwa anapoamua kumwuliza mama huyo ni kwa nini haendi shule. Anajibiwa:

> "Watoto wanalipiwa pesa na wazazi wao ... na wewe huna wazazi"
> Uk. 50)

Katiwa anaenda pembeni na kuanza kulia. Anashinda na huzuni nyingi siku hiyo. Hata anapolala alnakosa utulivu kabisa. Anamsihi shangaziye amrudishe kwa babu anapowatembelea (Uk. 48). Maisha ya Katiwa kwa Mam' Peter ni ya huzuni na majonzi. Iwaniec (1996:46) akijadili juu ya uhusiano wa watoto na wazazi anasema kuwa:

> "Kudhalilisha, kupigia kelele, madharau na matusi ni baadhi ya mambo yanayosababisha dhuluma za kihisia".

Masingizio ya uongo pia ni mambo yanayomwumiza Katiwa kihisia. Siku moja Peter anayamwaga maji kitandani mwake na kumsingizia kuwa kakojoa kitandani. Mam' Peter anamgombeza zaidi na kumlazimisha kulianika godoro (Uk. 54). Siku nyingine Peter aliingia nyumbani na kuchukua pesa katika kikebe. Peter alimsingizia Katiwa kuwa ndiye aliyeiba na yeye alimwona. Mamake alimpiga Katiwa sana na kumfukuza nyumbani usiku akisema kuwa:

> "Mimi siwezi kuishi na mwizi ondoka!" Uk. 64

Akishadidia juu ya kubainika kwa dhuluma za kihisia, Benedicts na wengine (2006), wanaeleza kuwa: huzuni, majonzi, mfadhaiko wa moyo, hali ya kutojali na kukosa utulivu ni baadhi ya mambo yanayobainika katika watoto. Mambo haya yanabainika kwa Katiwa. Babu anapomkataa na kumfukuza anaingia bandani mwa mbuzi na kuanza kulia (Uk. 9).

Katika riwaya ya *Tumaini*, mhusika Tumaini anadhulumiwa kihisia na babake Mzee Masumbuko. Ingawa ni mmoja wa wasichana wanaopinga tohara za wanawake na wanaokuwa na lengo la kusoma mpaka chuo kikuu, juhudi zake

zinazuiwa na babake. Mzee huyo amepanga kumpasha tohara na baadaye kumuoza (Uk. 17). Tumaini anauona kama mwisho wa ndoto yake ya kuwa daktari. Alnapojaribu kumweleza babake ili aelewe dhamira yake, Mzee huyo anakataa kabisa (Uk. 10). Juhudi za kuzungumza naye zinapoambulia patupu, anachukua hatua ya kutoroka kwao na kwenda kwa mamake mdogo, Bi. Halima. Kwa kutoroka huku, babake anatuma ujumbe kuwa asirejee kwake tena.

Mabezo ya nduguye Idi yanaendelea kumkata Tumaini moyo. Yeye ana mwelekeo sawa na babake wa kuwaona dada zake kama watumishi tu pale nyumbani. Mara kwa mara anawaambia kuwa:

> "Wao ni kama bidhaa za uwekezaji pale nyumbani. Walisubiri kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomeshea" (Uk. 16)

Utani wa Kijungwe wakiwa shuleni pia unamkosesha furaha. Anamwuliza:

> "Tuma hivi uliikimbia tohara kwa sababu ya woga au mchumba uliyechaguliwa hukumpenda?" (Uk. 59)

Utani huo unamchoma moyo Tumaini na anamrushia jiwe analoliepa na kumpiga mwalimu aliyekuwa amesimama mbali kidogo. Ukweli ni kuwa, Tumaini haogopi tohara. Anaogopa kuwa baada ya kupashwa tohara, babake hangemruhusu kuendelea na masomo. Tayari ameanza kumtafutia mchumba ili amuoze mara moja baada ya tohara hiyo. Maisha yake ya baadaye yangeathirika sana (Uk. 27). Matusi yanayoelekezwa kwa Tumaini yanaathiri hisia zake sana. Hakupendezwa na yale aliyofanyiwa Zena. Msichana huyo alinyanyuliwa juu juu na genge la vijana akaozwa kwa Mzee Chumo, kinyume na mapenzi yake. Ndoa za aina hiyo ambazo hazina msingi wa mapenzi anazichukia sana Tumaini.

Matusi yanayoelekezwa kwake yanasononesha moyo wake pakubwa. Mamake anapoenda kwa Halima anamweleza kuwa:

"Masumbuko hatakubali binti yake kuwa msungo". (Uk. 30)

Matumizi ya maneno kama hayo dhidi yake yanamsononesha moyo .Tumaini anaona kuwa hata mamake anamwunga mkono babake katika mipango ya kumpasha tohara, kisha wamuoze. Wasiwasi unamwingia zaidi anapowaona wazee wakikutana na kufanya mashauri na kuondoka. Nao akina mama huja huko kila mara. Mkutano wa faragha na mama mmoja aliyezuru kule kwao unamtia wasiwasi sana. Mama huyo, (Bi. Nemsi), ndiye angekuwa somo lake. Mamake anapomshauri ili akubali tohara, maneno hayo yanashuka moyoni mwake huku "yakimchoma na kumchachafya" (Uk. 19). Akiwa shuleni, anapenda kujiunga na wale wasichana wasiopashwa tohara na pamoja wanaipinga vikali. Anawazia vile waalimu na wenzake watakavyosema kama atakubali kupashwa tohara.

Kero za kihisia zatokana na waalimu. Almasi anavunjwa moyo na mwalimu wa Hisabati kwa vile hata atiapo bidii, anaendelea kupata sufuri tu na mwalimu huichora sufuri kisha akaitia macho pua na mdomo. Jambo hili ni la kumvunja mwanafunzi moyo. Mwalimu ana wajibu wa kuwatia moyo wanafunzi wala si kuwatia katika lindi la simanzi.

Kwa Tumaini, dhuluma hizi zinabainika katika hatua ya Tumaini ya kuamua kutoroka kwao, ili aiepuke. Ule ujumbe wa babake kuwa asirejee kwake, unadhihirisha ukweli kuwa yote anayoyahofia Tumaini, babake amepanga kuyatekeleza.

Kutenganishwa kwa watoto na mama yao, au watu na wanaowaamini husababisha upweke na wasiwasi usioisha. Akishadidia hoja hii Bowlby (1969) anaeleza kuwa:

> "Ukuaji wa wanadamu hasa watoto hukamilika vizuri wakiwa karibu na mtu wanaomwamini na kumpenda."

Jambo hili ni kinyume na ilivyo katika *Kipimo Cha Mizani*, Umari anawachukua watoto wa nduguye Amini baada ya kifo chake na kuwatenganisha na mama yao. Anapowachukua watoto hao na kuwapeleka kwake, hawakuelewa ni kwa nini mama yao asiwachukue. Anapokuja kuwachukua, ugomvi kati yake na baba yao mdogo unawashtua na kuwaliza. Kilio chao chao kinazidi wanapoona mama yao akishikwa na polisi (Uk. 97). Zaidi ya hayo,wanasononeka zaidi wanapoachishwa shule na kulazimika kukaa nyumbani na kufanyishwa kazi nyingi na Mariyamu. Hawapewi nafasi ya kucheza na wengine wala kutoka nje.

> Walijiona kamawafungwa wasio na haki yoyote ikiwemo
> Ya kusema (uk 105)

Ali anawajibika kuwatunza na kuwalisha nduguze na kuwafanyia kazi ili wasiadhibiwe. Utengano huo unasababisha madhara makubwa. Kila mara Ali anawaza mahali mamake aliko na mara humwota usingizini. Mawazo haya

yanazidisha hamu ya kutoroka na kwenda kumtafuta mamake. Anapofanya hivyo anaadhibiwa vibaya sana, anaporudi. Baadaye anapoitwa na ami yake anakereka zaidi anaposikia sauti ya Mariyamu ikimwambia:

> Muongo, mama yako umekwenda kumtafuta wapi. Basi kama hujui mama yako amekwisha kufa, wala humwoni tena." (Uk. 116).

Baba yao mdogo ambaye aliyejidai kuwa angewatunza anajitenga nao na hakuingiliana nao. Kwa hivyo, hawangeweza kumwuliza chochote kuhusu mama yao. Baadaye, mama yao anatoroka hospitalini alikokuwa amepelekwa kwa kisingizio cha ugonjwa. Watoto wanafurahi sana kwa kumwona. Polisi wanaporudi kumchukua, watoto wanapigana nao, lakini wanashindwa nguvu na kurejeshwa ndani ya nyumba. Ali hakujali tena vitisho vya Mariyamu hata anapowatisha kuwa angewaitia polisi, alimjibu "Bora" Uk. 151. Kilio cha daima, huzuni na wasiwasi ni miongoni mwa ishara zinazombainisha mtoto anayetendewa dhuluma hii.

Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani Mapunda anamtusi na kumdunisha Kongowea pakubwa. Anamwita

> "kikojozi" au "Mwanaharamu" (Uk. 8)

Matusi haya yanamkeketa maini na kumkosesha furaha daima. Huko shuleni, binamu zake Butambo, Daniel na Rehema hawakutaka kunasibishwa naye. Baada ya kifo cha mamake, Kongowea analazimika kwenda kuishi kwa mjomba wake Kitwana. Bibiye Kitwana anaanza kumtesa kwa kumfanyisha kazi nyingi

zinazoishia kumnyima hata wakati wa kusoma. Yote anayavumilia bila kulalamika akitarajia kuwa siku moja atatoka huko kwa mjomba wake. Binamu zake hawapewi kazi nyingi kama yeye. Mbele ya Mwanasaumu, anaonekana kama masimbi au matapishi na pengine alihisi kitefutefu kila anapomuona. Kijana huyu hakuwa na mahali pengine pa kuenda wala hakuwa na mtu mwingine wa kumtegemea kwa mahitaji ya kila siku. Si shule wala nyumbani, hakuweza kukaa kwa raha. Kitwana anapofunga karakana yake baada ya kuugua, bibiye anaanza kulalamika. Anasema kuwa fedha anazopata kwa ususi zinafaa kukidhi maslahi mengine muhimu kuliko kulisha na kunenepesha 'kupe' kama Kongowea na mjomba Kitwana. Mwanasaumu anamwona Kongowea kama mtoto asiyetakikana. Gielles, (1973) akichangia hoja hiyo anaeleza kuwa:

> "mtoto asiyetakikana huchukuliwa kama mzigo
> Usiotakikana,mfadaiko na chanzo cha usumbufu"
> (tafsiri ya mtafiti)

Selemani Mapunda anapomtisha kwa kumwua baada ya yeye kutolewa jela, wasiwasi mwingi unamwingia na hamu ya kuhama Tanga ikazidi. Anaamua kumwambia mjomba wake sababu za kuhama na siri kuhusu babake kama alivyoelezwa na Bi. Rahma.

### 2.1.3 Unyanyasaji wa Kimapenzi

Aina hii ya dhuluma hueleweka kama uhusiano wa kimapenzi na mtoto. Inaweza kuwa kwa njia ya ngono au kumpapasa kwa nia ya kufanya mapenzi,(Finkelhor 1984). Ni kweli kwamba watoto hukumbwa na uovu huu unaosababishwa na

watu mbalimbali. Mara nyingi huweza kujikuta katika mazingira ambayo huwafanya wawe windo rahisi la wadhulumu wao. Nelson (1987), anaeleza kuwa dhuluma za kimapenzi dhidi ya watoto huweza kutokea pamoja na aina zingine. Hivi ndivyo ilivyo katika riwaya ya *Tumaini*. Majuto (mtoto wa chifu Andrea) anaanza tabia ya kuwabaka wasichana anapofukuzwa shuleni. Baadhi ya wazazi wanapoamua kupeleka mashtaka yao mahakamani babake anayazima kwa kutoa milungula na kuwahonga mahakimu ili watupilie mbali kesi hizo (Uk. 46). Vilevile katika mtaa wa Mkwajuni, Tumaini aliwahi kusikia kuwa mara nyingi wasichana waliwahi kubakwa katika mtaa huo na wahuni. Vitendo hivi vinasababisha madhara makubwa kwa watoto. kutokana na sifa hii mbaya kijiji hiki kinaogopwa na watu, hasa watoto.

Chifu Andrea ana tabia ya kuwatongoza waajiriwa wa kike wa nyumbani mwake. Baadhi ya wasichana anawapachika mimba na wengine anawafadhili kuharibu mimba hizo (Uk. 46). Ili kuziba uovu wake wasichana wengine anawatishia maisha yao iwapo wangethubutu kumsema. Uhusiano wa karibu na watu kama Chifu Andrea, ndio Finkelhors (1991) anaouelezea kuwa:

> "wasichana wanaotokana na familia zisizo thabiti huweza kuwa windo rahisi la wanaume wazinzi". (Tafsiri ya mtafiti).

Mahitaji fulani huwafanya wasichana wadogo kutaka kuajiriwa kama wasaidizi wa nyumbani. Nia ya kutaka kuwapunguzia walezi wake mzigo wa kifedha atakapokuwa akienda katika shule ya upili, unamfanya Tumaini aamue kwenda

kufanya kazi kwa Andrea. Chifu alianza kwa kumletea zawadi ndogo ndogo. Siku moja alimjia na kutaka kumbaka. Kwa ghafla chifu alimrukia kama kozi na kujaribu kumbusu huku akihema na kumpapasa mwili mzima. Tumaini alishangazwa na kitendo cha mzee huyo. Ili kujinasua alipiga unyende uliomfanya chifu amwachilie.

Vilevile anajikuta taabani, mtotowe chifu anapomshika na kutaka kumbwaga chini. Ili kujinasua, anampiga majuto katika sehemu ya kinena kwa kiwiko cha mkono. Kwa kuhisi maumivu Majuto anamwachilia. Akatoka akiapa kuwa angemuonyesha yeye ni nani. Tishio hili linaashiria kuwa, Majuto angepanga mikakati mingine ili kuhakikisha kuwa amefaulu kumbaka Tumaini.

Ingawa watoto wa kike ndio wanaokabiliwa na tatizo hili, watoto wa kiume hawajaepuka kudhulumiwa kimapenzi. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Kongowea anajikuta katika hali ya kudhulumiwa anapofika Mombasa. Anaandamana na Amina hadi kwake. Huko kuna wanawake wanaokaa kiholelaholela. Mmoja wao anamtaka Kongowea akidai kuwa amempenda sana. kisha akamshika Kongowea na kumvuta kuelekea chumbani mwake. Amina akamshika Kongowea kiuno na kumvuta. Haja ya mwanamke huyu ilikuwa kufanya mapenzi na Kongowea. Jitihada zake zinapogonga mwamba akasema:

> "Hukumbuki umenipokonya wangapi? Leo wahaja kila Pembe,wa kufyota hakuna....kesho hiyo itakwisha"
> (uk 52)

Usemi huo unaonyesha hasira anayokuwa nayo mama huyo baada ya kumkosa Kongowea. Pia inaonyesha kuwa nia yake ya kumtaka Kongowea ni mapenzi ya kimwili. Wanapokula, Amina anatoa nguo na kuogea ndani ya nyumba bila kumwogopa Kongowea. Baadaye akamkaribisha kitandani huku akimwambia:

> "Kwani kuna ubaya gani. Sisi ni maharimu ... Isitoshe wewe ni kijana mzuri sana, hakuna cha kutuzuia" (Uk. 58).

Maneno haya ya Amina kumshawishi Kongowea ili akubali wafanye mapenzi yanaweza kuchukuliwa kama nia ya kutaka kumdhulumu kimapenzi.

Amina anadhulumiwa kimapenzi na babake wa kambo. Kitendo hiki kinatendeka mamake anaposafiri Sumbawanga kumwona kakake na kumwacha Amina pamoja na babake wa kambo. Usiku ulipoingia baba huyo alijichoma chumbani mwa Amina na akambaka. Jitihada za kutaka kujiokoa hazikufaulu kwa vile baba huyo ana nguvu kumshinda Amina (Uk.56) .

### 2.1.4 Kutowatunza Watoto

Kutojali kuwashughulikia watoto mahitaji yao ya kila siku kunachukuliwa kuwa dhuluma dhidi yao. Mahitaji haya ni kama vile: chakula, nguo, kiafya, kihisia na kuwaelimisha (Benedictis na wengineo 2006). Utunzaji wa mtoto humsaidia kukua vyema. Wajibu wa wazazi kuwafunza watoto maadili mema hujitokeza wakati huu. Kwa mujibu wa Ciccheti (1983), watoto wasiotunzwa vizuri utotoni

huishia kutopata maadili mema na wengine huingilia vitendo viovu. Mojawapo ya utunzaji huu ni kuwaonyesha mapenzi ili wahisi kuwa salama.

Katika riwaya ya *Yatima*, shangazi anakataa kumshughulikia Katiwa kiafya. Katiwa anapomwambia kuwa ana maumivu ya tumbo anamdanganya kuwa Mam' Peter angempeleka hospitali. Yeye hachukui hatua ya kuzungumza na mama huyo. Haja yake kubwa ni kuchukua pesa za Katiwa. Naye Mam' Peter anapojua kuhusu maumivu ya Katiwa hamjali. Kwa madharau, anamjibu ifuatavyo:

> "Basi kwa nini shangazi yako huyo hakukupeleka kwa daktari mwenyewe" Uk. 62.

Mama huyo bali na kutojali maumivu ya Katiwa, anaendelea kumwachia kazi nyingi za kufanya. Maumivu hayo yanatokana na kile chakula anachokula. Mam"Peter hajali kama kimeharibika au la. Siku moja umeme ulipotea na chakula cha akina Peter kilichokuwa katika friji kikaharibika, aliamrisha kitupwe lakini kile cha Katiwa alikataa kisitupwe huku akisema:

> "Hapana! Hiki chako hakiharibiki, ni kizuri tu, chakula kinachoharibika ni cha akina Peter tu, wewe utakula hiki hadi kimalizike" (uk. 57)

Hali hii ni ya kutojali kabisa. Anawajali watoto wake mwenyewe lakini hamjali Katiwa hata kidogo ingawa walikuwa wa umri mmoja na Peter. Hakuna uwezekano wa chakula kuharibika na kingine kisiharibike. Mam" Peter anajua kuwa chakula hicho kinaweza kuwadhuru watoto wake pamoja na katiwa. Lakini anamkataza katiwa dhidi ya kutupa chakula kinachokuwa chake. Hata anaposingiziwa na Peter kuwa ndiye aliyeiba pesa, anampiga vibaya sana na

kumfukuza usiku (Uk. 64). Hajali hatari ambayo inaweza kumpata Katiwa wakati huo wa usiku. Ingawa shangazi anamchukua na kumlea Katiwa baada ya wazazi wake kuaga, hajali kumpeleka shule, ilhali watoto wake mwenyewe Maria na Kelvin wanaenda shuleni.

Katika *Tumaini*, Masumbuko hajali maisha ya awali ya watoto wake. Bali na kuwalea kikatili, hajali kuwaelimisha zaidi ya shule ya msingi. Anapanga mpango wa kumpasha Tumaini tohara kisha amuoze. Vilevile Rehema anapashwa tohara na kuozwa kwa Mzee Shauri. Anafanya hivyo ili ajipatie pesa za matumizi yake ya starehe. Anakataa kumlipia karo Tumaini anapoitwa katika shule ya upili. Anapanga mpango na Chifu Andrea wa kulitoa jina la Tumaini katika orodha ya wale watoto watano waliofanya vyema na ambao wangepata ufadhili wa serikali (Uk. 70). Lengo la kufanya hivyo ni akose karo ya shule kisha amuoze baadaye. Ingawa anapata pesa nzuri kutokana na mauzo ya shamba lake, anashikilia kuwa masomo ya wanawake hayana maana kwa vile lazima wangeolewa baadaye.

Ingawa watoto wa Amini katika *Kipimo Cha Mizani*, wanafurahia kwenda shuleni, furaha hii inakatika wanapochukuliwa na baba yao mdogo bila hiari ya mama yao baada ya kifo cha baba yao. Umari anajifanya kuwa angewatunza vizuri kuliko mama yao, lakini lengo lake ni kurithi mali ya nduguye Amini. Baada ya kufaulu kufanya hivyo, bibi yake Mariyamu anawaachisha shule kwa kisingizio kuwa hana wakati wa kuwatayarisha asubuhi (Uk. 104). Ali ambaye ana umri wa miaka tisa

anaachiwa mzigo wa kuwatunza ndugu zake. Kwa kukosa utunzaji bora, watoto wanakonda na kubadilika miili yao. Hata nguo zao si nadhifu kama zamani kwani wanajivalisha wenyewe nguo yoyote inayokuwa karibu (Uk. 106). Bibi huyo anawanyima chakula kama mojawapo ya njia za kuwaadhibu. Spinetta na Rigler (1972) wanauchukulia mtindo huu kama mtindo hafifu wa kuwaadhibu watoto. Watoto wachanga kama hao huhitaji kupewa chakula bora ili kudumisha afya yao . Mariyamu angeeelewa kuwa umri mdogo wa watoto hao, haungewawezesha kufanya kazi nyingi kama anavyotarajia. Baadaye anawafukuza watoto hao nyumbani kwake bila kujali yatakayowafika. Hawana msaidizi mwingine kwani mama yao walikuwa wamemzuia hospitalini.

Katika riwaya ya *Siku Njema,* Mwanasaumu hamjali Kongowea. Ingawa ni mtoto mdogo, anamfanyisha kazi nyingi bila kujali umri wake. Kazi hizo zinamkosesha hata wakati wa kusoma. Ingawa mama yake ameaga dunia, bibi huyo hamtunzi Kongowea. Anakiuka hali inayodhaminiwa sana katika jamii. Kama wanavyoeleza Bloom na Ottong (1987), kuwa watoto huchukuliwa kama wanajamii wa ukoo mpana. Kulingana na kauli hiyo, watoto wana haki ya kutunzwa na kulindwa na aila zao. Dhana hii inafafanua kuwa wanajamii wana jukumu la kuwasaidia watoto ambao wana shida mbalimbali. Kongowea anapopita mtihani na kuitwa katika shule ya upili, mkazamjomba huyo anakataa kumlipia karo ya shule ingawa ana uwezo wa kifedha.

Hali ya kutotunza na kutojali watoto huweza kubainika kwa vitendo wanavyotendewa watoto kama vile: kutopelekwa hospitalini wanapougua kama Katiwa anavyofanyiwa, kulishwa chakula kinachovunda, kutoruhusiwa kwenda shuleni, mavazi yasiyo nadhifu na watoto wengine kama Kongowea huishia kuanza kufanya kazi wakiwa na umri mdogo.

## 2.2 SABABU ZA UTEKELEZAJI WA DHULUMA DHIDI YA WATOTO

### 2.2.1 Ufuasi wa Tamaduni za Kijadi

Utamaduni wa jamii yoyote unahusu imani, sherehe, tambiko na tamasha za jamii hiyo. Kwa hivyo, kuwa mmoja wa jamii fulani ni kushiriki katika mambo hayo yote (Mbiti 1989:2). Ni vigumu kwa mtu yeyote kujitenga na utamaduni wa jamii yake. Mojawapo ya sherehe iliyotiliwa maanani sana baadhi ya jamii hapa nchini Kenya, ni kupashwa tohara kwa watoto wa kiume na wa kike. Sherehe hii ilitarajiwa kufanywa mara tu mtoto alipofika umri wa miaka kumi na mitano (Adegbola 1983:74). Sherehe hii ilihusu ukataji wa sehemu fulani katika sehemu za siri za watoto wa kiume na wa kike. Mbiti (1989) anaeleza kuwa sherehe hii ilikuwa na umuhimu wa kipekee katika maisha ya mhusika, kwa vile ilikuwa ni ishara ya kuacha maisha ya utoto na kuingilia maisha ya utu uzima. Anayetahiriwa alipata mamlaka mapya katika jamii kwa vile alipata kibali cha

kushiriki katika mambo muhimu ya jamii kama vile kwenda vitani kwa vijana wa kiume, na kujua siri za jamii ile. Vilevile ilikuwa kama kuwaingiza katika majukumu ya watu wazima kama vile kuoa au kuolewa na kuiendeleza jamii. Mafunzo muhimu kuhusu mambo mbalimbali yalipitishwa kwao baada ya kupashwa tohara. Mafunzo hayo yalihusu jinsi ya kukaa kwa amani na watu wote, kutunza jamii na kuheshimu wazee, baadhi ya mengine. Ili kufanikisha sherehe hii, jamii nzima ilihusika katika kutayarisha sherehe hii. Baada ya sherehe hii, mzazi wa mtoto aliyehitimu vizuri aliheshimiwa na wengine kwa vile iliaminiwa kuwa alifanya kazi nzuri katika kumtayarisha mtoto (Adegbola 1983). Sherehe hii ilikuwa ya lazima kwa watu wote katika jamii zilizohusika na yeyote aliyeiepuka alichukuliwa kama mtoto hata akiwa na umri mkubwa (Mbiti 1992:97). Kulingana na Oṣabuley (1990), akimnukuu Clarke (1892), iliaminika kuwa, Mungu ndiye aliyeelekeza tohara ifanywe baada ya kuumba ulimwengu kama njia ya kuwaingiza watoto washiriki katika juhudi za kuiendeleza jamii kwa kuzaa na kuwalea watoto.

Baada ya kutahiriwa, msichana alipaswa kuolewa, na mvulana alikuwa huru kuoa na kuiendeleza jamii. Ndoa ilitukuzwa na kuchukuliwa kama tendo takatifu ambalo kila mtu alipaswa kutimiza. Juhudi zote zilifanywa ili kuwandaa watu kwa ndoa, na kuwafikirisha kidoa (Mbiti 1992:104). Ili kufanikisha shughuli hiyo, wazazi walikuwa na wajibu wa kuwatafutia watoto wao wachumba na kuwaoza. Jambo hili linachangia dhuluma dhidi ya watoto. Wazazi walishikilia kuwa

lazima utamaduni huu ufuatwe. Katika ufuasi wa utamaduni huu, watoto walinyimwa nafasi ya kujiendeleza kimasomo.

Ni katika muktadha wa utamaduni huu ambapo mhusika Masumbuko katika riwaya ya *Tumaini*, anapojitahidi kuutekeleza kwa watoto wake bila kusita. Tumaini anatambua kwamba tangu shule zifungwe kulikuwa kukifanyika mambo ambayo hakuyaona kule kwao. Kila mara wazee wanakutana, wanawake nao wanakuja kila mara (uk. 17). Watu hao wote wanafanya mipango ya tohara ya yake kama ilivyohitajika katika jamii. Akiwa shuleni, anajihusisha na wasichana wanaopinga tohara. Anajaribu kuzungumza na babake ili amuelewe lakini akawa "haambiliki hasemezeki" (uk. 10). Pia mamake mdogo anajaribu kuzungumza naye ili abadilishe msimamo wa kumpasha Tumaini tohara lakini Masumbuko anamtukana na kumwambia kuwa anavunja miiko (uk.12).

Mzee Masumbuko ako tayari kutekeleza mipango yote bila kutingisika. Mamake Tumaini anapoona kuwa bwanake hako tayari kubadilisha msimamo, naye anaendelea kupanga mipango ya kumtafutia Tumaini mwanamke ambaye angekuwa somo wake. Mwanamke huyu, Mama Nemsi, anakuja na wakashauriana kuhusu jambo hilo (uk. 19). Mamake akaanza kumshawishi Tumaini ili akubali kupashwa tohara, akimshauri kuwa, hangependa kuona akichekwa na walimwengu kwa sababu ya tabia zisizolingana na maisha yao (uk. 19). Analazimika kumdanganya kuwa angeruhusiwa kuendelea na masomo

baadaye, na kumweleza kuwa hata binamuye Riziki amepashwa tohara. Jambo hili anamweleza kuwa ni mila ya tangu zamani na hawakuwa na lingine ila kulitekeleza kwa vile amefikisha umri ufaao. Anamshawishi akisema kuwa:

"Mkono usioweza kuukata ubusu" (Uk. 18).

Tumaini anajaribu kumweleza kuwa ingawa ni mila, ya tangu zamani, jambo hilo limepitwa na wakati na tohara kwa watoto wa kike zimepigwa marufuku na serikali. Mamake hashawishiki. Tohara hizi za kulazimishwa kwa kisingizio cha ufuasi wa mila za jadi, ni kuwadhulumu watoto kwa vile zingine hutekelezwa bila mapenzi yao. Bi. Namvua, shangaziye Tumaini ana mawazo kama ya babake Tumaini, ni mfuasi kamili wa tamaduni hizo.

Masumbuko anapotambua kuwa Tumaini ametoroka ili kuepuka mipango yake ya kupashwa tohara, anakasirika sana na kumtuma Idi amwambie asirejee kwake tena. Kutoroka kwa Tumaini kunachukuliwa na babake kama, jambo la aibu ambalo hangeweza kulihimili. Mpango huo unapoharibika, anaanza mpango wa kumuoza kisirisiri ili aepukane na aibu hiyo.

### 2.2.2 Mfumo wa Kuumeni

Huu ni mpangilio katika jamii unaodhihirisha uwezo na mamlaka makubwa ya wanaume dhidi ya wanawake. Mbilinyi na wengine (1985), wanaeleza kuwa

mtawala wa familia huwa mwanaume. Yeye ndiye anayemiliki na kudhibiti njia kuu za uchumi pamoja na kupanga mambo yote ya jamii yake. Kwa mujibu wa kauli hii, mamlaka yote pamoja na maamuzi yanategemea uamuzi wao. Wakishadidia hoja hii, Kabira na wengine (1994), wanaeleza kuwa baada ya kuolewa mwanamke huondoka nyumbani mwa wazazi wake na kujiunga na familia ya mumewe. Mwanamume alipaswa kulipa mahari kwa wazazi wa mke ili kuwafidia kwa kuondokewa na binti yao, na kama kitu cha kuimarisha uhusiano kati ya familia hizo mbili. Katika mfumo huu koo zilifuata jadi ya mwanamume na shughuli mbalimbali ziliongozwa na wanaume.

Nafasi ya wanawake ilikuwa finyu sana, (Nasimiyu 1994). Ni katika mfumo huu ambapo watoto wa kiume hutukuzwa na kupendelewa kuliko watoto wa kike. Familia isiyo na mtoto wa kiume ilikosa furaha. Juhudi zote zilifanywa, kama vile kuoa wake wengi mradi tu mtoto wa kiume apatikane, ambaye angekuwa mrithi wa mali ya babake na wa kuendeleza ukoo wao. Watoto wa kiume walipewa mafunzo ya jamii na jinsi ya kuongoza. Mengi ya mafundisho haya yalitolewa baada ya tohara. Wasichana walifundishwa mafunzo ya kuwaandaa kwa kazi za nyumbani kama vile: kuwatunza wototo, upishi na uvumilivu baadhi ya mengine. Gatobu (2003:2) akizungumzia hoja hii anauona mfumo huu kama mojawapo ya mambo yanayosababisha vurugu nyingi za kinyumbani, zikiwemo dhuluma dhidi ya watoto. Hii hutokea kwa vile ulipaji wa mahari huchukuliwa na baadhi ya wanaume kama kuwapa mamlaka ya kuwapiga wake na watoto kila wafikiriapo. Vilevile Nasimiyu (1994) akiunga mkono hoja

hii anaona kuwa ulipaji wa mali nyingi kama mahari huwafanya wanaume wahisi kuwa wamewamiliki wanawake kwa njia zote. Kwa hivyo kuwapa uwezo wa kuwatendea maovu wayapendayo. Ni kutokana na mwelekeo huu ambapo wanaume hufikiria kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi hata bila kushauriana na wanawake, au watoto wao.

Kupuuzwa kwa wanawake hasa wasichana huendelea hata katika shule. Wanaoshikilia msimamo huu huchukulia kuwa masomo ya wanawake hayana umuhimu wowote na ni kupoteza muda kwa vile lazima wangeolewa na kuinufaisha familia nyingine (Gatobu 2003:5). Katika masomo, kuna ubaguzi dhidi ya watoto wa kike. Wavulana hufikiriwa kuwa na uwezo mkubwa wa kimasomo kuliko wasichana. Shule za wavulana hutengewa vifaa vya kisayansi ili kuwaandaa kwa taaluma zinazofikiriwa kuwa za wanaume kama vile, uhandisi, utabibu, na zile rahisi kama vile kilimo na ualimu zikatengewa wanawake.

Kutokana na mwelekeo huu, wanaume hujitwika mamlaka ya kuwaadhibu wanawake na watoto wakosapo. Baadhi ya adhabu hizi ni, vita dhidi yao na matusi ambayo hulenga kuwatia adabu na kuwakosoa. Ni kwa mujibu wa mwelekeo huu ambapo mhusika mwalimu katika *Tumaini* anapomdhulumu Tumaini kihisia. Ingawa alikuwa akifanya vyema katika masomo ya sayansi, mwalimu anamkataza asijaze masomo ya sayansi katika fomu za usajili wa chuo kikuu akisema kuwa:

> "Nimesema masomo ya Sayansi yasijazwe. Nyie wasichana ni vigumu sana kufuzu katika masomo haya. Kwanza ni wasichana wangapi ambao mmesikia hufuzu udaktari chuo kikuu" (Uk. 90)

Mwelekeo huu uliwanyima watoto wengi wa kike nafasi ya kujiunga na taaluma kama za utabibu. Wasichana wengi huvunjwa moyo na kunyimwa nafasi za kujiendeleza katika taaluma zinazohusiana na sayansi. Pia nduguye Tumaini, Idi anaongozwa na msimamo huu wa kuumeni na mara nyingi anamuudhi Tumaini kwa kumfananisha na bidhaa za uwekezaji.

Pia anawaambia kwamba wanasubiri tu kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomeshea (Uk. 16. Tumaini anapojaribu kumweleza babake kuhusu maneno hayo ya Idi, badala ya kuchukua hatua ya kumkanya, babake anamkemea na kumuonya vikali dhidi ya kuingilia malezi ya Idi kwani yeye ni mtoto wa kiume. Tumaini anapotoroka kwao, Idi anatumwa kumtafuta. Anapomkuta kwa mamake mdogo, hasira inampanda na kuanza kumsemesha Tumaini hata bila kuwasalimia wengine. Ingawa Tumaini ni mkubwa kwa umri kuliko Idi na anawajibika kumheshimu, hamheshimu dadake Tumaini. Anaendelea kumtolea maneno ya kumuudhi kwa kumwambia:

> "Heh! Tuma leo utapambana na kikoto, Wewe waogopa ku...si Utaolewa tu"(uk27)

Babake Tumaini anashikilia kuwa na mamlaka ya kuwaadhibu watoto wake kikatili kwa vile mfumo wa kuumeni unashikilia kuwa wanawake na watoto ni mojawapo ya mali ya wanaume. Yeye hachelei kutumia njia za kikatili za kuwaadhibu watoto wake kama vile kuwatia kwa gunia iliyowekwa upupu na kuwapiga kwa fimbo hadi itakapovunjika. Dhana hii inakashifiwa na Geles (1973) kuwa, baadhi ya wazazi huchukulia kuwa kuwatia watoto adabu ni kuwapiga. Kwa hivyo mfumo huu unawapa wanaume mamlaka ya kuwadhulumu watoto wa kike kama Tumaini. Vilevile ni katika mfumo huu ambapo wazazi huwapangia watoto wao ndoa. Babake Tumaini anamtafutia mchumba ili ajiepushe na aibu. Wanapanga na rafikiye Suleimani, wamwoze Tumaini kwa mwanawe Mabruk. Tumaini haulizwi akubali ndoa hii, babake anaendelea kuipanga peke yake hata bila kumhusisha mkewe. Anajihisi kuwa na mamlaka kamili ya kumuoza Tumaini kwa vile ni mtoto wake.

Katika *Kipimo Cha Mizani,* Umari nduguye Amini anachukulia kuwa yeye ndiye angewatunza watoto wa nduguye vyema hata kuliko mama yao mzazi. Kwa kushirikiana na wakili wake, mahakimu wanahongwa ili kutoa hukumu hiyo. Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo anawachukua watoto wa nduguye na kuwapeleka kwake. Anachukua baadhi ya mali ya nduguye na kuitumia kwa mahitaji yake mwenyewe. Umari anafaulu kuwashawishi polisi kuwa Halima ni mwendawazimu, kwa hivyo inawalazimu wamchukue na kumpeleka katika kituo

cha polisi alipoenda kudai watoto wake kwa Umari. Polisi wanalikubali jambo hilo bila kufanya uchunguzi zaidi kuthibitisha madai ya Umari.

### 2.2.3 Kufurahisha nafsi zao

Watoto huweza kuwatendea wenzao madhara ya aina mbalimbali ili kufurahisha nafsi zao. Jambo hili hutendeka sana wakati wa michezo. Huenda ikawa wanajua kuwa matumizi ya maneno fulani yatawaudhi wenzao au huenda ikawa hawajui, huchukulia tu ni mchezo wa kujifurahisha.

Katika riwaya ya *Yatima,* watoto wanamwimbia Katiwa wimbo unaomuudhi sana (Uk. 54). Wimbo huo unamkejeli Katiwa kwa kutosoma kwa hivyo anaonekana mjinga mbele ya watoto wanaosoma, hali wanayoiona kama ya kuchekesha. Pia ni kama Peter anafurahia kumchezea Katiwa. Anapofika kwao, anampaka ice cream usoni. Kwa ajili ya baridi kali aliyoihisi, Katiwa analalamika, na sauti hiyo ikamtoa mamake Peter jikoni. Anapokuja kuona kinachoendelea, Peter akasema kuwa msichana mchafu anataka kumnyang'anya ice cream. (Uk. 47). Mamake alimkaripia Katiwa.

Siku nyingine akachukua maji na kuyamwaga katika kitanda cha Katiwa, akakimbia kumweleza mamake kuwa Katiwa kakojoa kitandani. Mamake akamkaripia Katiwa kelele na kumlazimisha kwenda kuanika godoro hilo. Vitendo

hivi vyote vinadhihirisha kuwa Peter anafurahia kuona Katiwa akisumbuliwa na kukaripiwa na mamake.

Katika *Tumaini*, wanafunzi wa darasa la Tumaini wanaanza kumkejeli kutokana na yale yaliyomfika wakati wa likizo. Anayezidi kumtania zaidi ni Kijungwe anapomwambia:

> "Nasikia ulichana mbuga hadi kwa mamako mdogo. Nilidhani wewe ni msichana jasiri sana wala hungeogopa kisu au ni wembe" (Uk. 59)

Utani huu ulimkasirisha Tumaini sana. Lengo la utani huu wa kijungwe ni kujifurahisha na kufurahisha wengine na kumcheka Tumaini kwa kuogopa tohara. Wengine walifanya hivyo kwa vile hawakuwa na ari yoyote masomoni na walitafuta jambo la kumkata tamaa (Uk. 38).

### 2.2.4 Kukata tamaa

Kulingana na nadharia inayoongoza utafiti huu, inasisitiza kuwa kuna baadhi ya mambo yanayoweza kutokea katika maisha ya mtu ambayo yanaweza kuwa chanzo cha kukata tamaa. Disbora na wengine(1977), wakifafanua dhana hiyo, wanaeleza kuwa mtu huweza kukumbwa na hali ngumu na ashindwapo kuisuluhisha, ukata tamaa hutokea. Naye Kelly (1983:42) anaonelea kuwa kuna ongezeko la viwango vya ukata tamaa. Ongezeko hili linaongeza viwango vya

ushari katika jamii. Kwa hivyo utekelezaji wa majukumu ya kibinafsi usipofaulu ushari huelekezwa kwa vitu vilivyo karibu, watoto wakiwemo.

Katika *Siku Njema,* tunaelezwa kuwa Selemani Mapunda ni mbumbumbu masomoni. Naye Kongowea ni mwerevu sana. Anapowashinda wenzake darasani, ingawa ana umri mdogo sana, wenzake wanaanza kumchukia na kumtukana wakimwita 'kikojozi' au Mwanaharamu (Uk. 8). Naye Selemani, inasemekana kuwa alikuwa ameenda kwa mganga kuagua kinachomfanya asiwe hodari masomoni. Aliambiwa kuwa Kongowea ndiye anayemkosesha bahati yake masomoni. Jambo hili linazidisha ukata tamaa kwa Selemani na chuki dhidi ya Kongowea ikazidi. Ikawa mojawapo ya sababu za kumtukana. Baadaye Kongowea anamsema Selemani kwa polisi alipowakuta wakimpiga Mwalimu mkuu wao. Wakashikwa na kufungwa jela. Selemani anapofunguliwa, anatisha kumwua Kongowea kwa kumsema kwa polisi. Inaonekana kuwa bado ana uchungu wa kukoseshwa bahati shuleni na Kongowea, halafu kusemwa kwa polisi na kufungwa jela. Anamuona Kongowea kama kama chanzo cha matatizo yake.

Pia Mwanasaumu bibi yake Kitwana, anamdhulumu Kongowea anapoenda kuishi kwake. Anamuonea wivu kwa kushinda katika mashindano ya hadithi. Kwa wivu mwingi anataka wanawe wawe ndio washindi (Uk. 7). Ukosefu wa ushindi kwa watoto wake unamletea kukata tamaa kunakomfanya akereke na kuungulika

ndani kwa ndani pamoja na wanawe. Wanawe Rehema, Daniel na Butambo hawakuwa werevu shuleni. Ushindi wa Kongowea unawakeketa maini kwa wivu na uchungu. Kwa sababu ya hayo binamu zake walikuwa wakimcheka Kongowea pamoja na wanafunzi wengine shuleni. Walitaka wamwumize kwa kuwashinda. Uchungu huu dhidi ya Kongowea unamfanya Mwanasaumu apange mpango wa siri na Bi. Rahma wa kumuangamiza apitapo mitihani. Bibi huyo hafurahishwi tena na ushindi wa Kongowea. Anaona bora kama ungekuwa wa watoto wake mwenyewe.

Katika *Yatima*, kuna hadithi ya Mwilu na Mwila. Baada ya kifo cha mamake Mwilu, mamake Mwila anaingiwa na wivu dhidi ya Mwilu anayeonekana kuwa shupavu kuliko mwanawe Mwila. Wivu huu unamletea ukata tamaa mwingi unaomshawishi kumwangamiza Mwilu kwa kumchimbia shimo kubwa na kuweka ngozi juu yake na kumshauri Mwilu akalie juu ya ngozi hiyo. Alipokalia alitumbukia ndani na akafukiwa kwa mchanga (Uk. 22-25).

Naye Momanyi anaeleza kuwa kuna baadhi ya wanafunzi wanaomkejeli Tumaini, hasa wale anaowashinda masomoni. Tunachukulia kuwa wivu wa kushindwa na Tumaini uliwakasirisha kwa hivyo kutaka kumkejeli, ili wamvunje moyo (Uk. 38). Wanamkejeli baada ya kujua kuwa Tumaini alitoroka kwao ili kuepuka kupashwa tohara na wazazi wake.

### 2.2.5 Ubinafsi

Hii ni tabia inayochochewa na hali ya mtu kutaka kutimiza matakwa yake bila kuzingatia hisia za watu wengine. Katika juhudi za kutimiza matakwa hayo, mtu huishia kuwadhulumu watoto wasio na nguvu za kujitetea. Mam' Peter katika *Yatima*, ana haja ya kufanyiwa kazi katika nyumba yake. Kazi hizi ni kufua, kuosha na kuwapikia watoto wake. Anapomuajiri Katiwa nyumbani kwake, hajali umri mdogo wa Katiwa wa miaka minane tu. Anaendelea kumpa kazi nyingi bila kujali kama anachoka. Hata anapomwambia kuwa anaugua, hajali kumpeleka hospitalini. Hali hii ya kutomjali Katiwa inasababishwa na ubinafsi wa mam'Peter.

Masumbuko katika riwaya ya *Tumaini*, ana ubinafsi mwingi. Azma ya kumuoza Tumaini ni kupata mahari ili aendelee na maisha yake ya ulevi.

Katika *Kipimo Cha Mizani*, mwandishi anaeleza kuwa baada ya Kifo cha Amini, Mariyamu alianza kumshawishi mumewe Umari, achuke mali ya Amini. Kwa matumizi ya hongo, anafanikiwa kupata hati ya kuwachukua watoto wa marehemu kutoka kwa mama yao. Baada ya kutwaa nyumba, duka na kiwanda cha marehemu Amini, anaanza kutumia pesa hizo kwa matumizi yake mwenyewe. Mariyamu anaona kuwa hana wakati wa kuwatayarisha watoto waende shule. Pia anaonelea kuwa masomo yao hayana maana kwa vile wanaweza kujifunza kazi za mikono kama baba yao. Kwa hivyo anawakataza kwenda shuleni na kuwagawia kazi za kuosha na kufagia kule nyumbani

kwake(Uk. 105). Ingawa anawakataza akina Ali kwenda shuleni, watoto wake wanaendelea na masomo yao kama kawaida. Anachukulia kuwa masomo kwa watoto wa Amini hayana umuhimu.

Shangaziye Katiwa katika *Yatima*, anapanga mipango ya kumpeleka Katiwa kwa Mam' Peter ili awe akienda kuchukua mshahara kila mwisho wa mwezi. Hata Katiwa hakujua kuwa shangazi yake ndiye anayepewa pesa badala ya yeye kupewa. Kwa ajili ya ubinafsi, wake, anazitumia pesa hizo kwa mahitaji yake mwenyewe bila kumgawia Katiwa. Hakuona ubaya wowote wa kwenda kumchukua Katiwa kutoka kwa babu yake na kumdanganya kuwa anampeleka kwa Kelvin na Maria ilhali anampeleka akaajiriwe. Pia wanashirikiana na rafikiye mmoja kuwakusanya wasichana na kuwapeleka kwa wanawake waliohitaji wafanyikazi. Mwandishi anasema kuwa:

> "aliongozwa na tamaa kubwa; aliongozwa na tamaa ya fisi" (Uk. 69).

### 2.2.6 Tabia mahsusi ya mdhulumu

Mtu anayetekeleza dhuluma dhidi ya watoto huenda ikawa ana tabia ya ukatili. Tabia hii humwelekeza mtu kufanya ukatili bila kujali. Akishadidia hoja hii, Kelly (1983) anasema kuwa, baadhi ya wazazi huwa wakatili kwa kupenda matusi. Vilevile Holter na Friedman (1968) wanataja tabia ya baadhi ya wazazi kuwa katili na wasiobadilishwa. Wazazi walio na tabia hizi, hawaambiliki hata wakishauriwa dhidi ya kufanya maovu. Tabia hii ya ukatili na kutopenda

mabadiliko ndiyo aliyokuwa nayo mhusika Masumbuko katika *Tumaini*. Inamfanya awatendee watoto wake ukatili mwingi. Anaelezwa kama:

> "mwingi wa hamaki ambazo zilivuka mpaka hasa alipopewa pombe". (Uk. 15).

Mtoto wake Idi alimrada sana babake kwa tabia ya wingi wa ukatili na hamaki, aliokuwa akiutolea dada zake wakubwa. Pia ni mgumu, haambiliki wala kusemezeka (Uk. 10). Kwa sababu ya tabia hii watoto wake walikimbia na kujificha kila aingiapo nyumbani akiwa mlevi kwani aliwapiga kwa makosa mandogo tu. Tabia hii ya kikatili ndiyo inayomfanya Tumaini achukue hatua ya kutorokea kwa mamake mdogo. Kwa ajili ya ugumu huu Mzee Masumbuko anakataa ushauri wa wazee wenzake wa kumsihi afuate uamuzi wa kupiga marufuku mila hii ya tohara lakini anakataa katakata (Uk. 24).

Mhusika mwingine aliye na tabia ya uzinzi ni Chifu Andrea. Anapenda kuwatongoza waajiriwa wa kike wa nyumbani mwake. Wasichana wengine aliwapachika mimba na wengine kuwafadhili kuharibu mimba hizo. Kwa tabia hiyo yake, anawadhulumu wasichana wengi kimapenzi. Vilevile mtoto wake Majuto ana tabia kama za babake. Anapofukuzwa shuleni, anaanza kurandaranda mitaani akiwababaka wasichana (Uk. 46). Kwa hivyo, uhusiano wa karibu na watu wazinzi kama Majuto na babake huwafanya watoto kuwa windo rahisi kwao.

Mhusika Zainabu katika *Siku Njema,* anaeleza kuhusu tabia ya kibinafsi ya Mwanasaumu kama mwenye inda na asiye na moyo safi (Uk. 18). Mamake Kongowea anapoaga dunia anafurahi ndani kwa ndani kwa msiba uliomsibu Kongowea. Hakutaka bwanake amsaidie dadake Zainabu anapokuwa mgonjwa. Kwa ajili ya tabia hii, anamfanyisha Kongowea kazi nyingi na kumtesa sana anapoenda kuishi kwake baada ya kifo cha mamake. Pia Amina anaieleza tabia ya babake wa kambo kama mfidhuli na mwenye ukware ( uk 56). Tabia hii ya ukware ndiyo iliyomfanya ambake bintiye walipoachwa peke yao nyumbani baada ya mamake Amina kwenda safari ya muda mfupi.

Katika *Kipimo Cha Mizani,* kuna Umari nduguye Amini, ni mbadhirifu anayependa vitu ghali. Kila mara anamuendea nduguye Amini akimshauri amkopeshe pesa za matumizi au wauze baadhi ya mali waliyorithi kutoka kwa baba yao. Bibi yake Mariyamu ni kama mumewe. Tabia hii yao inadhihirika wazi wanapowachukua watoto wa Amini na kushindwa kuwatunza vyema.

Tabia ya mhusika babu katika *Yatima,* inaelezwa kama mtu mbaya asiyeshirikiana na watu. Shangaziye Katiwa alionywa kuwa kutokana na tabia hiyo mbaya ya Mzee Kiseku, Katiwa angesumbuka sana (Uk. 4). Hayo ni kweli kwa vile wanapofika, babu anamkataa Katiwa. Jambo hilo linamletea Katiwa usumbufu mwingi wa akili. Kwa hivyo mdhulumu huweza kumdhulumu mtoto

kutokana na tabia yake ya kuwa mbaya. Ubaya huu huendelea kuwatendea watu anohusiana nao hasa watoto.

### 2.2.7 Utegemezi

Kuna mikasa mbalimbali inayowakumba watoto. Mojawapo ya mikasa hiyo ni kuwapoteza wazazi. Wazazi wanapoaga dunia huwaacha mikononi mwa jamaa na wahisani wengine wanaowachukua na kuwatunza. Mzigo wa kuwatunza pamoja na watoto wao wenyewe, huwa mkubwa. Bishop (1971) akiendeleza hoja hiyo anasema kuwa, familia kubwa huwa mzigo mkubwa kwa wazazi au walezi na huwa vigumu kuwatimizia mahitaji yote. Watoto wengine huanguka mikononi mwa walezi wabaya. Ile hali yao ya kutojiweza huweza kuwafanya wavumilie baadhi ya vitendo wanavyotendewa kwa kuhofia kufukuzwa nyumbani.

Burhani katika *Kipimo Cha Mizani,* anaeleza kuwa, Ali na nduguze hana mtu mwingine wa kumtegemea baada ya mama yao kushikwa na kupelekwa polisi. Baba yao mdogo anawachukua na kuwapeleka kwake. Mariyamu havumilii kuwahudumia watoto wale wote. Anawaona kama mzigo mkubwa kwake. Kwa hivyo, anawaachisha shule ili mzigo wa kuwatayarisha, kuwapeleka shuleni, ulipaji wa karo na kuwachukua umpungukie. Adhabu za kuwanyima chakula na

kuwapiga mara kwa mara, ni thibitisho tosha ya chuki ya ulezi aliyokuwa nayo Mariyamu.

Naye Wamitila katika *Yatima* anaeleza kuhusu Katiwa ambaye ni mtoto yatima. Baada ya kifo cha wazazi wake anachukuliwa na shangazi yake Juliana (Uk. 1. Baadaye, Juliana analazimika kumpeleka Katiwa kwa babu yake huko mashambani. Aliona kwamba:

> "Nitalazimika kuhamia huko kwa sababu kima ni mbali sana na Bambo, na isitoshe nyumba niliyoipata huko kima ni ndogo sana. Inatutosha mimi na wanangu wawili, Kelvin na Maria" (Uk. 1)

Kutokana na hayo, tunaweza kuchukulia kuwa Katiwa ni mzigo kwake, na analazimika kuutua kwa kumpeleka mashambani kwa babu yake. Naye babu anamkataa Katiwa kwa vile angepata kazi ya ulezi ambayo hakuwa tayari kuifanya wakati huo. Ingawa anabadilika baadaye, anaendelea kumtunza shingo upande.

Mwanasaumu katika *Siku Njema*, anamtesa Kongowea anapoenda kuishi kwake kwa vile anahisi mzigo wa kumtunza Kongowea na mjombake Kitwana ukimlemea. Baada ya Kitwana kuugua na kulazimika kufunga karakana yake, bibi yake anaendelea kulalamika (Uk. 25). Malalamiko hayo yote, Kongowea anaelewa kuwa yanamlenga yeye. Mateso hayo yote yanayoelekezwa kwake kama njia ya siri ya kumfukuza. Kama alivyosema Kongowea "akufukuzaye hakwambii toka" (Walibora 1996:25).

## 2.3 Hitimisho

Sura hii imejadili aina mbalimbali za dhuluma zinazotendewa watoto katika vitabu vilivyoteuliwa. Jinsi mbalimbali za kubainika kwa dhuluma hizo zimetolewa. Lengo la kuonyesha namna dhuluma hizo zinavyobainika lilikuwa kurahisisha utambuzi wake. Sababu mbalimbali zinazosababisha utekelezaji wa dhuluma dhidi ya watoto zimejadiliwa. Watoto hukabiliwa na aina nne kuu za dhuluma. Hizi ni dhuluma zinazoumiza viungo vya mwili. Aina hii husababisha majeraha mbalimbali mwilini. Dhuluma za kimapenzi, huhusu kuwalazimisha au kutumia njia za hila ili kuwashirikisha watoto katika mapenzi ya kimwili. Mdhulumu hulenga kutimiza haja zake za kimwili. Matumizi ya nguvu yamedhihirika kuwa mojawapo ya njia zinazotumiwa kufanikisha dhuluma hii. Dhuluma nyingine inayojitokeza ni ya kihisia. Hii humwumiza mtoto kihisia, matumizi ya maneno ya kuudhi kama vile matusi, kukejeli na masimango hutumika. Kutotulia, wasiwasi na kulia daima ni ishara zinazoibainisha dhuluma hii. Utafiti umedhihirisha kuwa aina hii huweza kujitokeza sambamba na dhuluma zingine.

Katika aina hii ushari wa wazi na wa siri huweza kujitokeza. Katika dhuluma za kutomtunza mtoto, dhuluma huweza kutokea, utunzaji umejitokeza kuwa wa kihisia na kimatumizi. Uchafu, njaa na nguo zisizofaa ni baadhi ya mambo yanayoibainisha. Katika sura ifuatayo tutajadili athari za dhuluma kwa watoto

pamoja na kutambulisha asasi mbalimbali zinazohusika katika utekelezaji wa dhuluma .

## SURA YA TATU

## UTEKELEZAJI WA DHULUMA DHIDI YA WATOTO

## NA ATHARI ZAKE

### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tutabainisha wanajamii mbalimbali wanaotekeleza dhuluma kwa watoto. Lengo la kuwabainisha ni kuwa baadhi yao hutekeleza vitendo hivi kwa visingizio vya kuwaadilisha watoto au kuwatunza ilhali baadhi ya vitendo vyao vimepita mipaka iliyokubaliwa na jamii. Vilevile tutachunguza athari za dhuluma katika maisha ya watoto. Kuna athari za muda mrefu na athari za muda mfupi kama waelezavyo Lynch na Roberts (1982). Dhuluma hizi huweza kuwaathiri watoto kwa muda mrefu baada ya kutendeka. Kwa mujibu wa Glaser na Frosh (1993), utambuzi wa asasi zinazotekeleza dhuluma ni muhimu ili kuweza kuwalinda watoto kutokana nazo. Waandishi walioteuliwa wameeleza kuwa kuwa baadhi ya wadhulumu ni kama wafuatao:

### 3.1.1 Wazazi

Wazazi katika muktadha huu, wanachukuliwa kuwa ni wazazi wa kibayolojia wa watoto. Wanaweza kuwa akina baba au akina mama. Hawa huweza kuwadhulumu watoto wao wenyewe. Wengine wanaweza kuwa wazazi wa kambo wa mtoto, wazazi au wafadhili. Jones na wenzake (1982:218) wanaeleza kuwa kuna tabia mbalimbali za wazazi wanaowadhulumu watoto

wao. Kuna wale wanaofuata kwa ukaribu sana kanuni za kijamii zilizowekwa juu ya malezi ya watoto. Mifano ya kanuni hizo ni kama vile:upashwaji wa tohara,kuozwa baadhi ya mengine. Hawa hutarajia watoto wao wafuate kanuni hizo bila kuzikiuka hata kidogo. Wazazi hawa huzua mbinu zozote za kuhakikisha kuwa aila zao zinafuata kanuni hizi. Mara nyingi misimamo yao huwa chanzo cha kutoelewanwa kwao na aila zao. Mhusika Masumbuko katika *Tumaini*, yuko katika kikundi hiki cha wazazi. Ni mfuasi kamili wa tamaduni za kijadi. Ili kuwatayarisha wanawe kwa maisha ya utu uzima aliwatengea majukumu mahsusi (Uk. 16). Kulingana naye, watoto wa kiume wanatarajiwa kuwa na moyo mgumu kama yeye ili waweze kuyakabili maisha ya baadaye. Ni kutokana na msimamo wake anapokosa kuyasikiliza mawazo ya mwanawe Tumaini kuwa anataka kuendelea na masomo, lakini Mzeee Masumbuko ana mpango wa kumpasha Tumaini tohara kisha amuoze. Mamake Tumaini naye pia anaamua kuungana na mumewe katika kutekeleza kanuni ile. Ako katika kikundi cha wanawake wanyamavu wasiopenda rabsha.

Kuna kikundi kingine cha wazazi ambacho ni cha wazazi wa kambo. Hawa hawana uhusiano wowote wa kidamu na watoto lakini ni watoto wao kwa mujibu wa ndoa. Baadhi ya wazazi hawa wa kambo huweza kuwaonea wivu watoto hawa au huwachukia kutokana na sababu zao za kibinafsi. Katika

*Siku Njema,* Amina ananajisiwa na babake wa kambo. Kitendo hiki kinamhuzunisha na akashindwa kuishi naye tena. Ingawa mzee huyo alikuwa babake aliyekuwa akimtii na kumheshimu kitendo alichomtendea kilikuwa kinyume kabisa na matarajio ya Amina. Naye Mwilu katika *Yatima,* anadhulumiwa na mamake wa kambo. Mama huyo anamwonea wivu Mwilu kutokana na sura yake nzuri na kuwa na akili kuliko mwanawe Mwila. Ingawa Mwilu anampenda na kumwamini mamake wa kambo kama alivyompenda mamake marehemu, mama huyo anapanga njama ya kumwangamiza Mwilu. Motifu ya mama wa kambo na dhuluma zake ni motifu ambayo hujikita zaidi katika fasihi simulizi. Kwa hivyo wazazi wanaweza kuwadhulumu watoto wao wenyewe au watoto wao wa kambo.

### 3.1.2 Walezi

Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, watoto ni mali ya jamii nzima. Hata baada ya kifo cha wazazi wao halisi, jamaa zao huchukua jukumu la kuwalea na kuwatunza watoto hawa. Ingawa jambo hili ni muhimu katika jamii, walezi wengine huwabagua na kuwadhulumu watoto hawa.

Katika *Siku Njema,* Kongowea analazimika kwenda kuishi kwa mjomba wake Kitwana baada ya kifo cha mama yake. Mjombake Kitwana alikuwa mwenye mkono wazi, na Mwema, (uk. 5). Bibi yake Mwanasaumu alikuwa mwenye

wivu na hakutaka mumewe awasaidie watu wa kwao (Uk. 10). Hiana ya bibi huyo inasababisha utengano kati ya mumewe Kitwana na nduguye Salim. Kongowea alianguka mikononi mwa mlezi mwenye sifa hizo baada ya kifo cha mamake. Anamdhulumu Kongowea kwa ajili ya ushupavu wake masomoni ambao alitaraji kuwa ungekuwa wa watoto wake binafsi. Vilevile anamuona kama ongezeko la mzigo wa ulezi ambao haukustahili hasa baada ya kuugua kwa bwanake na akalazimika kuifunga karakana yake.

Mlezi mwingine ni mhusika Juliana katika *Yatima*. Baada ya kifo cha wazazi wa Katiwa, alimchukua Katiwa na kumlea. Baadaye aliamua kumrudisha kwa babu yake bila sababu ya kuridhisha. Hajali kumtoa kwa babu yake na kumpeleka akamfanyie kazi Mama Peter. Kila mwisho wa mwezi alikuwa akienda kuchukua malipo ya mshahara wa Katiwa, ambazo aliyatumia kwa mahitaji yake mwenyewe.

Walezi wengine ni Miriam na Umari katika *Mwisho Wa Kosa*. Hawa wanajitwika ulezi wa watoto wa ndugu yao Amini, ili waweze kurithi mali yake baada ya yeye kuaga dunia. Wanatumia hila za udanganyifu na hongo ili kupata kibali cha kuwachukua watoto wa Amini kutoka kwa mama yao. Watoto hawa wanayapata mateso mengi nyumbani kwa ami yao Umari. Lengo la ulezi wao ni kujinufaisha wao wenyewe kutokana na mali ya

marehemu. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa baadhi ya walezi hukosa huruma kwa watoto walioachwa mikononi mwao na hufikiria kujinufaisha kutokana nao. Walezi wa aina hii wameongezeka sana katika jamii ya kisasa ambapo watoto wengi wanakuwa mayatima baada ya kupoteza wazazi wao kutokana na janga la umaskini.

### 3.1.3 Watoto

Watoto wanaweza kuwadhulumu watoto wenzao. Wao hufanya hivyo kupitia kwa vitendo wanavyowatendea wenzao au vitendo vya kejeli. Katika *Yatima,* mtoto Peter anamdhulumu Katiwa anapofika kwao. Anamjia Katiwa na kitu na kumpaka usoni. Katiwa anapotoa sauti kali ya kulalamika Peter anamwambia mamake kuwa "Yule msichana mchafu alitaka kuninyang'anya Ice Cream" (Uk. 47). Siku nyingine alimwaga maji katika kitanda cha Katiwa na kumwambia mamake kuwa Katiwa alikojoa kitandani. Watoto wa Mama Peter walikuwa wakimwimbia Katiwa wimbo uliokuwa ukimuudhi sana.

Kila alipousikia wimbo huo alisikitika na kulia sana (Uk. 54). Watoto hawa wanamcheka Katiwa kwa kutoweza kujua kusoma na kuandika na hali yake ya uduni wa kuwa mtumishi wa nyumbani.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Idi anamdhulumu dadake Tumaini kwa kufuata maneno aliyokuwa akiyasikia kutoka kwa babake. Idi anawaona dada zake kama bidhaa za kuuzwa ili wazazi wao wapate mali. Maneno hayo yanamwudhi sana Tumaini. Anapokimbilia kwa mamake mdogo, Idi hakuchelea kumdharau anapomkuta huko akimwambia:

> "He! Tuma, leo utapambana na kikoto. Wewe waogopa ku ..." Uk. 27
> Idi alichukulia kuwa hatima ya mwanamke yeyote ni kuolewa tu.

Watoto wengine ni wale waliokuwa wakisoma na Tumaini. Shule zilipofunguliwa walifahamu mambo yaliyompata Tumaini wakati wa likizo. Wenzake wanamkejeli lakini Tumaini hayatilii maanani. Aliyewapiku wote alikuwa kijungwe aliyemkejeli waziwazi kwa kumtania kuwa alichana mbuga kwa kuogopa kisu (Uk. 59). Maneno haya yanamchoma Tumaini roho na kumkasirisha sana.

Majuto pia alitaka kumbaka Tumaini alipoajiriwa kwao. Kejeli zake anazijua kwani anamwonya mamake Majuto kuwa hangetaka Majuto ajue kuwa ameajiriwa kule kwao. Anamtaka amwambie kuwa anamsadia mamake akitafuta msaidizi. Tumaini anahofia kejeli zake, kama alivyokuwa akiwafanyia shuleni. Ingawa mamake alimwonya dhidi ya kumchezea Tumaini, siku moja alijitahidi kumbaka, lakini Tumaini alijiokoa kwa kumpiga Majuto katika sehemu ya kinena (Uk. 71).

Kongowea katika *Siku Njema*, anachekelewa na watoto wenzake kwa wivu wa kuwashinda masomoni. Wengine wanamramba kisogo na wengine wenye ushupavu wanambeua waziwazi, kwa kumwita kikojozi au mwanaharamu. Zaidi ya wote Selemani Mapunda anamzomea waziwazi kwa kumwita:

"Mwanaharamu msi baba" Uk. 8

Wengine wanaomcheka ni binamu zake akina Daniel Butambo na Rehema na hawatamani kunasibishwa naye. Ingawa Lynch na Roberts (2002) wanawachukulia watoto kuwa viumbe hafifu. Wanaweza kuwadhulumu wenzao kama inavyobainika katika utafiti huu.

### 3.1.4 Waajiri

Watoto huajiriwa kama wasaidizi wa nyumbani au viwandani. Patron (1983) anaeleza kuwa watoto walikuwa wakiajiriwa viwandani katika kipindi cha kuzuka kwa viwanda. Baadhi ya waajiri ni wazuri kama vile Athmani katika *Siku Njema.* Anapomuajiri Kongowea, anamtendea mema na kumlipa mshahara mzuri. Pia Amini katika *Kipimo Cha Mizani*, anamtendea Rajab mazuri anapomuajiri kiwandani kwake, zaidi ya kumpa mshahara mzuri anamnunulia baiskeli. Lakini kuna waajiri wengine wanaowadhulumu watoto waliowaajiri kama vile Mam' Peter katika *Yatima.* Mama huyo anamfanyisha Katiwa kazi nyingi sizizolingana na umri wake. Anamdhibiti Katiwa ndani ya

nyumba na hampi uhuru hata wa kutoka nje (Uk. 55). Haruhusiwi kucheza na watoto wa majirani au hata kuota jua. Anakula chakula tofauti na wengine na analia chakula chake jikoni, haruhusiwi kula pamoja na watoto wengine wa Mam' Peter. Mateso, mengine yanahusu ugomvi na hata kumpiga. Hajali kumpeleka hospitali hata baada ya kuambiwa na Katiwa kuwa anaugua, anamjibu:

> "Huu si wakati wa kuumwa na matumbo! Huu ni wakati wa kulala. Usinisumbue tena", (Uk. 58).

Ingawa ni mtoto mdogo anayefaa kutunzwa, mama huyo hamjali, anashikilia kuwa anatoa pesa zake ili ahudumiwe (Uk. 59).

Mwajiri mwingine alikuwa chifu Andrea katika *Tumaini.* Ana tabia ya kuwatongoza wasichana aliowaajiri kwake kama wasaidizi wa nyumbani. Wengine aliwatunga mimba na wengine akawasaidia kuharibu mimba hizo (Uk. 76). Pia anajaribu kumbaka Tumaini anapoajiriwa na mkewe kama msaidizi wa nyumbani. Chifu huyo anatumia cheo chake kuwanyamazisha wazazi wanaolalamika.

### 3.1.5 Waalimu

Waalimu huwa na uhusiano wa moja kwa moja na watoto wanapokuwa shuleni. Walimu wana jukumu la kuwasaidia watoto wakue wakijiamini na kujipenda, (Taasoni 2002:164). Wakosapo wanatarajiwa kuwaelekeza kwa

njia ya kuwatia moyo. Baadhi ya waalimu huwavunja moyo wanafunzi wao. Kwa mfano, katika *Tumaini*, mwalimu wa Hisabati anamvunja moyo Almasi kwa kuichora sufuri na kuitia macho pua na mdomo (Uk. 60). Kitendo hiki hakikufaa kwa vile Almasi anaendelea kulichukia somo hilo pamoja na mwalimu mwenyewe. Mwalimu mwingine ni Bw. Majaaliwa, mwalimu mkuu wa shule ya Milimani Mission School. Ana imani potofu kuwa wasichana hawawezi kufanya vyema katika masomo ya Sayansi. Anawashauri akina Tumaini wasijaze masomo ya Sayansi. Imani hiyo ilikuwa potovu kwani Tumaini alikuwa akifanya vyema katika masomo ya Sayansi. Mwelekeo huu huweza kuwalazimisha wasichana wasiingilie kazi wazitakazo na kufanya zile wasizotaka. Tumaini hakuwa tayari kuzaja somo lingine ila utabibu. Yaonekana walimu walikuwa wakiwanyima watoto haki zao kwa kuwaamulia masomo wasiyoyataka. Ni heri wanafunzi wapewe nafasi ya kujichagulia wenyewe na waalimu wawaongoze tu bila kuwalazimisha kufanya masomo wasiyoyataka.

### 3.1.6 Walinda haki

Katika jamii kuna watu walio na mamlaka ya kulinda usalama wa jamii. Wametwikwa jukumu la kuhakikisha kuwa sera za serikali zinaendelezwa ipasavyo lakini badala ya kufanya ipasavyo wanakiuka matarajio ya wajibu wao. Katika *Tumaini*, kuna mhusika chifu Andrea. Ingawa serikali imepiga

marufuku tohara za wanawake anaendelea kushirikiana na wazazi wanaoshikilia mila hiyo. Baadhi ya wazazi kama Mzee Masumbuko wanampa hongo ili wasichukuliwe hatua wafanyapo yale yanayokuwa kinyume na matarajio ya Serikali. Baadhi ya mambo anayoyafanya ni kukubali ushawishi wa Masumbuko wa kuhakikisha kuwa Tumaini hakuwa katika orodha ya wanafunzi ambao wangefadhiliwa na serikali, ili apate nafasi ya kumuoza (Uk. 77). Kwa kushirikiana na babake, chifu huyo anafanya juhudi za kumdhulumu Tumaini ili akose ufadhili wa kimasomo, kwa kuondoa jina lake katika orodha ya watoto watano ambao wangepata ufadhili wa serikali. Jambo hilo linapogunduliwa anaonywa vikali dhidi ya kushirikiana na wazee kama Masumbuko ili kuzorotesha elimu ya watoto wa kike (Uk. 82).

Katika *Kipimo Cha Mizani,* kuna mahakimu ambao wana wajibu wa kulinda sheria na haki. Hukumu wanayoipitisha kuwa Umari awachukue watoto wa nduguye na kuwalea badala ya kukaa na mamaye mzazi inawadhulumu watoto hao wachanga. Umri wao ni mdogo na wanamhitajia mama yao zaidi (Uk. 90). Kwa kuahidiwa hongo kutoka kwa Umari, wanakata hukumu hata bila ya kumsikiliza Halima, kama inavyohitajika kisheria. Walisikiliza tu upande wa Umari. Hakimu hao wangemhoji Halima ili wathibitishe kama ni mwenda wazimu kama alivyodai Umari. Hukumu hiyo iliwanyima watoto wa Amini haki ya kulindwa na kulewa na mama yao na kupata mlezi mwingine

Mariyamu aliyewadhulumu pakubwa. Tasonni (2002:172) akieleza juu ya utunzaji wa watoto anaeleza kuwa "watoto huwa na uhusiano bora zaidi wakiwa na wazazi wao halisi". Uhusiano huu ambao ni muhimu katika malezi ya watoto uliathirika baada ya watoto hao kuteganishwa na mama yao mzazi. Utafiti huu unachukulia kuwa kama asasi hii ya mahakama ingefanya ipasavyo ingezuia dhuluma dhidi ya watoto.

## 3.2 ATHARI ZA DHULUMA KATIKA MAISHA YA WATOTO

### 3.2.1 Majeraha ya mwili

Baadhi ya dhuluma kama vile matumizi ya mikono, au fimbo dhidi ya watoto huweza kusababisha majeraha ya kimwili. Wakichangia hoja hii Margan na Zeder (1992) wanaeleza kuwa "baadhi ya majeraha yanayosababishwa na wadhulumu huhitaji kutibiwa hospitalini".

Katika *Kikimo Cha Mizani,* watoto wa Amini, wanapigwa na Mariyamu. Ali anapigwa zaidi anapotoka nje bila ya ruhusa yake. Anapigwa kwa mateke na baadaye kwa henzirani. Pigo hilo linasababisha maumivu mengi mwilini mwa Ali (Uk. 115). Hata mtumishi anamwonea Ali huruma kwa ajili ya hilo.

Henzirani iliyotumiwa na mama huyo haikufaa kutumiwa kwa mtoto wa miaka tisa kama Ali. Ingawa Ali alivumilia pigo hilo hakuweza kutembea vizuri kuitika wito wa Ami yake alipokuja na kutaka kujua sababu ya kutoroka kwake. Aliendda "akijiburura kwa maumivu aliyoyaona" (Uk. 115). Mwendo huu unathibitisha ukubwa wa majeraha aliyoyapata Ali.

Katika *Yatima,* Katiwa alipata majeraha baada ya kupigwa na Mam' Peter kwa kupoteza pesa za kununua mkate. Pigo hilo lilisababisha majeraha mwilini mwake kwani hata alipoamka siku iliyofuata bado alikuwa akihisi maumivu mwili mzima. Hata jicho la kushoto lilikuwa limevimba na alishindwa kuinua mikono yake vizuri (Uk. 52). Ingawa baadhi ya majeraha hayo yalikuwa yakionekana wazi, mama huyo aliendelea kumpa kazi nyingi zaidi za kuosha vyombo na kufua nguo. Pigo hili lilisababisha huzuni kubwa kwa Katiwa na kufanya maisha yake yakose raha. Kwa kuogopa kupigwa aliendelea kufanya kazi na kuiweka hasira yake ndani akitarajia "itatoka siku moja akiwa msichana mkubwa" (Uk. 52).

Utafiti huu unachukulia kuwa huko ni kutarajia kulipiza kisasi dhidi ya mama huyo labda kwa kumpiga au kumfanyia mabaya kwa maovu aliyokuwa akimtendea. Katiwa anapigwa tena anaposingiziwa na Peter kuwa ndiye aliyeiba pesa. Mama huyo anampiga kwa mshipi kama mtu anayepiga gunia.

Kilio cha Katiwa kinathibitisha uchungu aliokuwa akiuhisi. Baadaye akamfukuza kutoka nyumbani kwake. Kufukuzwa huku kunamfanya Katiwa ateseke usiku akitafuta msaidizi, na mahali pa kulala.

Katika *Tumaini*, kuna watoto wa Masumbuko. Baba yao anawaadhibu kikatili kwa kuwapiga hadi kijiti kivunjike. Majani ya upupu aliyokuwa akiyatumia kwa kuwaweka ndani ya gunia yalisababisha majeraha mengi miilini mwao. Adhabu hii inawafanya watoto wamwogope baba yao sana. Mara nyingi iliwabidi watoto wake wamkimbie na kujificha waliposikia sauti yake akiingia nyumbani. Aingiapo nyumbani, nyumba nzima huingia tafrani kwani alikuwa akipasuka kama radi (Uk. 15). Maisha ya watoto kujificha baba yao aingiapo nyumbani hudhihirisha utomvu wa mapenzi kwake labda kwa ajili ya kuogopa kupigwa na kujeruhiwa naye.

### 3.2.2 Huzuni

Aina mbalimbali za dhuluma husababisha, huzuni, huzua hofu na wasiwasi kwa watoto. Pia huweza kuzua hisia za ukosefu wa usalama katika mazingira wanamoishi. Wakati mwingine hukosa usingizi kwa kuhofia yale yatakayowakumba wakati utakaofuata. Tassoni (2006:7) anasisitiza kuwa watoto wanapaswa kuwekwa katika mazingira yenye usalama ili wahisi kuwa wanatunzwa vilivyo. Jambo hili ni zaidi ya kuwatimizia haja zao za kila siku. Hali hii inapokuweko huchangia katika ukuaji wa watoto.

Hali hii muhimu inakosekana kwa watoto wa Amini Ali, Uledi na Baraka katika *Kipimo Cha Mizani.* Umari anapowachukua na kuwapeleka kwake, wanakaa wakiulizia alipoenda mama yao. Kutenganishwa na mama yao kunawaletea huzuni nyingi. Wanapokatazwa kwenda shuleni ilhali watoto wa Umari bado wakiendelea na masomo yao, huzuni inawazidi. Wananyimwa ruhusa ya kutoka nje na kucheza. Waliachiwa kazi nyingi ambazo walitarajiwa kuzikamilisha. Ukiukaji wa amri hizo ulifuatishwa na adhabu kali kama kunyimwa chakula na kupigwa. Kila mara Ali alikuwa akichoka sana kwa kuwafanyia nduguze kazi kwa kuchelea adhabu za Mariyamu, mtoto kama Baraka aliyekuwa mchangamfu alibadilika akawa hasemi lolote hata kuzungumza na ndugu zake. Naye Ali "alikuwa amejaa hofu na wasiwasi" (Uk. 106). Kwa ukosefu wa raha kule kwa Mariyamu kila mara alikaa akiwaza vile angeweza kujiepusha na ukali wa Mariyamu. Alilala kwa wasiwasi. Siku zote ndiye aliyekuwa wa mwanzo kuamka na wa mwisho kulala (uk.106).

Dhuluma zinazomkumba Kongowea katika *Siku Njema,* zinamkosesha furaha kabisa katika nyumba ya mjombake Kitwana. Zaidi ya kudharauliwa, kufanyishwa kazi nyingi kunyimwa wakati wa kusoma, aliepuka njama za Mwanasaumu za kumuua kwa sumu. Kwa ajili ya ukosefu wa furaha alikosa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

ladha ya chakula, hata Mwanasaumu akagundua mabadiliko hayo (Uk. 36) na akamwambia:

> "Kongowea mwanangu mbona leo umeinama sana kama kondoo? Aliniuliza. Changamka mwanangu. Niliona hata chajio hukula sawasawa." (Uk. 36).

Ukosefu huu wa furaha unamfanya Kongowea awe akitarajia kutoka kwa Mwanasaumu, siku hiyo ingekuwa njema kwake. Vile vile kwa ajili ya huzuni hii alikosa mtu wa kushauriana naye kuhusu matatizo aliyokuwa akiyapata kule kwa mjomba wake. Pia ilichangia katika tabia yake ya kuwa msiri, kwa vile aliiweka siri kuhusu babake kama alivyoelezwa na Bi. Rahma bila kumwambia yeyote. Hata anapoipokea barua ya tisho kutoka kwa Selemani hakujua amwambie mjombake au la, lakini mwishowe anaamua kumweleza.

Katika *Tumaini,*mhusika Tumaini anaingiwa na hofu na wasiwasi alipoelewa kuwa babake amepanga kumpasha tohara. Juhudi za kuzungumza naye ili amwelewe zinapoambulia patupu huzuni inamzidi hasa anapojua kuwa maisha yake ya baadaye yako hatarini. Kwa ajili ya uchungu uliokuwa moyoni mwake machozi yalimtoka kupukupu (Uk. 10). Pia Kejeli za wanafunzi wenzake zinamkosesha furaha hasa wanapomsema kuhusu yale yaliyompata wakati wa likizo. Kwa ajili ya matatizo hayo yote, Tumaini aliongeza bidii masomoni kama mojawapo ya njia za kuepuka huzuni hiyo siku za baadaye. Pia anatarajia kufanya vyema na

kufuzu ili awe daktari. Baadaye ndoto yake inatimia anapopita na kwenda kusomea utabibu katika chuo kikuu.

Naye Katiwa katika *Yatima*, anaingiwa na huzuni baada ya kutengwa na binamu zake na kurejeshwa kijijini kwa babu yake. Furaha inamwisha babu yake anapomkataa. Katiwa anaendelea kujiuliza sababu za babu yake kutotaka kuzungumza naye. Alilia sana alipofukuzwa na babu yake na akalazimika kulala katika kibanda cha mbuzi na kondoo (Uk. 9). Anapopelekwa na shangazi yake kwa Mam'Peter anahuzunika zaidi anapoona watoto wake wakienda shuleni, hata yeye alitarajia kwenda.

### 3.2.3 Kukata tamaa

Hii ni hali ya kutojali jambo lolote liwe nzuri au mbaya. Kulingana na nadharia inayoongoza utafiti huu, hali ya ukata tamaa huweza kuzua ushari. Ili ushari uwepo, lazima mhusika awe amefika katika hali ya kukata tamaa. Mtoto huweza kukata tamaa baada ya kukumbwa na vitendo vya ushari kutoka kwa watu ambao aliwaamini na hangetarajia mambo hayo yatokee. Baada ya kusalitiwa kwa uaminifu wake na watu aliowaamini na kuwaheshimu,hasa wazazi na walezi, hukumbwa na hali ya kukata tamaa. Hali hii ndiyo iliyomkumba mhusika Amina katika *Siku Njema*. Baada ya babake na mamake kutengana, yeye anafuatana na mamake anapolewa na bwana mwingine. Siku moja huyu bwana alimbaka

walipoachwa peke yao nyumbani. Kitendo hicho kilimfanya Amina akate tamaa maishani. Hali hii inabainika kwa maneno kwa maneno yake anaposema:

> "Niliingiwa na wazimu au mahoka sijui ... Lo! Mama na binti kukaangiwa kwenye kaango moja! Maisha yalikosa maana" (Uk. 56).

Unyama anaotendewa Amina na babake wa kambo unamfanya akate tamaa ya kuishi vyema duniani. Ingawa ana umri mdogo anahama kwao na kwenda Mombasa anakoanza kufanya kazi ya ukahaba. Ubaya wa kitendo hicho unamliza hasa anapomueleza Kongowea vile alivyoingilia maisha hayo (uk. 56). Tunachukulia kwamba kama hangefanyiwa unyama huo hangeingilia maisha ya ukahaba. Maisha ya Amina yaliathirika pakubwa. Alimchukia babake wa kambo kwa kiasi kuwa hata hakuwa na nia ya kuhudhuria mazishi yake. Kwa hivyo dhuluma huzua uhasama mkubwa kati ya mtoto na anayemdhulumu na wakati mwingine kwa watu wote wa jinsia ya yule aliyemdhulumu. Wanaume waliokuwa wakibisha kila mara katika nyumba ya Amina ni thibitisho tosha la jinsi alivyokuwa amejizamisha katika maisha ya ukahaba.

Mhusika Ali na nduguze katika *Kipimo Cha Mizani*, waliachishwa shule, kupewa kazi nyingi, na kupigwa. Mateso hayo yote yaliwakatisha tamaa na hawangeweza kuishi kwa furaha tena kama walivyokuwa wakiishi zamani (Uk. 107). Mama yao alipokuja siku moja furaha iliwarudia tena. Anapochukuliwa na polisi kwa ghafla, huzuni inawaingia tena. Wakaanza kulia mfululizo. Mariyamu

anapojaribu kuwatisha kuwa angewaitia polisi ikiwa hawangenyamaza, Ali alimjibu "Bora" (Uk. 151). Majibu haya ya Ali yanaonyesha kuwa amekata tamaa na hajali, liwe liwalo. Hajali kupigwa, kunyimwa chakula au adhabu yoyote ile. Anaona kuwa afadhali kupelekwa polisi kuliko kuendelea kukaa kule kwa Umari. Hata wanapofukuzwa baadaye, Ali anawaongoza nduguze wakaondoka mahali hapo kabisa.

### 3.2.4 Kutoroka nyumbani

Taathira nyingine ya dhuluma dhidi ya watoto ni kutoroka nyumbani. Kwa ukosefu wa utulivu na amani mtoto huonelea kuwa hana lingine ila kutoroka na kwenda kutafuta mahali pengine penye usalama ili aepukane na dhuluma hizo. Hatua hii huwa ya mwisho baada ya juhudi zote za kujaribu kuvumilia hali hizo kugonga mwamba.

Mhusika Tumaini, katika *Tumaini*, anaamua kutoroka nyumbani kwao baada ya kuhakikisha kuwa babake amepanga kumpasha tohara. Anajitahidi kuzungumza naye ili aelewe nia yake ya kutaka kusoma lakini babake anakataa. Mamake mdogo anapojaribu kuzungumza na babake ili abadilishe msimamo anamtusi na kumwambia kuwa anavunja miiko (Uk. 12). Tumaini anajua kuwa, baada ya tohara angetafutiwa mume na kuozwa. Jambo hili halitaki kamwe. Alipoona kuwa matayarisho yalikuwa yakiendelea na hakukuwa na matumaini yoyote ya babake kubadilisha mipango hiyo aliamua kutoroka nyumbani na kwenda kwa mamake mdogo, Bi. Halima. Alidhamiria kuwa, mamake mdogo angemuelewa

na kumsaidia. Alikitekeleza kitendo hiki kwa kuamka usiku wa manane na kuenda katika kijiji cha Miembeni. Uamuzi huu ni mgumu kwa Tumaini kwani alihofia hatua za baadaye za babake, na hakuwa na uhakika kama kweli babake mdogo alikuwa na uwezo wa kumuelimisha pamoja na mtoto wao Riziki.

Babake anapogundua kuwa Tumaini ametoroka, alituma ujumbe kuwa asikanyange kwake tena. Juhudi za kumrudisha Tumaini zinapokosa kufaulu anamkana kuwa si mtoto wake tena. Kutoroka huku kunamwokoa Tumaini kutokana na ukatili wa babake. Kwa msaada wa walezi wake pamoja na serikali, aliweza kusoma vyema mpaka chuo kikuu na kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari. Hatua aliyoichukua Tumaini ya kutoroka kwao iliyabadilisha maisha yake na kuweza kuruka vizuizi vilivyokuwa njiani. Kama hangefanya hivyo, angeozwa kama nduguze na kuishi maisha ya ukata pale kijijini kwao.

Kongowea katika *Siku Njema*, anaamua kutoroka Tanga baada ya kukumbwa na mateso mengi nyumbani kwa mjomba wake. Zaidi ya hayo, tisho la mauaji la Selemani Mapunda (Uk. 33) liliharakisha tamaa yake ya kutaka kuhama Tanga. Kongowea alimjua Selemani kama mtu mkatili na alijua kuwa angeyatekeleza yale aliyokuwa akiyasema. Alipomfichulia mjombake azma yake ya kutaka kuhama Tanga, mjombake alifikiri kuwa ni kwa ajili ya vitendo viovu vya bibi yake, na ndiyo akamuuliza:

> "Wataka kuondoka hapa kwa sababu ya huyu mwanamke"
> (Uk. 39)

Alipomwonyesha barua ya Selemani na kumhadithia chanzo cha tisho lile, mjomba Kitwana aliridhika. Baada ya kutoroka Tanga, Kongowea anaenda Mombasa. Anatamani sana aende Kitale kumtafuta babake mzazi lakini hakuweza kufanya hivyo mara moja kwani akiba ya pesa zake iliibiwa melini walipokuwa wakisafiri kutoka Tanga hadi Mombasa.

Vile vile Amina anaamua kutoroka kwao Dodoma baada ya kubakwa na babake wa kambo. Anakimbilia mjini Mombasa anakoanza kufanya ukahaba. Hangeweza kustahimili aibu ya kukaangiwa katika chungu kimoja na mamake. Hakuwa na njia ya kupata mahitaji yake ya kila siku, kwa hivyo alijiingiza katika kazi hii ili kujikimu kimaisha (Uk. 57). Kwa hivyo hali ya uhitaji pamoja na madhara ya babake wa kambo yalimwingiza katika uovu huo.

Mhusika Ali katika *Kipimo Cha Mizani*, anaamua kutoroka kwa Umari ili aende akamtafute mamake. Ingawa hakuwa na ruhusa ya kutoka nje hangeweza kuvumilia tena mateso ya Mariyamu pamoja na ndoto za mamaye zilizokuwa zikimjia usingizini (Uk. 107). Anaamua kutoroka na kuwaambia nduguze:

> "Sikiliza! Mimi nitatoka leo. Nitakwenda kumtafuta mama lakini usiseme! Usimwambie mtu yeyote hata akikuuliza" (Uk. 108).

Anatoroka nyumbani kwa kupitia upande mwingine. Kwa usaidizi wa Bakari, anamtafuta mamake bila mafanikio. Ni wakati huu alipokuwa ametoroka ndipo walipojuana na Bakari". Baadaye wanapofukuzwa kutoka kwa Umari, Bakari anawasaidia watoto hawa kwa kuwapeleka kwa Rehema walikopata malezi mazuri pamoja na kurejeshwa shuleni. Pia ni kupitia kwa juhudi za Bakari ambapo Mzee Hasani anapatikana.

### 3.2.5 Maisha mabaya

Dhuluma huweza kubadilisha maisha ya watoto yakawa mabaya zaidi kuliko yalivyokuwa hapo mbeleni. Jambo hili huthibitika kwa kuzorota kwa afya na matatizo mengine ya kimwili. Athari hii inaonekana katika *Kipmo Cha Mizani*, ambapo watoto wa Amini wanabadilika kutokana na ukosefu wa chakula pamoja na kutoshughulikiwa na Mariyamu. Afya yao inabadilika sana baada ya muda mfupi. Mwandishi anasema:

> "Watoto walikonda wakabadilika miili yao. Hata nguo zao hazikuwa nadhifu kama zamani" (Uk. 106).

Watoto hawa wanapata maisha magumu kwani hawana mazoea maisha ya kujitunza. Kila mara walikuwa na mama yao aliyekuwa akiwahudumia kwa kila kitu na walifurahia kwenda shule na kucheza na wenzao. Mabadiliko haya ya ghafla yaliwafanya waishi maisha mabaya. Adhabu za kila mara za Mariyamu pamoja na maneno yasiyokuwa na alama ya mapenzi yanawakosesha furaha na

kufikiri kuwa maisha yangekuwa tofauti kama wangekuwa na mama yao. Akishadidia hoja hii, Sidebotham (2006), anaeleza kuwa watoto wanaodhulumiwa hukua wakihisi kuwa hawapendwi na kuthaminiwa. Mtoto aliye na mawazo haya huwa na maisha mabaya na hadhi yake huwa duni kwa vile hajithamini wala kujiamini.

Katika *Tumaini*, dada zake Tumaini wanaishi maisha mabaya baada ya kuozwa mapema na baba yao. Mashaka anaozwa kwa mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Tunaambiwa kuwa,

> "Ndoa hiyo ilimsababishia Mashaka madhara makubwa ya kimwili na kiakili pia, ... Mzee huyo alikuwa na umri sawa na babake Mashaka wakawa hawasikilizani kabisa" (Uk. 96).

Mashaka anaishi maisha mabaya na mumewe kwani mumewe anamsuta kwa makosa madogo anayoyafanya. Vilevile anapata taabu ya uzazi kutokana na umri wake mdogo. Inabidi apasuliwe wakati wa kujifungua, jambo linaloathiri afya yake. Kama Mashaka hangeolewa akiwa na umri huo mdogo, labda hangepata matatizo hayo. Utafiti huu unachukulia kuwa kama hangechaguliwa mume, angejichagulia mume wa kumfaa zaidi kuliko mzee huyo wa umri sawa na babake.

Baadaye inakuwa shida kwa mzee Lusimbo kukimu mahitaji ya jamii yake alipofutwa kazi, Idi anasema kuwa:

"Hushinda akitafuta vibarua mitaani kuyakimu maisha kazi za kijungu jiko tu" (UK. 101).

Kazi hii haingetosheleza mahitaji ya jamii yote ipasavyo kwa hivyo tunachukulia kuwa maisha ya Mashaka yaliendelea kuwa mabaya zaidi. Laiti babake hangemuoza mapema hangepatwa na taabu hizi zote.

### 3.2.6 Magonjwa

Baadhi ya dhuluma watendewao watoto vinaweza kusababisha magonjwa. Katiwa katika *Yatima,* anaanza kuugua ugonjwa wa tumbo baada ya kula chakula kilichokuwa kimeharibika. Aliambiwa na Mam' Peter akitupe chakula cha watoto lakini kile chake aliambiwa hakijaharibika (Uk. 57). Baada ya kula chakula hicho, anaanza kuhisi maumivu ya tumbo na likaendelea kunguruma. Usiku huo tumbo lilimuuma sana lakini alipomwamsha Mam' Peter alimpigia kelele badala ya kumsaidia. Shangazi yake alipozuru huko siku iliyofuata akamweleza naye akamdanganya kuwa angemweleza Mam' Peter ili ampeleke hospitali. Kutokana na kazi nyingi anazofanyishwa na Mam' Peter mikono yake ilianza kumwuma (Uk. 62). Vilevile alipofukuzwa na mama huyo alikuwa amevalia nguo nyepesi ambayo haingeweza kumzuia baridi, baridi hii ingeweza kumwambukiza ugonjwa wa homa na magonjwa mengine pia.

### 3.2.7 Hitimisho

Sura hii imebainisha aina mbalimbali za wanajamii ambao huwadhulumu watoto. Imebainika kuwa watoto wako hatarini kutokana na kuweko kwa wanajamii wengi wanaowadhulumu. Ingawa wazazi halisi wa mtoto wanatakiwa kuwa walinzi bora wa mtoto, kuna wengine wanaowadhulumu watoto wao binafsi. Jambo hili ni kinyume na matarajio ya kijamii. Ingawa kuna walezi wengine wanaowalea watoto wa wengine vizuri, wengine huishia kuwadhulumu. Wengine huwaona kama mzigo mkubwa ambao haustahili na wao hutumia njia zote za kuutua mzigo huo hata ingawa ni kwa kuwadhulumu watoto walioachwa mikononi mwao.

Watoto nao huwadhulumu wenzao, labda hawajui ni kwa kiasi gani wanavyowaumiza wenzao. Baadhi ya vitendo kama kejeli vinaweza kuchukuliwa kama dhuluma.

Wanajamii wengine ni kama waajiri na walinda haki. Wao hutumia uwezo wao wa kifedha, kimamlaka na kisheria kuwafanyia watoto mabaya. Imebainika kuwa ukosefu wa sheria kama ipasavyo huchangia katika kupitisha hukumu ambazo haziwanufaishi watoto, ila huwanyima haki zao kama za urithi.

Utafiti huu umeonyesha kuwa kuna athari nyingi ya dhuluma. Baadhi ya athari hizo ni majeraha ya mwili na ya kiakili. Majeraha ya kimwili huweza kupona lakini ya kiakili huchukua muda mrefu kupona na huwaandama watoto hata wanapokuwa watu wazima. Kwa ajili ya kukata tamaa wengine hujitumbukiza katika maisha maovu kama ya ukahaba. Afya ya watoto huzorota na wengine hukumbwa na magonjwa mbalimbali.

Dhuluma pia huweza kuwa njia ya kuwaamsha ili wajikakamue na watafute njia za kuepuka matatizo hayo katika maisha yao ya mbeleni. Kuasi na kupinga dhuluma kwa kutoroka kulibadilisha maisha ya awali ya Tumaini na Ali. Wale wasiojitahidi kupinga huishi maisha ya taabu na yenye matatizo mengi.

Katika sura ifuatayo tutaonyesha namna waandishi wa jinsia tofauti walivyolisawiri tatizo hili na mapendekezo waliyoyapendekeza ili kukabilianana tatizo hili.

# SURA YA NNE

# USAWIRI WA WAANDISHI WA JINSIA TOFAUTI KUHUSU DHULUMA DHIDI YA WATOTO NA JINSI YA KUYAKABILI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inaonyesha namna waandishi wa jinsia tofauti walivyolisawiri tatizo la dhuluma dhidi ya watoto. Ulinganifu na tofauti kati ya waandishi wa kiume na wa kike umeonyeshwa. Waandishi wa kike watakaoshughulikiwa ni Burhani (2004) aliyeandika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* na Momanyi (2006) aliyeandika riwaya ya *Tumaini*. Waandishi wa kiume nao ni Wamitila (2006) aliyeandika riwaya ya *Yatima* na Walibora (1996) aliyeandika riwaya ya *Siku Njema*. Pia, sura hii inachunguza hatua zifaazo kuchukuliwa kama zinavyopendekezwa na waandishi ili kukabiliana na tatizo hili.

## 4.1 Waandishi wa Kiume

### Walibora *(1996) Siku Njema*

Mwandishi huyu anamtumia mhusika Kongowea kuthibitisha kuwa watoto wanadhulumiwa. Ingawa mamake Zainabu na mjombake Kitwana wana uhusiano mzuri, uhusiano huo unalemazwa na bibi yake Mwanasaumu. Yeye hataki bwanake awasaidie watu wa kwao. Umaarufu wa Kongowea shuleni unaanza kuonekana anaposhinda katika mashindano ya uandishi wa insha. Ushindi huu ulizua wivu katika moyo wa Mwanasaumu. Alipopata habari za ushindi huo, alinuna na hakutaka kumpa hata salamu (Uk. 7). Kulingana na mwandishi, huu

ndio msingi wa dhuluma zote alizozipata Kongowea baadaye hasa alipoenda kuishi kwa mjombake baada ya kifo cha mamake. Bibi huyu alitaka wanawe wawe washindi, kwa vile walianza kuenda shuleni mapema na walikuwa wakubwa kuliko Kongowea.

Watoto wa Kitwana wanarudiarudia madarasa hata Kongowea akawafikia na kuwapita. Inaonekana hawapendezwi na tabia ya Kitwana ya kuusifu werevu wa Kongowea. Jambo hili liliongeza wivu katika mioyo ya watoto wake Kitwana pamoja na mama yao. Kulingana na nadharia inayoongoza utafiti huu, jambo hili la sifa ni kama lililoongezea ukata tamaa katika mioyo ya binamu zake na mkaza mjomba wake. Kwa hivyo, kitendo hiki kikazaa ushari ulioelekezwa kwake. Inaonekana kama wanalipiza kisasi dhidi ya fedheha walizokuwa wakizipata kwa kulinganishwa na Kongowea anayewashinda masomoni ingawa ana umri mdogo.

Kongowea analazimika kwenda kuishi kwa mjomba wake baada ya kifo cha mamake. Kwa hivyo Mwanasaumu alipata nafasi nzuri ya kulipiza kisasi dhidi ya maumivu ya moyoni aliyokuwa akiyavumilia kwa muda mrefu. Alijua wazi kuwa Kongowea hakuwa na mahali pengine pa kwenda baada ya kifo cha mamake. Naye Kitwana alikuwa amekabidhiwa wajibu wa kumtunza Kongowea, mpaka awe mtu mkubwa na dadake (Uk. 39). Yaonekana kuwa kutokana na tabia mbaya ya Mwanasaumu, Kitwana hakumweleza wajibu huu alioachiwa na dadake kwa hivyo aliendelea kumuona Kongowea kama ongezeko la mzigo usiotakikana

kule nyumbani kwake. Watoto wake pia wanaendeleza dhuluma zao kwa kumcheka pamoja na watoto wengine shuleni hata wakikataa kujihusisha naye.

Huko shuleni watoto hao walikuwa wakiyasikia matusi aliyokuwa akirushiwa Kongowea "Mwanaharamu msi baba", na hawakutaka kumtetea. Jambo hili linaonyesha kuwa nao walipata nafasi ya kuutoa uchungu waliokuwa nao moyoni. Mwandishi amemwonyesha Mwanasaumu kama mwanamke mwenye ubinafsi na aliyejawa na wivu. Kwa ajili ya tabia hii anamfanyisha Kongowea kazi nyingi kama za kupika, kupiga deki, ilhali hakuwapa watoto wake kazi. Kazi hizi alizompa Kongowea, tunachukulia kuwa alilenga kumnyima nafasi ya kusoma ili aanguke mtihani. Maneno machafu aliyoyatoa dhidi ya Kongowea na Kitwana kama vile kuwaita 'kupe' (Uk. 25), yalimfanya Kongowea akose utulivu wa akili.

Mpango kati ya Mwanasaumu na Bi. Rahma wa kumwibia Kongowea urithi wake kwa kumtuma mpwa wake Enock Minja akajitambulishe kwa Juma Mukosi kama Kongowea, ni mojawapo ya njia za siri alizotumia Mwanasaumu kumdhulumu Kongowea. Mpango huo unaambulia patupu Enock anapokufa katika ajali ya gari huko Kitale. Wakaikosa mali na kumpoteza mpwa wake Mwanasaumu. Lawama alizozipata kutokana na watu wao kwa kusababisha kifo cha Enock, zilimkasirisha sana akazielekeza kwa Kongowea hata akakataa kumsalimia walipoenda kumlaki alipokuwa akitoka kwenye matanga hayo (Uk. 24).

Mpango huo wa kumpoka urithi ulipokosa kufaulu, walipanga mwingine wa siri wa kumwekea sumu katika chai apitapo mtihani. Labda mpango huu ulipangwa ili kumtoa duniani kabisa ili wapange mipango mingine mipya ya kuchukua urithi wake Kongowea. Tunaweza kuchukulia kuwa alitaka aondokewe na mzigo wa kumwelimisha katika shule ya upili. Vile vile mpango huu haukufaulu, Kongowea aliikataa chai kwa vile alikuwa amepewa fununu hiyo na Vumilia alipoambiwa:

> "Mwanasaumu na Bi. Rahma wanafanya njama ya kukuangamiza, jihadhari nao. Juzi nimepita barabarani nikawasikia wakisema watakutilia sumu kwenye chai pindi ukiupasi mtihani (Uk. 25).

Hii ni mojawapo ya dhuluma za siri wanazotendewa watoto. Sifa waliyopewa wanawake hawa wawili na mwandishi huyu ni ile ya motifu ya mama wa kambo. Ingawa Bi. Rahma alikuwa msiri mkubwa wa Zainabu alimsaliti mwenziwe kwa kushirikiana na Mwanasaumu wakaanza kumdhulumu mtoto wa rafikiye na msiri wake. Kitendo cha kumwokoa Bi. Rahma kutokana na fahali, ndicho kinachomzidua Bi. Rahma kutokana na ushirika wa Mwanasaumu wa kumdhulumu Kongowea. Basi, kama si hivyo, labda wangeendelea kushirikiana katika kutenda maovu mengine.

Ingawa Mwanasaumu ana uwezo wa kifedha wa kumlipia Kongowea karo katika shule ya Sekondari, anakataa kumlipia. Kwa hivyo, akaipoteza nafasi yake katika shule ya Buruguni, Dar es Salaam. Jambo hili linaonyesha umaskini na taathira zake kwa watoto. Watoto kama Kongowea huingilia kazi za sulubu wakiwa wadogo kwa ukosefu wa utunzaji bora. Pesa alizozipata baada ya kufanya kazi

hizo alimpa Mwanasaumu fungu moja (Uk. 27). Ukubalifu wa Mwanasaumu wa kupokea pesa hizi unaonyesha tamaa aliyonayo mama huyo.

Kwa kumchora Mwanasaumu hivyo, mwandishi anawalaumu baadhi ya wanawake kwa kuendeleza dhuluma dhidi ya watoto ambao si wao binafsi. Dhuluma wazitendazo hawataki zijulikane. Mwanasaumu alipoanza kumsimanga Kongowea kwa kukataa chai, Kitwana alitaka kujua kilichokuwa kikiendelea, badala ya kuambiwa ukweli aliambiwa:

> "Hamna kitu. Ni shamrashamra tu za kupita kwa mpwa wako" (Uk. 27)

Mwanasaumu hataki Kitwana ajue kuwa Rehema alikuwa akitaka chai, iliyokuwa imeandaliwa Kongowea peke yake. Haingeeleweka kwa nini alipikiwa peke yake na haikuwa nyingi ya kuwatosha watoto wote.

Ingawa dhuluma zinaelekezwa kwa watoto wasio na hatia, inaonekana kwamba mkono wa Mungu unawalinda. Kama Bi. Rahma anavyomweleza Kongowea:

> "Unayo sudi njema mwanangu, ungalikufa" (Uk. 31).

Naye Selemani Mapunda alitaka kumuua Kongowea ili alipize kisasi kwa kuchongewa kwa polisi. Tangu zamani Selemani alimuona Kongowea kama chanzo cha ukosefu wa bahati yake masomoni. Uhasama huo wa zamani, uliongezwa nguvu kwa kuchongewa huko. Walishikwa kwa kumpiga na kumwumiza Mwalimu Mkuu. Alipofungwa jela, aliapa kuwa angemuua mtu, na mtu huyo alikuwa Kongowea. Tishio hili dhidi ya maisha ya Kongowea pamoja

na mateso ya kila siku ya Mwanasaumu yanaongeza hamu ya Kongowea ya kuhama Tanga. Ingawa ana umri mdogo, analazimika kuhama Tanga na kwenda Mombasa anakoishi kwa kujitegemea. Hili ni suala la watoto wa mitaani. Kazi aliyopata ya kusukuma rukwama haikumfaa mtoto wa umri kama wake, ilimletea maradhi ya kifua kikuu. Haya ni baadhi ya matatizo yanayowakumba watoto baada ya kukosa utulivu miongoni mwa jamaa na walezi ambao wangefaa kuwatunza na kuwakimu maishani.

**Wamitila (2006):** ***Yatima***

Mwandishi huyu ameshughulikia maudhui haya ya dhuluma dhidi ya watoto kwa kumtumia mhusika Katiwa. Amefaulu kuonyesha kuwa watoto wanadhulumiwa kutokana na misingi ya utegemezi wa jamaa zao wanaowalea.

Katiwa ni msichana mdogo wa karibu miaka minane. Wazazi wake walifariki akiwa mtoto mdogo. Shangazi yake Juliana anamchukua na kwenda naye katika mji wa Bambo anakofanya kazi. Katiwa anazoeana na binamu zake Maria na Kelvin na akakua akiwa na furaha. Siku moja shangaziye alimuambia juu ya uamuzi wake wa kumpeleka mashambani alikoishi babu yake katika mlima wa Kipweke. Ingawa anakubali, ana maswali mengi, hasa babu yake anapokataa kuishi naye akisema kuwa yeye si mlezi wa watoto (Uk. 6). Anawaza kama kweli shangazi yake anampenda na kwa nini hawezi kumchukua akihamia huo mji mpya. Maswali haya na mengine yanamdhulumu Katiwa kihisia. Anakotoka ni



UNIVERSITY LIBRARY

kama hapendwi anakopelekwa anakataliwa. Hali hii inatuonyesha matatizo waliyonayo watoto hasa wale mayatima kama Katiwa.

Kuna watoto wengi mayatima katika jamii wanaokumbwa na hali kama hii. Idadi yao inazidi kuongezeka kila kukicha hasa kwa ajili ya majanga kama ya ukimwi. Jamii inatakiwa itafute njia za kuliidhibiti suala hili ili watoto hawa wasidhulumiwe. Kulingana na maoni ya Parton (1985), ni wajibu wa jamii kuwatunza watoto kama hawa. Kukataa kwa shangazi ni kinyume na maoni haya. Yeye kama mwanamke alitarajiwa kujua kwamba mtoto wa umri huo anafaa kulelewa na mwanamke siyo mwanamume kama babu. Angepata matatizo mengi kutokana na mabadiliko ya ghafla kutoka mjini alikozoea kwa muda mrefu na mashambani ambako hakukuzoea. Sababu ya udogo wa nyumba aliyoitoa kama sababu ya kumrejesha Katiwa kwa babu haikuridhisha. Tena hawakuafikiana na babu kuwa angemwacha. Alipotoka kibandani alimweleza Katiwa kuwa lazima atayapenda maisha ya pale mlimani. Alimwachia mfuko na "Alitembea haraka haraka huku akiangalia nyuma kama mtu aliyeogopa kitu fulani" (Uk. 6). Jambo hili linaonyesha kuwa alimtupa Katiwa kwa babu yake na kujiendea zake bila kujali yatakayompata. Alimuacha katika hali ya wasiwasi. Babu alibadilika baadaye na kuwa mwema kwa kuona kuwa amempata msaidizi wa kumsaidia katika utunzaji wa mbuzi na kondoo. Sababu ya kukataa kwa babu ni kutokana na tabia yake ya kuwa mwenye hasira nyingi. Tabia hii ndiyo iliyomfanya wakosane na wazazi wa Katiwa na kuwafukuza kwa

Panga. Pia alikosana na mkewe na walikuwa wakiishi mbalimbali. Mzee huyo alizoea kuishi maisha ya kipweke na kutoshirikiana na watu (Uk. 4).

Wamitila anamulika hali ngumu inayowakumba watoto, hasa mayatima. Shangaziye Katiwa aliporudi kijijini na kutaka kumchukua Katiwa babu hakuweza kumzuia, alionekana tu "akitupa mikono yake juu". Ishara hii inaweza kuchukuliwa kama kutopendezwa na usemi wa shangazi lakini hakuwa na uwezo kamili wa kumkataza. Kwa hivyo mtoto kama Katiwa aliachwa katika njia panda hataki kuwaacha babu na nyanya na pia angetaka kurudi mjini wakacheze na Kelvin na Maria. Alipomchukua Katiwa hakumpeleka kwake alimpeleka kwa Mam' Peter akamfanyie kazi. Katiwa aliyajua haya baadaye. Shangazi ndiye aliyekuwa akipewa pesa badala ya Katiwa. Hii ni biashara haramu waliyoianzisha na rafikiye mmoja baada ya hali ya maisha kuwaendea vibaya. Mam' Peter alimfanyisha Katiwa kazi nyingi kwa sababu alikuwa akitoa pesa kwa huduma hizo.

Ingawa mwajiri ana haki ya kupewa huduma na mwajiriwa wake, lazima kuwe na makubaliano ya malipo na kazi. Katiwa hakujua kama shangaziye anapewa pesa zake. Ilistahili Katiwa alipwe pesa zake mwenyewe. Waajiri hawa hawajali hali ya afya ya watoto, hata wanawafanyisha kazi hata wakiwa wagonjwa. Zaidi ya hayo wanawatusi na kuwapiga kelele waajiriwa wao. Mwandishi anamulika maisha ya dhuluma wanayoishi watoto mikononi mwa waajiri wasiokuwa na utu.

Wanalishwa chakula tofauti na wengine na hawakubaliwi kula pamoja na wengine.

Wazazi wanapowafanyia hivyo, nao watoto wao huendeleza udhalimu wa wazazi wao kwa kuwasimanga na kuwakejeli (Uk. 54). Kwa hivyo mwandishi huyu anailaumu jumuiya ya kike kwa dhuluma za aina mbalimbali zinazowakabili watoto. Kama shangazi angemtunza vizuri Katiwa hangekuwa na sababu ya kumrudisha kwa babu na baadaye kumpeleka kwa Mam' Peter. Vile vile kama Mam' Peter angemwonyesha Katiwa mapenzi hata watoto wake wangefuata mfano wake, kama Bettina alivyofanya. Watoto wa Bettina, Roda na Rita walimpenda na kumsaidia Katiwa kujifunza kuhesabu na hata kusoma (Uk. 72).

Hadithi ya Mwilu na Mwila iliyotolewa na Nyanya pia inamulika matatizo ya dhuluma yanayoendelezwa na mama wa kambo kwa watoto wasio wake. Wivu unajitokeza kama mojawapo ya sababu za kuwadhulumu watoto hao. Mpango wa kumwangamiza Mwilu unaopangwa na mamake Mwila haukufaulu kabisa. Ingawa Mwilu anamtii na kumheshimu mamake wa kambo, mama huyo anamwonea wivu, kwa umaarufu wake ulioshinda ule wa mtoto wake Mwila. Hakujali kumwangamiza kwa kumwekea mtego uliomwingiza ndani ya shimo na kisha kumzika akiwa hai. Kuokolewa kwa Mwilu baadaye kunadhihirisha ukweli wa methali "asiye na wake ana Mungu". Kutumbukia shimoni kwa mama huyo kunaonyesha malipo ya kuwadhulumu watoto wasio na hatia yoyote.

## 4.2 Waandishi wa Kike

**Burhani (2004):** ***Kipimo cha Mizani***

Katika kushughulikia swala hili la dhuluma dhidi ya watoto, mwandishi huyu amewatumia watoto wa Amini: Ali, Uledi na Baraka. Hawa wanadhulumiwa kutokana na tamaa ya ami yao Umari ya kutaka kuchukukua mali ya baba yao anapokufa. Tabia ya ami yao inajidhihirisha kama mtu anayeiishi maisha yaliyopita mapato yake. Ili kukimu mahitaji yake mengi anamtaka Amini auze baadhi ya mali waliyorithi kutoka kwa baba yao ili apate sehemu yake. Amini analazimika kutafuta pesa ili ampe sehemu yake ya nyumba, duka na baadaye shamba. Baada ya hayo, hakutosheka alikuwa akimwendea Amini na kutaka apewe au akopeshwe pesa. Amini alipomuambia kuwa hana hasira ilimpanda . Siku nyingine alienda dukani kwa Amini akitaka kuchukua baadhi ya vitu lakini Mzee Hasani alimkataza, kwa hasira Umari alisema:

> Wewe imekuhusu nini? Ninaweza kuchukua ninachotaka!" ...
> Hivyo "eh! Basi subiri utaona" (Uk. 67)

Maneno hayo ya uchungu aliyoyataja Umari yanaashiria ukata tamaa moyoni mwake baada ya kukosa alichokitaka ili atimize mahitaji yake. Anamuona Mzee Hasani kama mojawapo wa vitu vinavyozuia kutimizwa kwa malengo yake. Kulingana na nadharia inayoongoza utafiti huu, ushari unaoelekezwa kwa watoto ni matokeo ya mambo haya ya ushari uliohamishwa.

Baada ya kifo cha Amini, tamaa ya Umari na Mariyamu inaizidi. Mariyamu anamshawishi Umari achukue mali ya Amini kwa vile Halima angeweza kuolewa na mtu mwingine na yeye Umari akaachiwa dhamana ya watoto bila chochote anasema:

> "Ninavyokwambia ni kuwa uzipate hati, uwe nazo wewe mkononi mwako. Mali ni ya ndugu yako" (Uk. 82)

Maneno hayo yanaamsha tamaa ya Umari na akaanza mikakati ya kuipata mali ya nduguye. Anaona kuwa akipata hati za mahakama za kumwezesha kukaa na watoto hao angepata haki ya kurithi mali yote. Huu ni mfano mzuri wa jinsi wajane au mayatima wanavyopokonywa urithi wao. Alipata hiyo akisaidiwa na wakili wake. Hawakuweza kupata hati maalum za mali ya Amini, kwani Halima alizihamishia kwingine. Jambo hili liliwakasirisha sana na wakataka kumwondoa Halima kwa vile walimuona kama kizingiti cha mipango yao (Uk. 92). Dhuluma ya kwanza waliyoifanya ni kumwondoa Halima katika nyumba yao, akalazimika kuhamia kwa Bi. Riziki. Watoto hawakuelewa sababu ya kuhama kwao nyumbani. Baadaye Umari aliwachukua na kuwapeleka kwake na wakatenganishwa na mama yao. Wakakosa mapenzi, ulinzi na utunzi wa mama yao. Watoto wakateseka kihisia hasa wanapomwona mama yao akigombana na ami yao alipoenda kuwachukua kutoka kwake. Umari aliwaita polisi na kusingizia kuwa Halima ni mwenda wazimu (Uk. 96).

Watoto waliteseka sana baada ya kuchukuliwa na Umari. Mariyamu aliwakataza kwenda shule, aliwafanyisha kazi nyingi, kuwapiga na kuwadhibiti kule nyumbani bila kuwapa ruhusa ya kwenda nje kucheza (Uk. 98). Ingawa Umari alisikia kuwa watoto hawaendi shuleni, aliposisitiza kuwa lazima wangeenda shule, alijibiwa na mkewe:

> "Lazima ya nini? Kwani wanataka kufanya nini? Si watajifundisha kazi tu baadaye? Mimi sina wakati wa kuwashughulikia asubuhi. Ninakuwa na haraka" (Uk. 106).

Hayo ya kuwashughulikia, Mariyamu aliyajua hapo baadaye lakini baada ya kupata nyumba, duka, shamba na kiwanda cha marehemu hawakuona haja ya kuwatunza watoto. Watoto wake waliendelea na masomo yao kama kawaida. Watoto wa Amini walikosa matunzo nyumbani kwa Umari, wakaachwa wajilishe na kujiosha. Ali alilazimika kuwahudumia nduguze ingawa hata yeye alikuwa na umri mdogo uliohitaji matunzo ya mtu mzima. Ami yao hakuwa na wakati wa kuwajulia hali kwani alikuwa na shughuli nyingi (Uk. 106).

Baada ya kukumbana na hayo yote, watoto hao waliendelea kuishi kwa huzuni na wasiwasi. Waliendelea kulia na kutamani kurudi kwa mama yao (Uk. 107). Ali aliyekuwa mkubwa aliamua kutoroka na kwenda kumtafuta mama yao. Anapogunduliwa akapigwa sana na Mariyamu. Baadaye Mariyamu akawafukuza kutoka kwake walipoendelea kulia wakimtaka mama yao.

Picha inayojitokeza ni kuwa tamaa ya kurithi mali ya baba wa watoto hawa zilipofaulu hawakuwa na maana tena, haikuwa lazima waende shule na kutunzwa. Wanawake kama Mariyamu ndio wanaopanga mipango ya kutwaa urithi wa watoto wengine. Ingawa jamii inawachukulia kama viumbe wenye huruma kuna baadhi yao kama Mariyamu wasio na hisia za huruma kwa watoto wa wengine. Wao huwashawishi waume wao watende maovu ili wajinufaishe wao na watoto wao. Kuna kikundi kingine kama cha Bi. Riziki na Rehema ambacho kina huruma.

Wanaume nao wamesawiriwa kama watu wasiopenda vurugu na wake wao kuhusu malezi ya watoto. Umari hakuendelea kubishana na mkewe aliporudi na kuelezwa na bibi yake kuwa amewafukuza watoto. Alimlaumu kwa kutenda vibaya na aliposema angeenda kuwatafuta alijibiwa:

> "Ukawatafute wapi? Tena ninakwambia kabisa ukiwaona, uwatafutie pa kwenda. Lakini sio hapai .... Na ukija nao humu ndani, basi mimi nitachukua wanangu nitoke" (Uk. 173).

Kwa msimamo huu dhabiti hakudhamiria tena kwenda kuwatafuta watoto wale. Alidhamiria kuuza mali ile yote kama angekuwa na hati. Bakari naye aliwaonea huruma watoto wale walipofukuzwa na Mariyamu, aliwachukua na kuwapeleka kwa Rehema walikopata malezi mema.

**Momanyi (2006):** ***Tumaini***

Naye Momanyi ameyashughulikia maudhui haya kwa kuwatumia wahusika Tumaini, Almasi na Mashaka. Amebainisha kuwa watoto wanadhulumiwa kwa misingi ya utamaduni wa kijadi. Masumbuko, babake Tumaini ni mfuasi kamili wa tamaduni za kiasili. Pia ni mtu asiyependa mabadiliko yoyote. Vilevile ni mkatili aliyewalea watoto wake kikatili. Anawaadhibu watoto wake kwa kuwapiga sana kwa fimbo, akiwa amewatia katika gunia lililokuwa limetiwa upupu. Kwa tabia hii watoto walikimbia na kujificha hasa alipokuja akiwa mlevi (Uk. 15).

Hathamini sana masomo ya watoto wa kike. Kwa hivyo shule zinapofungwa anaanza kufanya mipango ya kumpasha Tumaini tohara, kisha amuoze bila mapenzi yake. Jambo hili ni kinyume na sheria ya haki za watoto (2001) inayopinga ukeketaji wa watoto. Masumbuko analiona hili kama jambo la lazima ambalo haliepukiki kamwe. Anakataa ushauri wa Bi. Halima na akamgombeza kwa kutaka kukiuka utamaduni (Uk. 24). Hata wazee wenzake wanapojaribu kumshauri ili atupilie mbali mila hii, anakataa kabisa.

Tumaini hakuogopa kupashwa tohara, lakini alijua baada ya tohara hangeruhusiwa kuendelea na masomo, angeozwa mara moja kama wanavyofanyiwa wasichana wengine pale kijijini kwao. Ni msichana mwenye heshima nyingi kwa babake, anapojaribu kuongea naye ili aelewe lengo lake la

kuendelea na masomo Mzee huyo anakataa. Tumaini anajihusisha na wasichana wanaopinga sana tohara na hangekubali kupashwa kwa vile jambo hili ni kinyume na msimamo wake. Anafikiria kuwa hata mamake angemsaidia. Lakini akatambua kuwa hata yeye anaendelea na mipango ya kumtafutia mwanamke ambaye angekuwa somo wake baada ya kupashwa tohara. Kwa hivyo hakuwa na lingine ila kutoroka kwao. Anateseka kihisia kwa vile hana na uhakika kama mamake mdogo na mjombake wangemuelewa na kumsaidia. Anaona kuwa wana mzigo wa kumuelimisha mtoto wao Riziki. Pia anapinga ndoa za mapema alizoziona kama pingamizi kubwa kwa kujitegemea kwa wanawake (Uk. 99). Mazingira ya nyumbani yamechorwa kama mojawapo ya mahali patendekapo dhuluma kwa watoto.

Dhuluma zinaendelezwa na wazazi halisi. Baadhi ya wasichana kama Zena, waliozwa kwa nguvu kwa wazee wa rika la baba zao ili wazazi wapate mali (Uk. 32). Pia dadake Tumaini, Mashaka aliozwa kwa lazima kwa Mzee Lusimbo na babake akapokea mahari. Kutokana na ndoa hiyo ya mapema na ya lazima, ilisababisha madhara makubwa ya kimwili kwa Mashaka. Kwa ajili ya tofauti kubwa ya umri, wakawa hawasikilizani kabisa. Kutokana na umri mdogo alipata matatizo ya uzazi yaliyodhalilisha afya yake. Nduguye mdogo Idi naye akaendelea kumdhulumu Tumaini kihisia. Huyu anamranda sana babake kwa sura na vitendo. Anawaona dada zake kama watumishi pale nyumbani. Anawaambia hadharani kuwa wao ni bidhaa za uwekezaji pale nyumbani.

Kuwaweka dada zake katika kiwango kimoja na bidhaa zozote za uwekezaji kama mbuzi na ngombe ni kuwadhalilisha pakubwa. Alipomkuta Tumaini kwa Halima alikotorokea, aliendelea kumrushia maneno ya dharau "yapi hayo, si utaolewa tu" (Uk. 27). Kwa maneno hayo Idi ana mwelekeo sawa na babake kuwa masomo ya msichana si muhimu kwa vile lazima angeolewa hatimaye. Kwa Tumaini, masomo ni muhimu ili aweze kujitegemea na kuboresha maisha yake.

Shuleni pia ni mahali pengine ambapo dhuluma hutendeka kwa watoto. Dhuluma hizi hufanywa na watoto wengine pamoja na waalimu. Shule zilipofunguliwa watoto wa darasa la Tumaini wanayapata yaliyotendeka wakati wa likizo. Wengine wanamsema kichinichini na wengine kama Kijungwe wanamtania wazi kwa kutoroka kupashwa tohara na kutorokea kwa mamake mdogo. Baadhi ya waalimu nao kama mwalimu wa Hisabati anawakata wanafunzi wake tamaa kama vile Almasi kwa kuchora sufuri na kuitia macho na masikio wanapoanguka mazoezi ya hesabu. Kwa ajili ya kitendo hiki wanalichukia somo hilo pamoja na mwalimu mwenyewe. Wengine kama Mwalimu Mkuu, Bw. Majaaliwa, anawakataza wanafunzi wa kike dhidi ya kujaza masomo ya Sayansi. Anaamini kuwa hawawezi kufanya vyema katika masomo ya Sayansi. Kama Tumaini hangekuwa na msimamo thabiti angenyimwa nafasi ya kuzaja Utabibu na angekosa kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari.

Hata baada ya kutoroka nyumbani, Mzee Masumbuko anaendelea na juhudi za kutaka kugandamiza juhudi za Tumaini za masomo. Anamhonga Chifu Andrea ili ahakikishe kuwa Tumaini hakuwa miongoni mwa wanafunzi ambao wangepata ufadhili wa serikali (Uk. 77). Baada ya juhudi hizo kuambulia patupu, akaanza kumtafutia Tumaini mchumba ili amuoze. Anatarajia kumuoza mbali kwa Mabruk kijana wa rafikiye mmoja Mzee Suleimani (uk. 50). Lengo lake ni kuepuka aibu ya kumuweka nyumbani msichana ambaye hajapashwa tohara. Kwa mawazo yake, aibu hiyo ni kubwa na angeiepuka tu kwa kumuoza mbali na kwao. Hakuweza kufanya hivyo kwa kuzuiliwa na Shaaban pamoja na Halima na Yusufu.

Nazo dhuluma za kimapenzi zinajitokeza pia. Chifu Andrea ana mtindo wa kuwatongoza waajiriwa wa kike wa nyumbani kwake. Tumaini anajikuta katika matata hayo anapoomba kazi kwake. Chifu huyo alianza kwa kumletea zawadi ndogo ndogo. Siku moja alimjia na kutaka kumbaka. Makelele aliyoyapiga Tumaini ndiyo yaliyomwokoa.

Ni jambo la aibu na utovu wa adabu kwa Mzee mwenye cheo kama Chifu, kutaka kufanya mapenzi na msichana wa rika la mtoto wake, ilhali ana mke. Jambo hili linaonyesha kuporomoka kwa maadili na matumizi mabaya ya mamlaka. Vilevile kijana wake Majuto alifanya juhudi za kumbaka Tumaini, lakini hakufaulu. Haya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

yanaonyesha kuwa watoto wamezingirwa na hatari nyingi, nyumbani na hata shuleni.

Mwandishi anawalaumu wazazi hasa baba na jamii ya wanaume kama vile Idi, Majuto na Andrea kuwa miongoni mwa wanajamii wanaowadhulumu watoto. Kuna wachache wanaopinga dhuluma kama vile Yusuf na Shaaban. Pia, wazee wa kijiji cha Mbuyuni wanaomshauri Masumbuko ili atupilie mbali msimamo wake wa kuwapasha watoto tohara,ni mfano mzuri wa wanaokubali mabadiliko ya kijamii na kutilia maanani elimu ya watoto.

### 4.3 Ulinganifu

#### 4.3.1 Aina za dhuluma

Waandishi hawa wote wa kike na wa kiume wanakubaliana kuwa kwa kweli watoto wanadhulumiwa. Dhuluma zinazowakumba ni za aina zote kama zile za kihisia, kimapenzi, zinazosababisha majeraha katika viungo vya mwili na kutotunzwa. Baadhi ya dhuluma hutekelezwa kutokana na misingi ya ufuasi wa utekelezaji wa kanuni za kitamaduni, na zingine hutokana na tabia za wadhulumu baadhi ya zingine. Wote wameshughulikia kwa mapana na marefu dhuluma za kihisia ambazo zinatokea sambamba na dhuluma za aina zingine. Ingawa matokeo ya aina hii huenda yasijitokeze hadharani au wakati huo huo, athari zake huweza kumwumiza mtoto kwa muda mrefu hata akiwa mtu mzima. Wamitila (2006) na Walibora (1996) wamewatumia watoto mayatima, kuelezea

aina za dhuluma zinazowakabili wanapoishi na jamaa zao baada ya vifo vya wazazi wao. Nao Momanyi (2006) na Burhani (2004) wanawatumia watoto ambao baadhi ya wazazi wao wangali hai. Dhuluma wanazozipata zinatekelezwa na wazazi wenyewe katika mazingira ya nyumbani. Katika Tumaini dhuluma zinatekelezwa na babake na mamaye. Zingine kama anavyoeleza Burhani (2004) zinatekelezwa na jamaa ambao wana uhusiano wa karibu sana na wazazi. Tamaa na ubinafsi zinajitokeza kama kichocheo cha utekelezaji wa dhuluma.

### 4.3.2 Utegemezi

Hali ya utegemezi wa wazazi au jamaa wanaowatunza imesisitizwa na waandishi wote kama mojawapo ya sababu za utekelezaji wa dhuluma. Watoto huwategemea wazazi au jamaa kuwatimizia mahitaji ya kila siku. Hali hii ya kutoweza kujitegemea maishani huwafanya wanaowalea kuona kuwa wana wajibu wa kuwaamulia baadhi ya masuala muhimu. Baadhi ya mengine yanatekelezwa kwa nguvu, kwa mfano katika riwaya ya *Tumaini,* Mzee Masumbuko anataka kumpasha Tumaini tohara na kumtafutia mume hata kabla ya kumaliza masomo yake. Anakataa maombi ya Tumaini ya kumruhusu aendelee na masomo. Jambo hili linaonyesha kuwa ni muhimu kutilia maanani yale yanayosemwa na watoto ingawa wana umri mdogo. Naye Mam' Peter katika *Yatima,* anaamua kulibadilisha jina la Katiwa na kumwita Mary, ilhali yeye hakuwa mzazi wake au hata hakujaribu kumshauri. Naye Walibora katika *Siku Njema* , anamtumia Kongowea kuonyesha ongezeko la mzigo wa utunzaji katika nyumba ya Kitwana, mjombake. Ongezeko hilo linasababisha matusi na

kufanyishwa kazi ili afidie chakula anachokula. Njia hii anayoitumia Mwanasaumu ni njia isiyo wazi ya kumfukuza Kongowea nyumbani kwake.

### 4.3.3. Mabadiliko ya kiuchumi

Waandishi hawa wa kike na wa kiume, wamegusia uhusiano wa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kama mojawapo ya hali zinazochangia katika utekelezaji wa dhuluma. Kama anavyoeleza Engels (1972) kuwa mabadiliko ya hali za kiuchumi katika baadhi za nchi kutoka mfumo wa kijamaa hadi wa kibepari hubadilisha muelekeo wa wanajamii. Jambo hili analolieleza ndilo linalobadilisha maneno ya watu wakaanza kuweka mahitaji yao mbele na yale ya jamii yakawekwa mwisho. Kama anavyofafanua mwandishi huyu, tamaa huweza kuchipuka. Ingawa hali hii haiepukiki waandishi hawa wanaonelea kuwa watoto ni mali ya jamii nzima wanaofaa kutunzwa bila kudhulumiwa.

Kwa kumtumia mhusika Umari, katika *Kipimo Cha Mizani* anaonyesha kuwa hali ya kujikimu katika maisha ya mjini yanamfanya Umari akose kujikimu vilivyo. Ingawa yeye na bibi yake w wameajiriwa, wanaishi maisha yanayopita mapato yao. Mkewe ni mhitaji wa vitu ghali kama gari, mifuo ya aina aina na nyumba nzuri. Kwa hivyo tamaa ya kutwaa mali ya nduguye inamwingia baada ya nduguye kuaga dunia. Naye Wamitila, anamtumia shangazi na rafikiye mmoja walioanzisha biashara ya kuwachukua watoto kutoka vijijini na kuwapeleka kwa waajiri wanaohitaji watumishi huko mijini ili waweze kujikimu kimaisha huko

mjini. Ingawa ukeketaji wa wasichana umepigwa marufuku, Masumbuko katika *Tumaini* haoni kuwa jambo hili linafaa kufuatwa. Anang'ang'ania kufuata kanuni hiyo ya kitamaduni ingawa imepitwa na wakati. Vilevile uozaji wa watoto kwa nguvu unajitokeza kama dhuluma dhidi yao. Jamii inachukulia kuwa mzazi ana wajibu wa kuwaadilisha watoto kwa njia zote. Inadhihirika kuwa matumizi ya nguvu iliyopita kiasi dhidi ya watoto ni dhuluma. Katika *Tumaini* Masumbuko anachukulia kuwa kuwaadhibu watoto wake na kuwatengea majukumu maalum ni kuwaandaa kwa maisha ya awali.(uk16) Ukatili anaoutekeleza kwa watoto wake na juhudi za kutaka kukatisha masomo ya Tumaini ni kinyume na matakwa ya jamii hiyo. Anasomewa vikali na mkuu wa tarafa kwa kutaka kukatisha masomo ya mtoto huyo.

### 4.3.4 Wadhulumu

Waandishi hawa wanalingana katika kumulika wanajamii wanaohusika katika utekelezaji wa dhuluma. Wanashikilia kuwa watoto wengi hudhulumiwa zaidi na jamaa zao kuliko wazazi wao halisi. Yale yanayotekelezwa na wazazi, wao wenyewe, hayafanywi yakiwa na lengo la kuwaumiza au kuwadhulumu watoto wao, bali hujaribu kufuata kanuni za kijamii. Katika *Tumaini* Masumbuko haoni yale anayowatendea watoto wake kuwa mabaya. Bi. Halima anapojaribu kuzungumza naye ili abadili tabia yake anamtusi na kumshtumu kwa kutaka

kuvunja utamaduni wao. Lakini kejeli za vijana wa darasa lake Tumaini kama vile Kijungwe yanadhamiria kumcheka wazi kwa kuogopa na kutoroka kwao ili asipashwe tohara. Nduguye Idi naye anajiona kama mtoto bora kwa wazazi wake kuliko dada zake. Hakukuwa na uhusiano kati ya Chifu Andrea na Tumaini. Kwa ukosefu wa uhusiano wowote haoni kama ni vibaya kumbaka ingawa ana umri mdogo. Katika *Siku Njema,* hakukuwa na uhusiano wa kidamu kati ya Kongowea na Mwanasaumu, na Selemani Mapunda. Waandishi wanashughulikia suala la mabadiliko katika mifumo ya kijamii na kiuchumi. Chini ya mfumo wa kijamaa, watoto ni mali ya jamii nzima, lakini ubepari huleta uchoyo na ubinafsi ambapo kila mtu hujali mtoto wake binafsi. Kwa ajili ya mabadiliko haya Mwanasaumu hangeweza kumhurumia Kongowea kwa ajili ya kifo cha mamake. Anamuona kama kupe kwa kuendelea kulishwa na hakuwa mmoja wa watoto wake. Maovu anayomtendea Kongowea kama kumtusi, kumfanyisha kazi nyingi na kutaka kumuua kwa sumu anayatenda kimaksudi akilenga kumdhuru Kongowea.

Naye Wamitila katika *Yatima,* anasisitiza kuwa Katiwa anazipata dhuluma nyingi akiwa nyumbani kwa Mam' Peter, kuliko akiwa kwa shangazi au kwa babu. Uhusiano kati ya Katiwa na mama huyu ni wa mwajiri na mwajiriwa. Mwajiri huhitaji mwajiriwa wake afanye kazi nyingi kwa vile anamlipa pesa. Hata aliporipotiwa na Katiwa kuwa alikuwa anaugua hakusikiliza, aliendelea kumwongezea kazi. Ingawa hapo mwanzoni babu yake Katiwa alionyesha

ukosefu wa utu, alibadilika akampenda sana;hakumpiga wala kumtesa kama mama huyu. Katiwa alikuwa akiyafurahia maisha alipokuwa akikaa na shangazi yake. Anatarajia kurudi huko akacheze na Kelvin na Maria. Jambo hili linatuonyesha kuwa shangazi hakuwa akimdhulumu. Hata maisha yanapokuwa magumu anaamua kumrudisha kwa babu yake ambako anatarajia kuwa angetunzwa vizuri.

### 4.3.5 Masuala ya haki za watoto

Pia kuna ulinganifu kati ya waandishi wa jinsia zote katika kushughulikia masuala yanayohusu haki za watoto. Haki hizo zinaambatana na maafikiano ya Muungano wa Umoja wa Kimataifa kama yalivyofikiwa tarehe 20/11/1959 (Kabeberi 1990). Maafikiano hayo yalitokana na umuhimu wa kimataifa wa kutetea haki za wanadamu wakiwemo watoto. Baada ya maafikiano hayo ya kimataifa nchi husika za muungano huo, ikiwemo Kenya, zilianza kutunga sheria ili kulinda haki za watoto. Kulingana na sheria ya haki za watoto (2001), haki zinazotiliwa maanani sana ni elimu, ulinzi wa watoto dhidi ya ukatili na mila zilizopitwa na wakati baadhi ya zingine. Utetezi wa haki hizi unatiliwa maanani na wasanii hawa. Momanyi katika riwaya ya *Tumaini*, anaonyesha juhudi za serikali za kutilia nguvu elimu ya watoto. Baadhi ya watoto wanaofanya vyema wanapewa ufadhili wa serikali katika shule za upili. Maafisa wa utawala kama Mkuu wa Tarafa, anamkemea Chifu Andrea na kumuonya kuwa atapoteza

wadhifa wake kama akiendelea kushirikiana na wazee kama Masumbuko ili kuzorotesha elimu ya watoto wa kike.

Umuhimu wa masomo haya unapatikana pale Tumaini anapoweza kuwasaidia dada zake ambao hawakusoma. Juhudi za babu katika *Yatima* zinadhihirika kwa kuamua kuwauza mbuzi na kondoo ili mjukuu wake asome. Anayatimiza kwa kuwapeleka shule pamoja na Mule na akachukua jukumu la kuwachunga mifugo. Katika *Mwisho Wa Kosa*, watoto wa Amini wanaathirika sana wanapozuiliwa kwenda shuleni ingawa binamu zao wanaendelea na masomo yao. Haki inatekelezwa baadaye Bi. Rehema anapowachukua na kuwapeleka shuleni. Wasiwasi unawaisha na furaha kuwarudia.

Vile vile wamedhihirisha kuwa watoto wenyewe wana uwezo wa kutambua kuwa wanatendewa dhuluma na wao hujibu dhuluma hizo kwa njia mbalimbali. Majibu hayo tunaweza kuyachukulia kama kupinga dhuluma hizo. Momanyi na Walibora, wanaonyesha kuwa watoto wanatoroka au kuhama nyumbani na kwenda kuishi mahali pengine. Mhusika Tumaini anahama kwao akaenda kuishi kwa mamake mdogo, Bi. Halima. Naye Kongowea anahama Tanga kwa Mjombake akaenda Mombasa ili atorokee udhalimu wa Mwanasaumu na Selemani. Naye Burhani anaonyesha kuwa, Ali anatoroka kwa ami yake na kwenda kumtafuta mamake. Ingawa alirudi alipokosa kufanikiwa, moyo wake haukutulia. Mama yao alipokuja na kuchukuliwa na polisi waliendelea kulia

mfululizo hadi walipofukuzwa na Mariyamu. Naye Katiwa katika *Yatima,* anajitetea vikali anaposingiziwa wizi na Peter kwa kumwambia mamake Peter:

> "Mimi sijawahi kuiba hata siku moja" (Uk. 63)

Maneno haya yanaonyesha uchungu anaohisi Katiwa kwa kusingiziwa kosa ambalo hakulifanya na aliyelifanya analindwa na mamake na lawama zinamjia yeye.

### 4.3.6 Unyonyaji wa watoto.

Sula la unyonyaji wa watoto linaonyeshwa kama mojawapo wa uovu wa kijamii na dhuluma kwa watoto. Watoto hunyanyaswa kwa kuajiriwa kama wasaidizi wa kazi za nyumbani au kufanyishwa kazi nyingi zilizopita umri wao. Wamitila anamuonyesha shangazi akimpeleka Katiwa kwa Mam' Peter, akamfanyie kazi. Masikilizano ya mshahara yanafanywa kati ya shangazi na Mam' Peter. Shangazi ndiye anayelipwa mshahara wa Katiwa hata Katiwa hajui kuwa shangaziye ndiye anayechukua pesa zake. Kazi anazotakiwa kufanya za kupika, kuosha na zingine zilnamchosha sana. Pia anapokosa hupigwa sana na mama huyo. Naye Walibora anaeleza kuwa Mwanasaumu anamfanyisha Kongowea kazi nyingi huku watoto wake mwenyewe wakikaa bure. Anapoajiriwa, Kongowea alianza kumpa nusu ya pesa alizokuwa akipata. Mwanasaumu alikuwa akipata pesa nyingi kutokana na kazi yake ya ususi na kukubali kupokea pesa kutoka kwa Kongowea tunauchukua kama unyonyaji wa watoto.

## 4.4 Tofauti

### 4.4.1 Wanaowadhulumu watoto zaidi

Kuna tofauti kadhaa kati ya waandishi hawa wa kike na wa kiume kuhusu wanavyoendeleza maudhui haya ya dhuluma. Kuhusu wanaoshiriki zaidi katika dhuluma, waandishi wa kiume wanawalaumu wanawake kama wanaoendeleza zaidi dhuluma. Nao wanawake wanasisitiza kuwa chanzo cha dhuluma ni wanaume, mbali na kuzitekeleza wao wenyewe. Jambo hili linatokana na misingi ya kibinafsi ya mwanadamu ya kutotaka kulaumiwa, kwani nyani haoni kundule. Walibora anamtumia Mwanasaumu kudhihirisha ukweli huu. Kitwana ambaye ni mwanamume anaonyeshwa kama mtu mzuri asiye na uovu wowote. Bibiye Mwanasumu anaonyeshwa akiwa muovu zaidi, anayemtusi Kongowea hadharani na kumlisha makombo, pia anayefanya juhudi za kumwimbia urithi wake. Vilevile anataka kumuua kwa sumu. Kitendo cha Vumilia cha kumfumania Kongowea anapooga, pamoja na Amina kutaka kufanya mapenzi na Kongowea kunaelekeza lawama kwa wanawake kwa kuwa wadhulumu wa watoto zaidi ya wanaume.

Naye Momanyi katika *Tumaini,* anawaonyesha wahusika wafuatao wanaume kama wadhulumu wa watoto: Masumbuko, kwa kuwapiga watoto kidhalimu na kutaka kuwaoza ili apate mali, Chifu Andrea kwa kuwabaka waajiriwa wa kike wa nyumbani kwake ili kutimiza mahitaji yake ya kimapenzi. Mwanawe Majuto kwa kutaka kumbaka Tumaini, Idi kuwadharau dada zake kama baba yake. Pia

Kijungwe kwa kumcheka Tumaini wazi kwa kutoroka tohara na mwalimu Majaliwa kwa kumkataza Tumaini asijaze masomo ya sayansi. Wahusika wa kike kama Bi. Halima wameonyeshwa kama wenye mapenzi kwa watoto, mamake Tumaini anabadilika na kuamua kuvumilia kupigwa na mumewe kwa ajili ya masomo ya mwanawe Tumaini.

Naye Wamitila katika *Yatima*, anawalaumu Mam' Peter na shangazi ambao ni wanawake kwa mateso yote anayopata Katiwa. Taabu anazozipata kwa mama huyu anazipata kwa vile shangaziye ndiye aliyempeleka akafanye kazi huko. Naye Mam' Peter akazitekeleza kwa kutaka ahudumiwe ipasavyo kwa vile anatoa pesa kila mwisho wa mwezi. Pia mamake Mwila analaumiwa kwa kumdhulumu Mwilu ilhali babake Mwilu anaonyeshwa kama mwenye mapenzi kwa watoto wake wote. Ingawa babu anapinga kukaa na Katiwa hapo mwanzo, baadaye anamuonyesha mapenzi makubwa kwa kumtunza na kumpeleka shuleni. Burhani anasisitiza kuwa chanzo cha dhuluma za watoto wa Amini ni Umari. Yeye anakubali ushawishi wa mkewe wa kuchukua mali ya Amini anapoaga dunia. Yeye anaona kuwa watoto hao ni wadogo na ni lazima wamhitaji mama yao, lakini hakuweza kupinga ushawishi mkubwa wa mkewe. Kama angekataa katakata, Halima angeendelea kukaa nyumbani kwake pamoja na watoto wake. Pia watoto hawangeteseka kama walivyoteseka alipowachukua kwake nyumbani.

### 4.4.2 Aina za watoto wanaodhulumiwa zaidi

Pia kuna tofauti kuhusu aina za watoto wanaoshughulikiwa na waandishi wa kike na wa kiume. Waandishi wa kike kama Momanyi na Burhani wanawashughulikia watoto walio na wazazi wao. Watoto hawa wana wazazi halisi wa kuwategemea maishani kwa mahitaji ya kila siku. Tumaini na dada zake walikuwa na wazazi ilhali baba yao alikataa kuwaelimisha na kuamua kuwaoza. Ali na nduguze wanatolewa na Umari katika matunzo ya mama yao, akawapeleka kwake ili aweze kutumia sababu hiyo kutwaa mali ya baba yao. Kwa hivyo inabainika kuwa wasanii hawa wanasisitiza kuwa baadhi ya dhuluma zinazowakumba watoto zinasababishwa na binadamu wenyewe ili waweze kutimiza malengo yao ya kibinafsi. Nao waandishi wa kiume, Wamitila na Walibora wanawatumia watoto mayatima. Kongowea katika *Siku Njema,* anakuwa yatima baada ya kifo cha mamake. Pia Katiwa, katika *Yatima* anakuwa yatima baada ya wazazi wake kuaga dunia akiwa mdogo sana. Ni dhahiri kuwa, dhuluma zinazowakumba watoto hutokana na hali ya Kudura isiyoepukika. Hali hii hutokea baada ya vifo vya wazazi. Tofauti hizi zinaonyesha kuwa hakuna ukubalifu kamili kati ya waandishi wa kiume na wa kike kuhusu watoto wanaodhulumiwa zaidi.

### 4.4.3. Ukubalifu wa tatizo hili

Kuna tofauti kuhusu ukubalifu wa kuweko kwa tatizo hili katika jamii. Wasanii wanaume ni kama hawaoni tatizo hili na hawalishughulikii kwa uzito zaidi. Nao

wasanii wa kike wanalichukulia kuwa tatizo muhimu na wanalisawiri kwa uzito zaidi kuliko wenzao wa kiume. Jambo hili lina misingi yake katika mfumo wa kuumeni ambapo wanaume hupuuza masuala yanayohusu wanawake na watoto (Dempey 1992). Katika *Yatima,* Babu haamini kuwa Katiwa kafanyiwa maovu hayo yote. Alipokuwa akielezwa alikuwa "akitikisa kichwa chake kwa kutoamini aliyoyasikia" (Uk. 76). Tunachukulia kuwa kutikisa kichwa huku ni kwa kutoamini, alifikiri yalikuwa yakitiliwa chumvi mno. Naye Kitwana katika *Siku Njema,* alishtuka alipoambiwa na Kongowea kuwa angetaka kuondoka Tanga na kuuliza "wataka kuondoka hapa kwa sababu ya huyu mwanamke?" (Uk. 39).

Usemi huo unaonyesha kuwa yale Mwanasaumu aliyokuwa akiyafanya yalikuwa mambo madogo ambayo hayangefaa kumtorosha. Kitwana alisisitiza kuwa Kongowea angeendelea kukaa pale ingawa bibi yake hakuwa akiyapendelea. Kwake Kitwana, hilo ni jambo dogo likilinganishwa na mengine ambayo Mwanasaumu alikuwa ameyatenda kama vile kumtenganisha na ndugu yake Salim.

Waandishi wa kike kama Momanyi, wanalionyesha tatizo hili kwa mapana na marefu. Kwa kuwatumia wahusika Tumaini na dada zake na kuonyesha dhuluma zinaizowakabili nyumbani kwao ambazo zinaathiri vibaya maisha ya dada zake. Ufanisi wa Tumaini baada ya kuhepa kutendewa dhuluma unaonyesha msisitizo

wa mwandishi kuwa dhuluma ni kizuizi kikubwa katika ufanisi wa maisha ya watoto.

## 4.5 Suluhu za dhuluma dhidi ya watoto

Kuna baadhi ya hatua zilizopendekezwa na waandishi hawa ili kutatua tatizo hili la dhuluma dhidi ya watoto. Galdstorm (1979:340), anaonelea kwamba suluhisho la tatizo hili ni muhimu ili kuimarisha maisha ya watoto katika jamii. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni uundaji wa vyama vya kutetea maslahi ya watoto. Vyama hivi vikiundwa huweza kuwatetea na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo viovu vya jamii. Katika *Tumaini* ,Mwandishi amefaulu kumtumia mhusika Bi. Halima katika kuendeleza hoja hii. Ni mmoja wa wanawake wakereketwa wanaohusika na vikundi vya akina mama vya kupinga udhalimu dhidi ya vijana wa kike (Uk. 46). Kikundi chao kiliitwa Jitihada Womens' Group. Kupitia kikundi hiki, akina mama wanashauriana jinsi ya kukomesha udhalimu. Kwa hivyo hii ni mojawapo ya juhudi za pamoja zinazohitajika. Pia Wamitila katika *Yatima,* anamtumia mhusika Bettina ili kufanikisha hoja hii. Ni mwanachama wa kikundi kinachochunguza jinsi watoto wanavyoteswa na kusumbuliwa katika miji mikubwa (Uk. 71). Kwa kuhusika katika kikundi hiki, anaweza kumsaidia Katiwa anapofukuzwa na kumrejesha kwa babu yake. Ingawa vikundi hivi ni muhimu, juhudi za pamoja za wanaume na wanawake zinatakikana ili kupiga vita vitendo vinavyowadhulumu watoto.

Jamii ina wajibu wa kuwashauri wanajamii wengine wanaotekeleza dhuluma dhidi ya watoto. Ushauri huu ni wajibu wa wanajamii wote wakubwa kwa wadogo. Momanyi katika riwaya ya *Tumaini,* anatoa mfano wa Bi. Halima anajitahidi kumshauri Mzee Masumbuko ili atupilie mbali mipango ya kuwapasha tohara watoto wa kike. Ingawa Mzee huyo hakumsikiliza, juhudi zake ni za kupewa heko. Wazee wa kijijini pia wanamketisha chini Mzee Masumbuko wakimshauri ili aungane nao katika kubadilisha tabia zilizopitwa na wakati. Hata hivyo anakataa katakata. Pia Tumaini mwenyewe anajaribu kushauriana na babake ili amwelewe. Juhudi hizi za pamoja zikizingatiwa zinaweza kupunguza tatizo hili.

Pia ni wajibu wa jamaa kuchukua jukumu la kuwasaidia watoto wanaodhulumiwa. Hatua inayochukuliwa na Yusuf na mkewe Halima ya kumsomesha Tumaini anapotorokea kwao inayaokoa maisha yake. Kama si usaidizi wao, elimu yake ingekatishwa ghafla na kuishi maisha ya ufakiri. Katika *Yatima,* Bettina anakuwa amemtafutia Katiwa ufadhili ili aende sheleni huko mjini. Usaidizi aliompa Katiwa ulimrejeshea furaha aliyoikosa akiwa kwa Mam' Peter.

Juhudi za serikali nazo zinahitajika ili kutunga sheria mwafaka zinazoweza kulinda haki za watoto. Mojawapo ya sheria hizi ni ile inayoelezwa na Momanyi, katika *Tumaini* kuwa, serikali ilipiga marufuku tohara kwa watoto wa kike.

Tumaini alijua kuwa ni haramu kumlazimisha apashwe tohara. Mzazi ambaye angekiuka sheria hiyo angechukuliwa hatua kali za kisheria. Uhamasishaji wa jamii kuhusu hatari za kukiuka sheria hii unahitajika ili wananchi waielewe zaidi. Basi uundaji wa sheria hizi kama sheria kuhusu haki za watoto nchini Kenya ya mwaka wa 2001, ni mojawapo ya hatua muhimu za juhudi hizi. Ili kuendeleza elimu ya watoto, serikali ilikuwa ikitoa ufadhili kwa watoto watano waliofanya vyema sana katika mtihani wa shule za msingi. Walinda usalama ni sharti wahakikishe kuwa sheria hizi zinafuatwa vilivyo bila kukiukwa.

Vilevile waandishi wanapendekeza kuwa watoto wana jukumu lao binafsi la kusimama wima na kupinga dhuluma zinazowakabili. Burhani anamtumia Mtoto Ali anayeamua kupinga uwongo wa Mariyamu kuwa, mama yao ni mwendawazimu. Hata wanapopigwa na kutishwa kuwa wangeitiwa polisi, anajibu "afadhali hivyo" (Uk. 151). Jibu hili ni hatua ya kupinga dhuluma dhidi yao. Pia mhusika Tumaini katika *Tumaini* anatumia mbinu kadhaa ili kupinga dhuluma anazotendewa. Anatoroka kwao, pia anampiga Majuto kinena anapojaribu kumbaka. Pia katika *Yatima* Katiwa anajitetea na kupinga vikali maneno ya Mam' Peter kuwa alikuwa mwizi. Alimjibu kuwa yeye si mwizi na hajawahi kuiba hata wakati mmoja (Uk. 63). Naye Kongowea katika *Siku Njema,* anapinga juhudi zote za Amina za kutaka kufanya mapenzi naye kwa kumjibu kuwa kitendo hicho ni haramu. Miongozo hii iliyotolewa na waandishi kama hatua mahsusi za kukabiliana na tatizo hili.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeangalia jinsi waandishi wa jinsia tofauti walivyolingana na kutofautiana katika usawiri wa maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto. Imedhihirika kuwa waandishi hawa wa kike na wa kiume wanalingana zaidi kuliko vile wanavyotofautiana. Wote wanakubaliana kuwa watoto wanadhulumiwa katika mazingira mbalimbali wanakokaa, kama vile nyumbani na shuleni. Nyumbani wanadhulumiwa na wazazi, walezi, au hata ndugu wengine. Shuleni wanadhulumiwa na wanafunzi wengine, pamoja na waalimu wao.

Imedhihirika kuwa: ubinafsi, tamaa, wivu na ufuasi wa mila za kijamii ni sababu zinazochangia katika utekelezaji wa dhuluma. Kwa kuonyesha mazingira tofauti panapotokea dhuluma waandishi wanaonyesha kuwa maisha ya watoto yako hatarini kwa vile hakuna pahala ambapo pana utulivu kamili. Kwa kuonyesha wadhulumu mbalimbali wa watoto, waandishi wanataka kuonyesha kuwa tatizo hili linafaa kusuluhishwa ili wadhulumu warekebishe tabia hii.

Kuna tofauati chache kati ya waandishi hawa, kama vile, waandishi wa kiume kutolipatia uzito mkubwa suala hili na waandishi wa kike kulipatia uzito mkubwa. Pia kumekuwa na tofauti kuhusu utambuzi wa wanaohusika zaidi na dhuluma, ambapo waandishi wa kiume wanawalaumu wanawake, nao waandishi wa kike

wanawalaumu wanaume kama chanzo cha dhuluma. Tunachukulia kuwa hili linatokana na hali ya kibinadamu ya kutotaka kukubali makosa yake binafsi.

Mapendekezo ya hatua mbalimbali kama yanavyopendekezwa na waandishi yametolewa. Imedhihirika kuwa sheria ya kuwalinda watoto inahitajika kutiliwa maanani ili kuwalinda watoto ipasavyo. Jamii pia ina jukumu la kuhamasisha wenzao wanaoendeleza tabia hii ili wakomeshe vitendo vya dhuluma dhidi ya watoto. Pia watoto wenyewe wana wajibu wa kupinga dhuluma wanazotendewa.

Katika sura ifuatayo tutaangalia mahitimisho ya utafiti, yatakayohusu muhtasari wa kila sura, matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa yaliyoshughulikiwa katika tasnifu hii. Pia inaonyesha matokeo ya utafiti huu kulingana na malengo ya utafiti yaliyotolewa. Vilevile, katika sura, hii mapendekezo ya tafiti zinazofaa kufanywa yametolewa.

### 5.1 Muhtasari

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto kama yanavyosawiriwa na waandishi teule wa riwaya za Kiswahili. Ulidhamiria kuchunguza aina za dhuluma zinazowakabili watoto na zinavyoweza kubainika. Pia utafiti ulidhamiria kuchunguza chanzo cha dhuluma hizo na utambuzi wa asasi zinazozitekeleza, pamoja na athari za dhuluma katika maisha ya watoto. Pamoja na hayo, ulikusudia kubainisha jinsi ambavyo waandishi wa jinsia tofauti walilisawiri tatizo hili na kuchunguza vile wanavyolingana au kutofautiana katika kuendeleza maudhui haya. Hatimaye, ulidhamiria kuonyesha mapendekezo ya wasanii kuhusu suluhu za tatizo la dhuluma dhidi ya watoto.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza inashughulikia ufafanuzi wa dhana muhimu kama zilivyotumiwa katika tasnifu hii. Pia imeshughulikia utangulizi na swala la utafiti . Vilevile maswala ya kuongoza utafiti pamoja na malengo ya utafiti yametolewa . Pia sababu muhimu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya tasnifu . Misingi ya nadharia ya ukatA tamaa na ushari iliyoongoza utafiti na mihimili yake imetolewa. Udurusu wa tafiti za hapo awali vilevile umetolewa. Hatimaye imeshughulikia njia za ukusanyaji wa data pamoja na uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili imejadili aina mbalimbali za dhuluma zinazowakumba watoto na sababu za utekelezaji wake. Aina nne kuu za dhuluma zimebainishwa na namna zinavyobainika zimeelezwa. Aina hizo kuu ni kujeruhiwa kimwili, dhuluma za kihisia, dhuluma za kimapenzi, na kutowatunza watoto. Ubainikaji wa dhuluma hizi umetolewa. Sababu za utekelezaji wa dhuluma hizi zimetolewa kulingana na zinavyojitokeza katika vitabu vilivyoteuliwa.

Sura ya tatu imechunguza wanajamii wanaotekeleza dhuluma dhidi ya watoto na athari zake. Baadhi ya watu wanaowadhulumu watoto: ni wazazi halisi na wazazi wa kambo, walezi, watoto wenyewe wanawadhulumu wenzao, waajiri , waalimu na watu mbalimbali wenye mamlaka. Athari mbalimbali za dhuluma dhidi ya watoto zimebainika.

Sura ya nne imejadili namna waandishi wa kike na wa kiume walivyolisawiri tatizo hili la dhuluma dhidi ya watoto . Imedhihirika kuwa kuna ulinganifu na tofauti mbalimbali za usawiri kati ya waandishi hawa. Wote wanakubaliana kuwa watoto hukumbwa na aina mbalimbali za dhuluma. Pia, utegemezi, mabadiliko ya kiuchumi, ni baadhi ya mambo yanayochangia dhuluma. Pia wanaeleza kuwa jamaa na walezi ni miongoni mwa wanajamii wanaowadhulumu watoto zaidi. Waandishi hawa wanatofautiana kuhusu wanaoshiriki zaidi katika kuwadhulumu watoto. Msisitizo wao kuhusu aina za wa watoto wanaodhulumiwa zaidi, hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo zimejadiliwa kama zilivyopendekezwa na waandishi. Hizi ni pamoja na uhamasishaji wa jamii, uundaji wa makundi ya kijamii ya kupinga vitendo hivi na wajibu wa serikali wa kutunga na kuhakikisha kuwa sheria za kuwalinda watoto zinafuatwa ipasavyo.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu . Muhtasari wa kila sura umetolewa . Pia, inatoa maelezo ya matokeo ya utafiti kulingana na maswali ya utafiti yaliyoongoza utafiti huu . Vilevile, sura hii imetoa mapendekezo ya tafiti zinazoweza kufanywa katika siku zijazo.

## 5.2 Matokeo ya utafiti

Katika riwaya zilizoteuliwa imebainika kwamba, maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto yamejitokeza. Dhuluma hizi zote zinaweza kugawika katika vikundi vinne. Hivi ni kulingana na nadharia iliyoongoza utafiti kuwa kuna

ushari wa siri na wa wazi. Dhuluma zinazoathiri viungo vya mwili hutokana na kupigwa kwa kutumia vifaa mbalimbali kama vile: mijeledi, fimbo au vifaa vingine vinavyoweza kuumiza mwili. Pia, matumizi ya mikono kwa kuvuta masikio, kupiga kofi au adhabu zilizopita kiasi . Dhuluma hii hutokana na hasira ya ghafla. Adhabu hutolewa baada ya kutambua kuwa mtoto amefanya kosa fulani linalohitaji adhabu ya papo kwa hapo. Ufuasi wa kanuni za kijadi kuwa mzazi au mlezi ana wajibu wa kumtia mtoto adabu akosapo. Wengine huwaadhibu watoto kwa ajili ya wivu dhidi yao. Dhuluma hii hubainika kwa kuwepo kwa majeraha katika miili ya watoto, mwendo wa kujiburura kwa ajili ya uchungu, na wengine husita kwenda nyumbani kwao na wengine huwaogopa watu wazima. Majeraha husababisha uchungu mwingi na wengine hulia kila wanapotendewa maovu hayo.

Vilevile watoto hukumbwa na dhuluma za kimapenzi zinazotokea kwa kubakwa, kuingizwa katika uhusiano wa kimapenzi na watu wazima, kupapaswa na ndoa za mapema. Hii hutokana na uchu wa wanaume, tamaa, au hali ya kutaka kulipiza kisasi. Wanapokabiliwa na dhuluma hii, wengine hukata tamaa maishani , huzua chuki isiyoisha kwa aliyemdhulumu. Matokeo mengine ni kuzorota kwa afya ya watoto wanaohusika . Baadhi ya dhuluma hizi hutekelezwa na wazazi halisi, wazazi wa kambo wavulana au hata wazee wazinzi. Utafiti umeonyesha kwamba

aina hii huweza kubainika kwa kupatikana kwa majeraha katika sehemu za siri za mtoto, hofu na wasiwasi.

Imebainika vilevile kuwa, watoto hudhulumiwa kihisia. Kulingana na nadharia ya ukata tamaa na ushari, hii ni aina moja ya ushari usioonekana wazi. Ushari wa aina hii kama ilivyoonyeshwa na watunzi walioteuliwa, hujitokeza baada ya watoto kutendewa mambo yasiyopendeza kama vile: matusi, kutishwa, kuaibishwa, ukosefu wa hisi za mapenzi kutoka kwa wazazi au walezi. Pia kulinganishwa na wengine, kurundikiwa lawama za kila mara na kupuuzwa baadhi ya vingine. Imedhihirika kuwa wivu, kukata tamaa, na ubinafsi ni baadhi ya misingi inayozua dhuluma hii. Huweza kubainika kwa kusikika kwa maneno ya matusi dhidi ya watoto, huzuni usoni mwa watoto, kujitenga na wengine, na wengine hutoroka nyumbani. Dhuluma hii huweza kutekelezwa na mtendaji bilakukusudia, na wengine kwa maksudi.

Kutotunzwa au kutoshughulikiwa ni aina nyingine ya dhuluma inayowakabili watoto. Kulingana na mtunzi Wamitila, ukosefu wa utunzaji bora hutokana na uchoyo au kutojali. Mifano ya dhuluma hii ni kama vile kutopelekwa shuleni, kutopelekwa hospitalini wanapougua, kutopewa maadili, kutolishwa, kukosa kulindwa ipasavyo na ukosefu wa mavazi yafaayo. Watoto huanza kufanya kazi za ajira wakiwa na umri mdogo, ukosefu wa afya bora na uchafu ni baadhi ya mambo yanayoibainisha dhuluma hii.

Sababu za utekelezaji wa dhuluma zimejadiliwa. Ufuasi wa tamaduni za kiasili umebainika kama mojawapo ya sababu kuu za kuwadhulumu watoto. Utamaduni ulimtarajia mzazi amlee mtoto hadi afikie utu uzima na kumfunza maadili ya jamii . Upashwaji wa tohara ulijitokeza kama ngazi ya kutoka utotoni na kuingia katika maisha ya watu wazima. Jamii nzima ilishirikiana ili kufanikisha mipango ya tambiko mbalimbali kama tohara. Mtoto aliyekosa kupashwa tohara alichekwa na wengine kwa kutotimiza wajibu huu. Baadhi ya wazazi nao huona aibu kwa kuwaweka watoto kama hao nyumbani na hufanya juhudi ya kuwaoza mbali ili waepukane na aibu hiyo. Upashwaji tohara umejitokeza kama mojawapo ya njia za kuwadhulumu watoto. Kutokana na hayo, utafiti huu umebainisha kuwa kuna mvutano wa kijamii kuhusu ufuasi wa utamaduni huu. Kuna kikundi cha watu kinachoonelea kuwa ufuasi wa tamaduni kama hizo umepitwa na wakati. Wengine nao wanachukulia kuwa, lazima uendelee kutekelezwa. Utafiti huu umeonyesha kuwa utekelezaji wa tambiko kama hizo ni dhuluma dhidi ya watoto kwa vile hutekelezwa bila mapenzi ya baadhi yao.

Vilevile utamaduni ulimtarajia ndugu awatunze watoto wa kakake afikwapo na mauti. Kwa hivyo, anayewatunza watoto hupata sababu ya kutwaa hata mali ya nduguze. Ingawa utunzaji wa watoto ni muhimu

baadhi ya jamaa hawalitekelezi jukumu hilo ipasavvyo. Wao hutwaa mali na kuitumia kwa mahitaji yao na kusahau kuwatunza watoto waliowarithi.

Utiaji wa adabu pia ni sababu nyingine ya kuwadhulumu watoto. Ingawa kuna njia nyingi za kuwaadilisha watoto kama vile ushauri na kutoa zawadi kwa tabia njema, baadhi ya wazazi hutumia vita, kuwanyima chakula na matusi kama njia njia za kuwaadhibu. Hata watoto wengine huishia kutumia njia hizi dhalimu kwa wenzao baada ya kuona wazazi wao wakizitumia. Ingawa ni muhimu kuwatia watoto adabu, matumizi ya nguvu na adhabu zilizopita kiasi ni vitendo vya dhuluma vinavyofaa kukomeshwa.

Watoto wengine hudhulumiwa na wenzao ili wenzao waweze kujifurahisha. Matumizi ya nyimbo za kukejeli , maneno ya dharau na vitendo vya dhuluma dhidi ya wengine hufanyika. Imebainika kuwa hata watoto huwadhulumu wenzao kwa kutosoma au kwa kutofanyiwa tambiko za kijadi. Mambo haya na mengine huwafanya waonekane wajinga mbele ya wenzao , yakawa chanzo cha ucheshi wa kujifurahisha.

Pia imedhihirika kuwa watoto wengine hudhulumiwa baada ya wazazi au walezi wao kukumbwa na ukata tamaa fulani. Hali hii inapotokea wao huonekana kama vizuizi vya kufaulu kwa malengo fulani. Kwa hivyo, dhuluma wafanyiwazo hutokea kama ushari uluohamishwa. Ingawa watoto

hawakushiriki moja kwa moja katika vitendo vilivyoleta ukata tamaa huo, wao hutumiwa kama njia ya kutolea hasira kwa waliohusika.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa ubinafsi huchangia pakubwa katika kuwadhulumu watoto. Anayedhulumu huangalia kutimiza haja zake binafsi bila kujali hisi za wengine. Hao ni kama waajiri wanaotarajia kuhudumiwa wakati wote bila kujali uchofu au afya ya wafanyakazi wa nyumbani kwao, ambao baadhi yao huwa watoto. Waajiri wengine hawasikilizi malalamiko ya waajiriwa wao. Pia imejitokeza kuwa watoto wengine huingizwa katika kazi za ajira wakiwa na umri mdogo sana ili kuwanufaisha walezi wao. Malipo yao huchukuliwa na walezi wao badala ya wao kupewa.

Pia imejitokeza kuwa watu wengine huwa na tabia ya kipekee. Wengine ni wakatili au kupendelea ukatili na wengine hawapendelei mabadiliko. Kwa ajili ya tabia hizi hawaoni ugumu wowote wakiwatendea watoto wanaowalea ukatili wowote. Pamoja na hayo , hali ya utegemezi wa watoto kwa watu wanaowatimizia mahitaji yao imedhihirika kuwa kisingizio cha walezi kujitwika mamlaka ya kuwatendea watoto kama wapendavyo. Wengine huwapiga , huwafanyisha kazi nyingi kupita kiasi na wengine huwadharau na kuwaona kama mzigo usiofaa nyumbani kwao.

Wanajamii wanaowadhulumu watoto na athari zake zimeonyeshwa katika utafiti huu. Wanajamii hawa ni kama vile: wazazi halisi na wazazi wa kambo, walezi, watoto, waajiri, watu wenye vyeo mbalimbali kama vile mahakimu, watawala na waalimu. Imedhirika kuwa watu hawa hutokana na asasi mbalimbali za kijamii. Pia wao huingiliana moja kwa moja na watoto kwa njia moja au nyingine.

Nadharia inayotumiwa katika utafiti huu inasisitiza kuwa vitendo vya ushari hulenga kumwumiza mlengwa kimwili na kihisia. Kwa hivyo, athari za dhuluma zinaweza kuchukuliwa kuwa na majeraha ya kihisia na ya sehemu za mwili. Dhuluma husababisha majeraha ya mwili kama vile: kuwasha, kuvimba na kuzoroteka kwa afya. Athari zingine ni za kihisia kama vile : huzuni isiyoisha, wengine hukata tamaa maishani na kuingilia vitendo viovu kama vile umalaya, wengine hukosa utulivu na kutoroka nyumbani kwao. Wengine huishi maisha mabaya yenye dhiki na taabu baada ya kuozwa mapema bila ujuzi wowote wa kujitegemea kimaisha. Pia dhuluma zingine husababisha magonjwa ya mwili na ya kihisia kwa wadhulumiwa. Vilevile ukuaji wa watoto huathirika kimwili na kiakili.

Katika kulinganisha usawiri wa maudhui haya, waandishi wa kike na wa kiume wanalingana na kutofautiana. Wote wanakubaliana kuwa watoto wanadhulumiwa. Hii imedhihirika kutokana na aina nne kuu za dhuluma

walizozisawiri. Aina zote za dhuluma zinaweza kuingizwa katika mojawapo ya aina hizo. Pia wanalingana katika kueleza sababu zinazopalilia dhuluma hizo kama vile: ufuasi wa tamaduni za kiasili, tamaa, ubinafsi na utegemezi. Pia wana maoni sawa kuwa wadhulumu wengi wana uhusiano wa karibu sana na watoto. Watoto huweza kuingiliana nao kwa njia moja au nyingine. Mabadiliko ya kiuchumi na ya kijamii pia yameongeza gharama ya maisha. Baadhi ya walezi wanalemewa na kubeba ulezi zaidi hasa wa watoto wasio wao.

Waandishi wote wanakubaliana kuwa masuala kuhusu ulinzi wa haki za watoto unahitajika ili kuwalinda watoto kutokana na wanajamii dhalimu. Haya ni kama vile ceria mwafaka za kuwalinda na kuhakikisha kuwa wazazi na walezi wanawatimizia watoto mahitaji yao ya kila siku .

Waandishi wa kike na wa kiume wanatofautiana katika utambuzi wa wadhulumu wa watoto. Wandishi wa kiume kama vile Wamitila na Walibora wanawawalumu wanawake kama wadhulumu wa watoto. Nao waandishi wa kike wanaelekeza lawama zao kwa wanaume. Pia aina za watoto wanaohasiriwa zaidi zinatofautina. Waandishi wa kiume wanaonyesha kuwa watoto wanaodhulumiwa zaidi ni watoto mayatima, nao wenzao wa kike wanaonyesha watoto wa kawaida walio na wazazi wao. Vilevile waandishi wa kiume ni kama hawalitilii maanani tatizo hili, wamelifunika pamoja na

mengine kama vile tamaa na ubinafsi. Wenzao wa kike wameliweka wazi hata kwa kumulika asasi tofauti zinazotekeleza udhalimu huu.

Utafiti huu umeonyesha kuwa, jamii inaweza kujumuika pamoja ili kukabiliana na tatizo hili. Uundaji wa vyama vya utetezi wa haki za watoto, uhamasishaji wa jamii dhidi ya vitendo viovu ni baadhi ya juhudi zinazohitajika ili kukabiliana na tatizo hili. Juhudi za serikali za kutunga sheria na kushurutisha utiifu wa sheria hizo zinahitajika ili kukabiliana na wanaozikiuka sheria hizo

Utafiti huu umebainisha kuwa waandishi wa kiume na wa kike wamelingana zaidi katika kulisawiri tatizo hili kuliko walivyotofautiana.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umejihusisha katika uchunguzi wa swala la dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa ili kutafiti kama maudhui haya yanajitokeza katika tanzu zingine za fasihi kama vile fasihi simulizi, tamthilia au ushairi. Vilevile utafiti wa nyanjani unaweza kufanywa ili kupima ukweli wa yale yanayoandikwa na waandishi.

## MAREJELEO


Adegbola,E.A.(1983). *Traditional Religion in West Africa.Ibadan:* Daystar press.

Aries, P. (1962). *Centuries Of Childhood.* New York: Vintage Books

Benedicts.T, Jafle S. J.(2006) *Child Abuse:Types and Symptons.Mental Health Issues* Internet publication.

Berkowitz,L.(1969) *Frustration Hypothesis Revisited.*New York:Atherton.

Bloom,L& Ottony,J(1987).*Changing Africa: An introduction to sociology.*London: Macmillan publishers.

Bolby J(1969).*Attachment and loss vol.*1New York: Basic Books.

Burgess (1979). *Child Abuse. A Situational Analysis in Advances in Clinical Child* Psychology Vol.2. New York: Plenum Press

Burhani,Z.W.(2004) *Kipimo Cha Mizani.*Nairobi: Longhorn publishers.

Buss .A.H (I961) *The Psychology of Aggression.*New York:Wiley.

Cicchetti, D. and Aber, J.K. (1980*). Abused Children - Abusive Parents. An Overstated Case?* Harvard Educational Review

Clarke,J.F.(1892) *Ten Great Religions.*Boston. J:Osgood.

Cutrufelli,M.R.(1983). *Women of Africa.Roots of oppression.*London:Zed press.

Dempey,K.(1992).*A Mans Town: Inequality between women in rural Australia.*Oxford:Oxford university press.

Disborn,M,A.et al(1977).*Measuring the components of parents potential for child abuse and neglect.*

Dollard,J;Miller,N.E; Mower,O.H Sears R.R (1939).*Frustration and Aggression.*New Haven: Yale Univ.Press.

Engels,F.(1972).*The Oigin of the Family,Private Property and the State.*New york: Pathfinder press.

Finkelhor, D.(1991). *The scope of the problem. In Gough, D.Intervening in childs sexual abuse.*Glascow:Scottish acadamic press.

Finkerhor ,D.(1984*). Child Abuse.*New York:Free Press.

Fraser, B.G. (1976). *The Child and His Parents. Child Abuse and Neglect.* Cambridge: M.A. Ballingen.

Galdstorn,R. *Preventing the abuse of little children. In abuse and violence.*U.S.A: Ams press Ltd.

Gatobu,A.Kathure(2003). *Domestic Violence in Kenya.Kenya:*Kijabe printing press.

Gelles R.J(1973). *Child Abuse as Psychopathology. A social critique and reformulation.*American journal of Arstralia pg 623-628.

George, and Main (1979).*Social interactions of young abused children:Approach avoidance and aggression.*journal on child development 50:306-318.

Gitau, E.N. (2005). *'Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili".* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta *(Haijachapiswha).*

Glaser,D.&Frosh.S. (1993) *Child Sexual Abuse.*London: The machmillan press ltd.

Goldstein, J., Freud, A. or Solnit (1973). *Beyond the best interests of the child.* New York Free Press.

Haugaad, J.& Reppuci,N.(1988). *The Sexual Abuse of Children.*London: Jossey-Babs.

Herman,J.and Hirchman,L.(1981). *Families at risk for father –daughter incest.*Amercan journal of psychiatry.138.

Holter,J. & Fredman,S. (1968) *Principles of Management in Child Abuse cases.*American journal of orthopsychiatry.1968,38.

Iwaniec, Dorota(1996). *The Emotinally Abused and Neglected Child.*England: John wiley and sons Ltd

Jones, D.N. (1982). *Understanding Child Abuse.* Chauses Press Limited. Boungay: Suffolk.

Kabeberi,Janet.( 1990). *The Child Custody, Care and Maintainance.*Nairobi: Oxford univrsity press.

Kelly,A Jeffrey(1983). *Treating child – Abusive families.*New York: plenum press

Kempe, H. (1995). *International Perspective Prospects Regarding Assault Against Chidlren in Assault Against Children.* Meier, J. San Diego California: College Hill –Press.

Kenya Gazette Supplement No 95 (2002)*The Children Act,2001.*Nairobi: Government Printer.

Kimani, C.K. (2003). *"Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili".* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (*Haiachapishwa).*

Korbind, J. (1977). *Anthropological Contributions to the study of Child Abuse and Neglect.*

Krakow,J.B.&Kopp,C.(1982):*The Child Development in a Social Context.*U.S.A: Addison-wesley publishing company inc.

Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin press.

Lynch,M.A.and Roberts J.(1982).*Consequences of Child Abuse.* London:Acadamic press inc.Ltd.

Mbilinyi,M.Mbughuni,P.Mascarenhas,O. *Wanawake wa Tanzania.Uchambuzi wa Harakati Zao za Ukombozi.*Dar Es Salaam:Dar es Salaam University press

Mbiti ,J.S.(1989). *African Religious and Philosophy.*(second revised and enlarged edition).Great Britain:Biddles ltd

Mbiti,J.S (1975) *Introduction to African Religion.* Great Britain:Whitstable Litho

Mbiti,J.S.(1992).*Introduction to African Religion.*(second edition).Nairobi: East African Publishers Ltd.

Meier, J. (1985). *Assault Against Children.* San Diego California:College Hill Press.

Meier,J.H.(1985*) Assault Against Children.*Sandiego: College hill press.

Momanyi, C. (1998). "*Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushari wa Kiswahili*'. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu Cha Kenyatta *(Haijachapishwa)*

Momanyi,C. (2006). *Tumaini* .Nairobi: Vide-Muwa.

Morgan ,J&Zedner,L.(1992) *Child victims.*New York: Oxford university press.

Namwamba A.(2005)*Kenyas young child abuse victims.in Chambers of justice* journal

Nasimiyu,A.W.(1994)*Domestic Violence Against Women.A cry for life in wholeness in pastrol care in Africa.* Nairobi: Action publishers.

Ndungo, C. (1998). *"Images of Women in Gikuyu and Literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs".* Tasnifu ya PhD.Chuo Kikuu Cha Kenyatta.*(Haijachapishwa)*

Nelson,S.(1987). *Incest and Myth.*Edinburg: Stramullion.

Obosabuley,Aguedze.(1990)*The principles Underlying the African religion and philosophy.*Nairobi:Maillu House Ltd.

Patron Nl.(1985).*The politics of Child Abuse.*Hong kong:Machmillan press ltd.

Rohner ,R.P(1986). *The Wamth Dimension:Foundations of parental acceptance-Rejection theory.*Beeverly Hills:.Sage.

Spinetta,J.& Rigler,D.(1972).*The Child Abusing Parent.A Psychological Review.*Psychological Bulletin.77.pg 296-304

Tassoni,P.(2002). *Certificate in Child Care and Education.*(third edition).Halley court:Heinman educational publishers.

Thonden, Y.(I997) Juvenile Injustice (*Police abuse and detention of street children in Kenya ).*Human Rights Watch: U.S.A.

Tomison, A.M. (1996). *Child Maltreatment and Substance Abuse.* Discusison Paper Number 2. Spring 1996. Australian Institute of Family Studies

Tucker N (1981) *The Child and the Book;A Psychological and Literary Exploration.*Cabridge:C.U.P.

Walibora,K.(1996). *Siku Njema.*Nairobi: Longhorn.

Wamitila, K.W. (2006) *Yatima.* Nairobi: Vide- Muwa



KENYATTA U[illegible]VERSITY LIBRARY